

**USAWIRI WA FAMILIA YA KISASA KATIKA
FASIHI YA WATOTO NCHINI KENYA**

**Na
Gatere Lucy Njeri**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya
mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu
cha Nairobi**

2019

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi Tarehe

Gatere Lucy Njeri

C50/85060/2016

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi Tarehe

Prof. Rayya Timammy

Sahihi Tarehe

Dkt. Omboga Zaja

TABARUKU

Kwa mume wangu Gabriel Muchoki na watoto wetu Clare Michelle Micere, Cindy Rita Kirigo na Pius Lee Kibuchi. Jitahidini kufikia kilele cha usomi kwa kuwa elimu ni mwangaza.

SHUKURANI

Ningependa kuwashukuru watu wote waliochangia katika kufaulisha tasnifu hii. Kwa hakika si rahisi kuwataja wote kwa majina yao, lakini siwezi kujizuia kuwataja baadhi yao ambao bila msaada wao tasnifu hii haingekamilika.

Mwanzo kabisa nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Dkt. Omboga Zaja na Prof. Rayya Timammy kwa jinsi ambavyo walinisaidia kuboresha kazi yangu na kujifunza mengi kuhusu jinsi ya kushughulikia suala la utafiti kitaalamu. Usaidizi wao umenifaa katika kuandika kiusomi na kwa kujamini.

Aidha, nawajibika kuwashukuru wahadhiri wote walionifundisha katika kozi hii ya uzamili na kunipa ushauri katika vikao vyta mawasilisho. Hao ni Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. P. I. Iribi Mwangi, Prof. Evans M. Mbuthia, Prof. Olali, Prof. Wamitila Kyalo, Dkt. Mwaliwa, Dkt. Michira, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Gichobi Mungania, Dkt. Jerono, Bw. Sanja Leo na Bi. Mary Ndung'u. Tasnifu hii isingekamilika bila mafunzo na ushauri wao. Asanteni nyote kwa kunivumilia na kunielekeza.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu wote tuliotiana shime kama vile akina Wairimu Mutai, Pauline Kaaria, Iman Hudaa Hamisi, Bridget Makena Mwenda, David Rachel Ndinda, Nyarunda Irene Monchari na Ndegwa David.

Hatimaye, shukurani kwa mume wangu Gabriel Muchoki na watoto wetu Clare Michelle Micere, Cindy Rita Kirigo na Pius Lee Kibuchi kwa kunitia moyo na uvumilivu wenu nilipokuwa katika shughuli za usomi.

Nyote niliowataja na wale ambao sikuweza kuwataja, Mungu awabariki.

IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza usawiri wa familia ya kisasa katika fasihi ya watoto nchini Kenya. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubainisha aina za familia zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto, kutathmini usawiri wa familia kama taasisi katika fasihi ya watoto na kuchunguza uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika hadithi za watoto. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamii ambayo ilitoa msingi madhubuti wa kutathiminia usawiri wa familia ya kisasa kwa vile imethibitika kuwa usawiri unaobainika unafungamana na hali ilivyo katika maisha ya jamii ya kisasa. Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo na ulikuwa wa maktabani. Vitabu vilivyoteuliwa vilisomwa kwa makini na data inayohusu usawiri wa familia kuchukuliwa kwa kujibu maswali ya utafiti. Vitabu vilivyoteuliwa kwa utafiti huu vilikuwa katika migao miwili; vitabu vya hadithi za watoto vilivyotungwa kati ya 2000 hadi 2010 ambavyo ni *Mwepesi wa Kusahau, Nampenda Mama wa Kambo* na *Madalala Abadilika* na vitabu vya hadithi za watoto vilivyotungwa kati ya 2011 hadi 2018 ambavyo ni *Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda*. Mgao huu wa kiuteuzi ulilenga kuangalia ni kwa jinsi gani tungo hizi zinaakisi uhalisi wa wakati katika kusawiri familia. Baada ya kuvisoma vitabu vilivyoteuliwa, muhtasari wa kila hadithi ultolewa na data kudondolewa kwa kuzingatia madhumuni na maswali ya utafiti huku maelezo yakitolewa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo na hatimaye matokeo na mapendekezo kuwasilishwa. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa aina za familia zimebaki kuwa zilezile hata vipindi vya kiwakati vinapobadilika. Aina hizo ni familia kiini na familia pana. Kuhusu usawiri wa familia, utafiti huu, ulibainisha kuwa katika kipindi cha awali familia ilisawiriwa kama ambayo inashughulikiwa na mama zaidi ya baba kuhusu malezi ya watoto. Hali hii inaendelea kubadilika katika kipindi cha sasa ambapo baba katika familia anasawiriwa kama anayeshughulikia majukumu yake vilivyo. Kwa mtazamo wa nadharia ya uhalisia, usawiri huu ulionekana kuwa na uhusiano mkubwa na familia halisi katika jamii. Kutokana na matokeo ya utafiti huu inapendekezwa kuwa usomaji wa fasihi ya watoto shulenii usiwe wa burudani tu lakini utilie mkazo ujenzi wa mitazamo chanya mionganii mwa watoto wakiwa wangali wadogo kuhusiana na usawiri wa familia. Makuzi ya watoto na ufunzaji wa maadili ni mambo yawezekanayo sio katika misingi ya familia tu bali pia kupitia mafunzo ya fasihi ya watoto. Aidha, inapendekezwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu usawiri wa familia katika nyakati za awali kabisa.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU	iii
SHUKURANI.....	iv
IKISIRI	v
YALIYOMO.....	vi
MAELEZO YA ISTILAHINI NA VIFUPISHO VYA MANENO.....	ix
SURA YA KWANZA	1
1.1 Usuli wa mada	1
1.1.1 Uelewa wa kijadi wa familia ya Kiafrika	1
1.1.2 Majukumu katika familia pana ya Kiafrika	2
1.1.3 Mabadiliko katika familia ya kisasa ya Kiafrika	3
1.1.4 Athari za mabadiliko katika familia ya Kiafrika	4
1.2 Tatizo la utafiti.....	7
1.3 Maswali ya utafiti	7
1.4 Madhumuni ya utafiti	8
1.5 Sababu za kuchagua mada hii.....	8
1.6 Upeo na mipaka	8
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii	9
1.8 Msingi wa nadharia.....	13
1.9 Njia za utafiti	15
1.9.1 Mbinu za uteuzi wa sampuli	16
1.9.2 Ukusanyaji wa data.....	16
1.9.3 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data	16
1.9.4 Mbeko za utafiti	17
SURA YA PILI.....	18
UMUHIMU NA UAMILI WA KUSOMA, KUTAFITI NA KUFUNDISHA FASIHI YA WATOTO	18
2.1 Utangulizi	18
2.2 Umuhimu na uamili wa kusoma fasihi ya watoto	18
2.3 Historia fupi na maendeleo ya hadithi za watoto wa shule za msingi	20
2.4 Sifa bainifu za fasihi ya watoto	21
2.4.1 Sifa bainifu za fasihi ya watoto kuhusu wahusika.....	22

2.4.2 Sifa bainifu za fasihi ya watoto mkabala wa matumizi ya lugha	23
2.4.3 Sifa bainifu za fasihi ya watoto na ujitokezaji wa maudhui	24
2.4.4 Sifa bainifu za fasihi ya watoto katika mkabala wa matumizi ya michoro na picha	26
2.4.5 Sifa bainifu za fasihi ya watoto kwa mkabala wa mvuto na ujitokezaji wa utamaduni	28
2.5 Dhima ya fasihi ya watoto	31
2.6 Wasifu wa muundo katika fasihi ya watoto.....	35
2.7 Hitimisho	36
SURA YA TATU	38
USAWIRI WA FAMILIA YA KISASA KATIKA <i>MWEPESSI WA KUSAHAU</i> , <i>NAMPENDA MAMA WA KAMBO NA MADALALA ABADILIKA</i>	38
3.1 Utangulizi	38
3.2 Muhtasari wa vitabu vya hadithi viliwyoteuliwa vya kipindi 2000 - 2010	38
3.2.1 Muhtasari wa <i>Mwepesi wa Kusahau</i>	38
3.2.2 Muhtasari wa <i>Nampenda Mama wa Kambo</i>	40
3.2.3 Muhtasari wa <i>Madalala Abadilika</i>	41
3.3 Aina za familia zinazosawiriwa katika <i>Mwepesi wa Kusahau</i> , <i>Nampenda Mama waKambo</i> na <i>Madalala Abadilika</i>	43
3.3.1 Aina ya familia inayosawiriwa katika <i>Mwepesi wa Kusahau</i>	43
3.3.2 Aina za familia zinazosawiriwa katika <i>Nampenda Mama wa Kambo</i>	44
3.3.3 Aina ya familia inayosawiriwa katika <i>Madalala Abadilika</i>	45
3.4 Usawiri wa familia kama taasisi katika <i>Mwepesi wa Kusahau</i> , <i>Nampenda Mama wa Kambo</i> na <i>Madalala Abadilika</i>	45
3.4.1 Usawiri wa familia kama taasisi katika <i>Mwepesi wa Kusahau</i>	45
3.4.2 Usawiri wa familia kama taasisi katika <i>Nampenda Mama wa Kambo</i>	47
3.4.3 Usawiri wa familia kama taasisi katika <i>Madalala Abadilika</i>	48
3.5 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika <i>Mwepesi wa Kusahau</i> , <i>Nampenda Mama wa Kambo</i> na <i>Madalala Abadilika</i>	49
3.5.1 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika <i>Mwepesi wa Kusahau</i>	49
3.5.2 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika <i>Nampenda Mama wa Kambo</i>	50
3.5.3 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika <i>Madalala Abadilika</i>	51
3.6 Hitimisho	51
SURA YA NNE.....	53

USAWIRI WA FAMILIA YA KISASA KATIKA <i>CHEUPE NA CHEUSI, LIKIZO YA MKOSI NA AHAA! RODA</i>	53
4.1 Utangulizi	53
4.2 Muhtasari wa vitabu vya hadithi vilivyoteuliwa vya kipindi 2011 - 2018	53
4.2.1 Muhtasari wa <i>Cheupe na Cheusi</i>	53
4.2.2 Muhtasari wa <i>Likizo ya Mkosi</i>	56
4.2.3 Muhtasari wa <i>Ahaa! Roda</i>	58
4.3 Aina za familia zinazosawiriwa katika <i>Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda</i>	60
4.3.1 Aina za familia zinazosawiriwa katika <i>Cheupe na Cheusi</i>	60
4.3.2 Aina za familia zinazosawiriwa katika <i>Likizo ya Mkosi</i>	61
4.3.3 Aina za familia zinazosawiriwa katika <i>Ahaa! Roda</i>	62
4.4 Usawiri wa familia kama taasisi katika <i>Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda</i>	62
4.4.1 Usawiri wa familia kama taasisi katika <i>Cheupe na Cheusi</i>	62
4.4.2 Usawiri wa familia kama taasisi katika <i>Likizo ya Mkosi</i>	63
4.4.3 Usawiri wa familia kama taasisi katika <i>Ahaa! Roda</i>	64
4.5 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika <i>Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda</i>	65
4.5.1 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika <i>Cheupe na Cheusi</i>	66
4.5.2 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika <i>Likizo ya Mkosi</i>	66
4.5.3 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika <i>Ahaa! Roda</i>	66
4.6 Hitimisho	67
SURA YA TANO	69
MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	69
5.1 Utangulizi	69
Muhtasari	69
5.3 Matokeo ya utafiti.....	69
5.3.1 Matokeo kuhusu aina za familia zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto	70
5.3.2 Matokeo kuhusu usawiri wa familia kama taasisi katika fasihi ya watoto	71
5.3.3 Matokeo kuhusu uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika hadithi za watoto	72
Hitimisho	73
5.5 Mapendekozo ya utafiti.....	74
MAREJELEO	75

MAELEZO YA ISTILAHINI NA VIFUPISHO VYA MANENO

- Familia:** inarejelea fasili ya kisheria inayoeleza kwamba familia ni muungano wa kiasili na wa kimsingi wa jamii ambao ni kiungo msingi cha mpangilio wa kijamii na unaotambuliwa na kulindwa kisheria. Vinginevyo ni muungano wa kiasili wa uanzishaji wa kizazi.
- Familia kiini:** inarejelea familia ambayo ni familia ya wazazi na watoto pekee.
- Familia pana:** inarejelea familia iliyo na wazazi, watoto na watu wengine wa ukoo kama vile babu, nyanya, wajomba na shangazi.
- Familia ya ulezii:** inarejelea familia ambapo watoto wanaishi na wazazi walezi wala si wazazi wa kibayolojia waliowazaa.
- Fasihi ya watoto:** inarejelea fasihi maalum inayoandikwa ikilengwa kwa hadhira ya watoto, ikiangazia masuala ya watoto na wakati mwingine ikiwa na asilimia kubwa ya wahusika watoto. Katika utafiti huu inarejelea vitabu vya hadithi za watoto.
- Hadithi za watoto:** inarejelea vitabu vya hadithi vilivyochapishwa vikikusudiwa kusomwa na watoto walio katika shule za msingi hasa darasa la nne hadi darasa la nane.
- Watoto:** inarejelea fasili ya kisheria nchini Kenya ambayo inatambua watoto kama watu ambao wana umri wa chini ya miaka kumi na minane. Katika utafiti huu, istilahi hii hasa inarejelea walengwa wa fasihi ambao ni wasichana na wavulana kati ya miaka tisa hadi kumi na mitatu ambao hasa wako katika shule za msingi darasa la nne hadi la nane.

SURA YA KWANZA

1.1 Usuli wa mada

Kifungu cha 45 cha Katiba ya Kenya 2010 kinafafanua na kutoa uelekezi kwamba familia ni muungano wa kiasilia na wa kimsingi wa jamii amba ni kiungo msingi cha mpangilio wa kijamii na unaotambuliwa na kulindwa kisheria. Vilevile Kifungu hicho kinaendelea kueleza kwamba kila mtu mzima ana haki ya kuoa mtu mzima wa jinsia nyingine, kwa misingi ya maafikiano ya kuridhiana na yasiyoshurutishwa; kila mshiriki katika ndoa (mwanandoa) ana haki sawa wakati wa kuasiwi kwa ndoa, wakati wa ndoa na wakati wa kubatilishwa kwa ndoa. Kifungu hiki kinaelekeza kwamba, Bunge litatunga sheria inayotambua ndoa zilizofungwa chini ya sheria za utamaduni wowote, mfumo wowote wa sheria za kidini, sheria ya kibinagsi au sheria ya kifamilia na kwamba, sheria hiyo itatambua mfumo wowote wa sheria ya kibinagsi au sheria ya kifamilia, au unaofuatwa na watu wowote walio waumini wa dini fulani mahususi, kwa kadri kwamba ndoa zilizofungwa chini ya sheria hizo au mifumo hiyo ya kisheria zina upatanifu na shabaha na nia ya Katiba. Ufafanuzi huu wa kisheria amba umewasilishwa hapa unaashiria uwezekano wa kuwepo kwa aina anuwai za familia pamoja na mipangilio ya kusihii kifamilia. Hili tumelifanya makusudi ili kuweka msingi wa kutaka kudadisi na kuelewa ni kwa kiasi gani watunzi wa hadithi zinazomwa na watoto shulenii wanawasilisha na kuakisi uchangamano huu wa kifamilia.

1.1.1 Uelewa wa kijadi wa familia ya Kiafrika

Katika mitazamo ya kijadi, familia inafafanuliwa kuwa ni muungano wa kuasiwi na kuendeleza kizazi. Ni kundi athirifu la wanajamii wanaohusiana kwa misingi ya damu au kupitia kwa ndoa na kwa kiasi fulani kupitia kwa taratibu za upangaji watoto au taratibu za uleaji watoto. Kwa misingi hii familia kiini inaweza kufafanuliwa kuwa ni familia inayojumuisha wazazi na watoto wao, ni familia iliyohuru kufanya maamuzi fulani ya kimsingi pasi na kuhitaji ushauri au idhini ya nje. Lakini katika miktadha ya Kiafrika, kwa mujibu wa tafiti za kisosholojia za Mbiti (1969), uelewa na ufanuzi wa familia una mawanda mapana kwa misingi ya uchangamano wa watu wanaoweza kujumuishwa kama wanafamilia. Kwa misingi hii, familia inaweza kujumuisha watoto, wazazi wao, mababu na nyanya, ami/wajomba na shangazi/halati, ndugu wa kiume na ndugu wa kike pamoja na watoto wao au hata jamaa zao. Mahusiano katika familia pana ya Kiafrika yanaweza kuwa ni katika misingi ya uzao/ukoo au misingi ya kinasaba au pia kupitia

mahusiano ya kindoa kwamba mwanandoa anaweza kuhusiana na jamaa za mwanandoa mwenzake. Familia ya aina hii inaweza pia ikajumuisha watoto wa kambo au watoto wa kulea. Katika nyakati za jadi, ndoa za mitara zilikubalika (Waruta, 2005), ambapo katika familia za aina hii msambao wa kimahusiano ulikuwa mpana mno na kwa hivyo waliweza kujumuishwa watu waliokufa na hata watoto walitorajiwa kuzaliwa kwa sababu walitarajiwa kuendeleza kizazi na familia. Familia kama hizi ziliweza kuishi katika boma moja au pia ziliweza kusambaa kijiografia katika eneo kubwa zikaunda mbari, koo au hata makabila, lakini kila yalipohitajika maamuzi ya kifamilia, mikutano ya kifamilia ilifanyika kufanya maamuzi hayo.

1.1.2 Majukumu katika familia pana ya Kiafrika

Katika jamii za Kiafrika, familia pana ilikuwa sababu na msingi wa mahusiano yote ya kijamii pamoja na majukumu yote ya kifamilia yaliyoibushwa na mipangilio hiyo (Ayisi, 1992). Katika familia pana ndipo mtu alipoweza kuupata na kuutumia uhuru wake; uwepo wa mtu binafsi uliwezeshwa kuwa na maana kwa kuhusiana na watu wengine katika familia. Mtu binafsi alipata utambulisho kutoka kwa familia, alitegemea familia kwa mahitaji yake ya hali na mali; na uwepo wake kama mtu ulitegemea uwepo wa watu wengine katika familia. Kupitia taratibu na matambiko mbalimbali ya kimpito, mtu binafsi aliweza kuwa mwanachama kamili wa jamii na kuanzia hapa akaweza kujukumishwa kuhakikisha kuendelea kuwepo kwa familia na njia moja ya kuhakikisha hayo, ilikuwa ni kupitia kuendeleza kizazi, kuoa au kuolewa na kuzaa kama alivyozaliwa. Kwa hivyo, kimsingi katika jamii za Kiafrika mtu hawezi kuwepo kwa misingi ya kibinafsi; uwepo wake unategemea na unaathiriwa na uwepo wa watu wengine katika familia, katika jamii, katika mbari, katika ukoo na ndio maana kukaibuka usemi, mtu ni watu. Kwa usemi mwingine, jamii ndiyo inayozaa, inayokuza na kumfanya mtu kuwa mtu. Mtu ni mtu kwa sababu ya uwepo wa watu wengine. Uwepo wa mtu binafsi unafasirika katika misingi ya uwepo wa watu wengine kwa sababu katika misingi hiyo ndipo mtu anapojenga ufahamu tambuzi wa uwepo wake, utambuzi wa majukumu yake, utambuzi wa mafao yake na utambuzi wa wajibu wake kwake binafsi na kwa watu wengine (Mbiti, 1969). Familia pana ilimwezesha mtu kupata utambulisho wake wa kibinafsi na utambulisho wa kikundi—katika misingi ya mbari, ukoo na nasaba. Kaida za kitamaduni na kimaadili zilizotumikishwa katika jamii, zilitumikishwa pia katika familia pana na zilimwezesha mtu kukua, kuzalisha na kuheshimiwa katika jamii. Familia pana ndiyo iliyokuwa msingi wa kwanza wa utambulisho wa kidini kwa maana ya utambulisho

na urithi wa mila na desturi. Katika familia pana kupyitia kwa mababu na akina nyanya, wazazi na wanachama wengine wa familia, mtu aliwezeshwa kutambua uwepo wa Mungu, miungu, mizimu, wahenga na mababu wa zamani. Familia pana ilikuwa mbinu ya kusaidiana na kutegemeana kwa imani kwamba uwepo wa mtu binafsi ulitegemea uwepo wa watu wengine.

1.1.3 Mabadiliko katika familia ya kisasa ya Kiafrika

Pamoja na kwamba familia na jamii ya Kiafrika imedhihirisha kuwa ilikuwa na mshikamano mkubwa tena wa karibu sana, ni kweli pia kuwa imekuwa ikipitia mchakato mkubwa wa mabadiliko na mageuzi ya kimsingi yanayoathiri takriban kila nyanja ya maisha ya kijadi na sana sana uelewa na ufanuzi wa familia (Kisembo, 1998, O'Donovan, 2000). Mengi ya mabadiliko haya yaliyoasisiwa na sababu za kibinadamu na kimaumbile, yameathiri moja kwa moja misingi na uelewa wa familia ya Kiafrika—kwanza athari za ukoloni zilihujumu asasi ya ndoa kwa njia nyingi kama vile kuondolewa kwa wanaume kwenda vitani au kufanya kazi za ujira katika mashamba na miradi mingine ya wakoloni na kuanzishwa kwa taratibu za kutokuwepo kwa kina baba nyumbani na katika kipindi kirefu cha makuzi ya watoto. Athari nyingine zililetwa na kuongezeka kwa umasikini kwa sababu ya mabadiliko ya taratibu za uzalishaji mali, kupanda kwa gharama ya maisha na kwa hivyo kubana ukubwa wa familia ya Kiafrika ya kijadi.

Vinginevyo, Ukristo ulizua changamoto nyingi dhidi ya tamaduni za Kiafrika kama vile kuziangalia na kuzipiga vita ndoa za mitara kwa sababu ya kuzihujumu kwa misingi kwamba ziliwa ni uzinzi, zinaa na dhambi. Badala ya ndoa za mitara zilizokubalika pakubwa, Ukrusto ulihimiza ndoa za mume mmoja kwa mke mmoja. Athari nyingine zilizoathiri familia ya Kiafrika ya kijadi ni pamoja na kuingizwa, kuchukuliwa na kukubalika kwa tamaduni za kimagharibi kama vile kuhimizwa kujali na kushereheke masilahi, ufanisi na maendeleo ya mtu binafsi, kuibuka kwa ushindani wa mali na fedha, kuasisiwa kwa elimu ya kisasa ya kimagharibi iliyohimiza maadili ya mtu binafsi na kudhalilisha maadili ya kijumuiya/kijamii, kuingia kwa usasa hasa uliohusishwa na utamaduni wa kufanya kazi za mishahara na kipato ikiwa na maana kwamba watu walitengea kazi muda mwangi kuliko muda uliotengewa familia, kuenziwa kwa michakato ya utandawazi, kukua kwa tamaduni za kimji, misukosuko ya kimji kama vile uhaba wa kazi, uhalifu, umasikini, ukahaba na uibukaji wa mitaa ya mabanda; yote haya yaliathiri sio

tu misingi ya familia ya Kiafrika bali pia uelewa wake, msambao wake pamoja na misingi yake ya kimahusiano (Kisembo, 1998, Magoti, 2004, Waruta, 2005, Warah, 2008).

1.1.4 Athari za mabadiliko katika familia ya Kiafrika

Mabadiliko haya yaliathiri familia pana ya Kiafrika kwa njia hasi na kuyumbisha misingi ya familia hiyo hivi kwamba, japo kuna chembechembe za familia pana katika sehemu za mashambani, uhalisi huo umetoweka sana sehemu za mijini ambapo kumeanza kuibuka kwa familia mbadala za aina nyingi. Uanzishwaji na uibukaji wa miji, uibukaji wa mitaa ya mabanda mijini ambapo kuna umasikini wa kutisha kutokana na watu kuwa na kipato kidogo au kutokuwa na kipato kabisa; hii ina maana kwamba watu wamenyofolewa kutoka mizizi ya asili zao na kuwepo kwa watoto wa kurandaranda mitaani na mijini ni ithibati ya kunyofolewa huku. Vilevile kwa sababu ya umasikini, uhalifu, viwango vya chini vya elimu na mapambano ya kila uchao ili kuishi yameathiri familia ya Kiafrika kwa njia hasi na kwa njia za moja kwa moja. Kwa upande mwingine kumekuwepo na kuibuka kwa familia zenye uwezo wa kifedha, kielimu na hata mali, hali inayosababisha utengano mkubwa wa kifamilia. Hali hizi zimeathiri taratibu za ndoa na mipangilio ya kifamilia, kwa mfano gharama za afya, gharama za elimu na gharama za kuishi zimeathiri idadi ya watoto wanaoweza kuzaliwa katika familia. Kwa sababu hii, kuna ithibati kwamba familia kiini imetokea kuwa mfumo wa kifamilia unaopendelewa. Taratibu za familia pana zimepotea au zimebanwa sana; miundo ya kudhibiti familia pana imetoweka katika sehemu nyingi ambapo uhalisia huu umechangia kuibuka kwa taasisi za ulezi wa watoto wasiokuwa na wazazi au wa wazazi wasiokuwa na uwezo. Ukweli uliopo kwa sasa ni kwamba dhana ya familia ina uelewa changamano hivi kwamba katika makutaniko ya wanafunzi katika miktadha ya shule yanaleta pamoja watoto wanaotoka katika familia za aina mbalimbali kama vile-familia za baba mmoja na mama mmoja, familia za baba bila mama, familia za mama bila baba, familia za mitara, familia za ulezi, na pia wako watoto kutoka taasisi/vituo vya ulezi. Suala ibuka katika muhtasari huu linapania kuuliza, je uhalisi huu wa kifamilia unaakisika kwa kiasi gani katika fasihi/hadithi za watoto zinazosomwa shulen?

Kadri mabadiliko na mageuzi yalivyokuwa yakitonea katika familia ya Kiafrika, kulikuwa kunatokea mabadiliko mengine sambamba na haya, yaani mabadiliko katika sera za elimu yaliyoathiri kwa njia chanya utunzi na usomaji wa fasihi ya watoto. Nchini Kenya, maendeleo ya

elimu yamechangia kukua kwa fasihi ya watoto kwa njia kubwa hasa baada ya uhuru. Kumekuwa na sera mbalimbali ambazo zimeasisiwa na serikali kuhusu mfumo wa elimu. Baadhi ya sera hizo zimekuwa na athari kubwa katika kuhamasisha, kupanua na kuimarissha maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya. Kwa mujibu wa kauli alizotoa Ngugi (2009) kutokana na utafiti wake, sera ya mfumo wa elimu wa 8 - 4 - 4 na sera ya elimu bila malipo zilichangia pakubwa maendeleo ya fasihi ya watoto kwa kuhimiza usomaji na matumizi ya Kiswahili shulenii hasa kule kufanya lugha ya Kiswahili somo la lazima, licha ya kwamba matumizi ya Kiswahili yalichangia kuibuka na kupanuka kwa soko la vitabu vikiwemo vitabu vya hadithi za watoto, mbali na sera hizi kuchangia maendeleo ya Kiswahili kwa jumla. Kutokana na mapendekezo ya Tume ya Mackay (1981), Kenya ilianzisha mfumo wa elimu wa 8 - 4 - 4 ambapo Kiswahili kilianza kuwa somo la lazima na linalotahiniwa katika viwango vya shule zote za msingi na shule za upili nchini. Kiswahili kilitahiniwa kwa mara ya kwanza katika mtihani wa kitaifa wa shule za msingi mwaka 1985. Ngugi (2009) akimnukuu MBAABU (1996:131) anakiri kuwa baada ya somo la Kiswahili kuwa somo la lazima na linalotahiniwa katika shule za msingi, vitabu vya Kiswahili vikiwemo vile vya hadithi za watoto vilianza kupata soko na mahitaji yake yalipoongezeka, vikaanza kuchapishwa kwa wingi.

Kuanzia mwaka wa 2003, serikali ilitoa sera ya elimu bila malipo katika shule za msingi. Chini ya sera hii, serikali ilianza kuzipatia shule pesa za kununulia vitabu vikiwemo vitabu vya hadithi za watoto. Miricho (2015) anatoa maoni kuwa kuanzishwa kwa elimu bila malipo katika shule za msingi kumefanya wanafunzi wengi wapate nafasi ya kusoma vitabu vya hadithi za watoto kwa vile shule huvinunua kwa wingi kuliko hapo awali kutokana na pesa zinazotengewa vitabu. Kwa hakika, idadi ya waandishi wanaoandika vitabu vya hadithi za watoto vya Kiswahili na ambavyo vinalenga watoto wa shule za msingi imeongezeka katika kipindi cha kuanzia mwaka wa 2003. Wachapishaji mbalimbali wamezindua miradi ya kuchapisha vitabu vya fasihi ya watoto ili kutosheleza mahitaji ya shule yaliyoongezeka hasa baada ya elimu bila malipo. Miongoni mwa wachapishaji hao ni kama Jomo Kenyatta Foundation ambao walianzisha mfululizo wa hadithi za *Adili*, Kenya Literature Bureau ambao walianzisha mfululizo wa hadithi za *Nasaha Zetu* na Phoenix ambao walianza mfululizo wa hadithi za kikwetu. Mbali na mashirika haya kuna mashirika mengine kama vile Sasa Sema (Longhorn), Moran (EAEP), Vide-Muwa na Queenex ambayo pia yana matoleo yao ya hadithi za watoto. Mashirika haya ya uchapishaji yamechangia

pakubwa katika ukuaji na uenezaji wa fasihi ya watoto kwa kuchapisha kazi za waandishi mbalimbali.

Kuimarika na kupanuka kwa utunzi wa hadithi za watoto kwa upande wake kumeibua haja ya kutokea kwa tafiti za aina mbalimbali zinazoangazia hadithi hizi. Hapana maafikiano ya wazi ni masuala ya aina gani yanayostahili kupewa kipaumbele katika tafiti hizi ndio maana Wamitila (2008) anahoji kwamba utafiti unaoangazia fasihi ya watoto umepuuzwa kwa miaka mingi katika maandishi ya kihakiki ambapo kazi nyingi za kihakiki hushughulikia fasihi ya watu wazima labda kutokana na imani ya kuwa fasihi ya watoto haistahiki kuchunguzwa kinadharia au ni masimulizi yenye lengo la kuburudisha watoto tu. Musau na Ngugi (1997) kwa upande wao wanadai kuwa utafiti katika fasihi ya watoto ya Kiswahili hauna historia ndefu ikizingatiwa kwamba hadithi za watoto zinakisiwa kuimarika kutokea miaka 1980. Katika utafiti mwingine uliofanywa na Ngugi (2009), mtafiti huyu anaibua madai kuwa mojawapo wa tafiti za awali za fasihi ya watoto ya Kiswahili nchini Kenya ni utafiti uliofanywa na Mpesha (1996). Hata hivyo, katika miaka ya kuanzia 2000, tafiti katika fasihi ya watoto zimeshika kasi kwa kuvutia watafiti wengi kwa sababu hadithi hizi na fasihi ya watoto kwa jumla inatokea kuibua masuala mengi ya kiusomi. Baadhi ya tafiti hizo ni kama vile zile za Karuga (2005), Muthubi (2005), Kairu (2005), Matundura (2007), Ngugi (2009) na Miricho (2015). Katika utafiti wake, Miricho (2015) alipendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu masuala yanayoibuka katika jamii.

Usawiri wa familia katika hadithi za watoto na katika fasihi ya watoto kwa jumla ni mojawapo wa masuala ambayo hayaonekani kama yamefanyiwa utafiti, yaani hadithi za watoto na fasihi ya watoto kwa jumla katika fasihi ya Kiswahili inamwelewesha nini mtoto kuhusu dhana ya uhalisia wa kifamilia? Je, ni mifumo gani ya kifamilia inasawiriwa katika hadithi za watoto? Mbali na haya, kunaweza kutolewa kauli kwamba katika siku za hivi karibu kupitia ripoti za vyombo vya habari kama vile redio, runinga na magazeti kumekuwa na mizozo ya mara kwa mara katika mahusiano ya kifamilia; mizozo hii inasawiriwa na kuhusishwa na familia za aina gani? Utafiti huu unakusudia kutilii na kudadisi ili kuelewa ni mifumo gani ya kifamilia imezoeleka kusawiriwa katika hadithi za watoto, kujaribu kuonyesha kama kuna upendeleo wa aina za familia zinazosawiriwa, na hatimaye kujaribu kutoa makisio ni kwa nini aina fulani za familia hazijitokezi katika usawiri utakaojitokeza katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Kulingana na kusoma kwangu, hakuna ithibati kwamba kumewahi kufanywa utafiti wowote kuhusu hadithi au fasihi ya watoto unaoangazia usawiri wa familia kama msingi wa mahusiano na makuzi ya mshikamano wa kifamilia. Utafiti huu unakusudia kuziba pengo hili la kiutafiti.

1.2 Tatizo la utafiti

Katika utafiti huu tunalenga kuangazia na kulichanganua suala la usawiri wa familia katika hadithi za watoto na fasihi ya watoto kwa jumla katika fasihi ya Kiswahili. Kimsingi tumehoji kwamba dhana ya familia ni dhana changamano kidhahania na kihalisi hivi kwamba kuna haja ya kutaka kujua ni kwa kiasi gani uchangamano wa kifamilia unaakisika katika hadithi za watoto. Kwa kuwa usawiri wa familia ni kiungo muhimu katika uwasilishaji wa maudhui ya kimaadili kwa watoto, kuna haja ya kuwepo na uhalisia wa kiusawiri ili uchangamano wa kifamilia uweze sio tu kuakisika bali pia kubainika katika hadithi za watoto. Kila panapotokea kauli na miito ya kuimarisha mshikamano wa kifamilia mara nyingi hii inakuwa miito ya kijumla kwa kuwa huwa haijulikani ni familia za aina gani zinazokusudiwa—je ni familia zilizo na wazazi wa pande zote au familia za mzazi mmoja? Je familia za mitara, familia za waelezi kama vile babu na nyanya kuwa walezi kutokana na changamoto zilizoletwa na janga la ukimwi na taasisi kama familia zinaakisika vipi katika hadithi zinazosomwa na watoto katika fasihi ya watoto shulen? Kwa hivyo kuna haja ya kuchunguza kama hadithi wanazosoma watoto ni hadithi ambazo zinasawiri familia kwa upana wa uchangamano wa kifamilia unaoweza kubainishwa nchini Kenya au kama ni familia ambazo baadhi ya watoto hawawezi kujitambulisha nazo ikizingatiwa kwamba watoto katika viwango na vitengo mbalimbali vya elimu wanaangaliwa kwa misingi ya kimajumuia na ilhali ukweli wa mambo ni kwamba kuna watoto wengi wanaotoka katika familia zilizo na upekee wa aina maalum.

1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

- (i) Je, ni familia za aina gani zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto?
- (ii) Je, familia kama taasisi inaakisika vipi katika fasihi ya watoto?
- (iii) Je, uhalisi wa kifamilia unaakisika kwa kiasi gani katika hadithi za watoto?

1.4 Madhumuni ya utafiti

- (i) Kubainisha aina za familia zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto.
- (ii) Kutathmini usawiri wa familia kama taasisi katika fasihi ya watoto.
- (iii) Kuchunguza uhalisi wa kifamilia unavyoakisisika katika hadithi za watoto.

1.5 Sababu za kuchagua mada hii

Sababu kuu ya kuchagua mada hii inatokana na ukweli kwamba tafiti nyingi za awali juu ya fasihi ya watoto katika fasihi ya Kiswahili zimeangazia masuala ya wasifu wa fasihi ya watoto, maudhui katika fasihi ya watoto, usimulizi katika hadithi za watoto, miundo ya kiutunzi katika fasihi ya watoto, uibushaji wa maadili katika fasihi ya watoto na mambo sawia na hayo. Hata hivyo, kulingana na kusoma kwangu hapana ithibati ya utafiti wowote uliofanywa unaoangazia suala la usawiri wa familia. Watoto ni kundi jamii lililo na umuhimu mkubwa na linaloambatanishwa kwa karibu sana na familia kwa maana kwamba makuzi ya watoto , ufunzaji wa maadili na mbeko ni mambo yawezekanayo katika misingi ya familia. Ufanisi wa watoto katika maisha yao ya baadaye unategemea kwa kiasi kikubwa walikuzwa na kulelewa katika familia za aina gani. Hii ina maana kwamba kuna haja kuelewa na kuitambua mifumo ya kifamilia na jinsi inavyoathiri makuzi ya watoto. Hili ni suala ibuka katika tafiti za kifasihi na inahalisi kulishughulikia katika fasihi ya watoto. Kwa hivyo, katika kubainisha familia katika hadithi za watoto, kuna uwezekano wa kuweza kuonyesha msambao wa mifumo ya kifamilia inayojitokeza katika fasihi za watoto, kuonyesha uhalisi wa kiusawiri kama njia ya kuwakinga watoto dhidi ya kulazimishiwa ufanuzi wa kijumla wa mifumo fulani ya familia na ilhali uhalisi wao wa maisha unatambua uwepo wa uchangamano wa kifamilia. Utafiti huu pia unanuia kuchangia kiusomi katika kubainisha dhima ya fasihi ya watoto katika usawiri wa kifamilia na kutoa mielekeo inayofaa ya maadili ya kifamilia ili isionekane kama fasihi ya kuburudisha tu.

1.6 Upeo na mipaka

Fasihi ya watoto inajibainisha kwa njia mbili kuu; fasihi ya watoto andishi na simulizi lakini utafiti huu ulijikita katika fasihi andishi ya watoto. Utafiti huu ulichunguza usawiri wa familia katika fasihi ya watoto kwa kurejelea hadithi za watoto sita zilizoteuliwa ambazo ni *Mwepesi wa Kusahau, Nampenda Mama wa Kambo, Madalala Abadilika, Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi*

na *Ahaa! Roda*. Utafiti huu basi ulijihuisha kuchunguza, kuangazia, kubainisha na kuakisika kwa mifumo changamano ya kifamilia kadri ilivyo katika jamii halisi kwa sifa, wasifu na aina za familia zilizosawiriwa katika hadithi za watoto. Usawiri huo wa kifamilia ultathminiwa kwa kuangalia ni kwa jinsi gani ungamano la mifumo ya kifamilia linaakisika katika hadithi hizi. Uchangamano huo una mawanda makubwa au finyu kwa kiasi gani na hatimaye jinsi uchangamano huo huo wa mifumo ya kifamilia unavyoathiri uwasilishaji wa maudhui na falsafa za kimaisha. Utafiti huu ulijishughulisha na hadithi za watoto zinazohusu familia na zilizo na wahusika wakuu ambao ni watoto. Ulichunguza sifa zinazojitokeza za kifamilia kwa jumla.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii

Sehemu hii iliangazia baadhi ya hoja na kauli zilizotokana na tafiti zilizofanywa kuhusu fasihi ya watoto katika fasihi ya Kiswahili ili kuonyesha zitakavyoufaa utafiti huu na zilivyo tofauti nao. Hapana shaka kwamba suala la fasihi ya watoto limewahi kuhakikiwa na kutafitiwa katika tungo za aina nyingi zinazohusu fasihi ya watoto katika fasihi ya Kiswahili. Ni kweli kwamba suala hili limewahi kujitokeza katika tafiti za aina mbalimbali, na limewahi kujadiliwa kiusomi kwa njia nyingi na kuegemezwa kwenye mikabala aina aina katika fasihi ya Kiswahili. Tafiti kuhusiana na fasihi ya watoto zimewahi kuangazia nafasi ya fasihi ya watoto katika jamii; baadhi zimeangazia usawiri wa wahusika watoto katika fasihi ya Kiswahili au pia wahusika wanyama wanaojitokeza katika hadithi hizo. Nyingine zimejishughulisha na masuala ya maudhui, maadili na mahusiko ya fasihi ya watoto katika makuzi ya watoto. Kwa jumla kipengele hiki cha fasihi ya watoto kina tafiti za kijumla na baadhi ya tafiti zikiangazia kazi mahususi au mkusanyiko wa hadithi mahususi za watoto. Kimsingi tafiti hizi zilizoko katika fasihi ya Kiswahili, zinatofautiana kwa misingi ya malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa. Tafiti hizi zimewahi kufanywa katika fasihi ya watoto iliyowasilishwa katika utanzu wa hadithi za watoto, baadhi katika riwaya, tamthilia, ushairi wa watoto na hata katika nyimbo za michezo ya watoto. Kutoptana na tafiti hizi kauli nyingi zimetolewa kuhusu fasihi ya watoto, baadhi zikiwa kauli za kijumla na baadhi zikiwa kauli kuhusiana na kazi mahususi.

Ufahamu huu ulituchochea kuhoji kwamba mapitio ya maandishi na machapisho yaliyodhamiriwa katika utafiti huu yalilenga kubainisha masuala ibuka katika fasihi ya watoto ambayo yametafiti na kuliangazia suala la uhusika wa watoto katika fasihi ya Kiswahili kwa

jumla na hasa ujitokezaji wa maadili na falsafa za makuzi na ushikamano wa kialila. Hii ni kwa kuwa kazi za aina hiyo zilizopo kwa kiasi zitakuwa zinaoana na mada ya utafiti huu na kwa hivyo zilichangia kukuza hoja na kauli zilizotuelekeza katika mahitimisho ya jumla juu ya usawiri wa familia katika fasihi ya watoto na zaidi kuonyesha uhalisia wa kiusawiri wa familia kadri zinavyosawiriwa katika hadithi za watoto. Kwa hivyo, mapitio ya maandishi na machapisho yanayojumuishwa hapa ni mapitio yaliyo na mlandano wa masuala ya uchangamano wa familia na mawasilisho yake katika hadithi za watoto na fasihi ya watoto kwa jumla, uhusika wa familia katika tungo za watoto, mifumo ya kifamilia inayosawiriwa na kupewa kipaumbele katika fasihi ya watoto, miundo ya familia na makuzi ya watoto kimaadili katika hadithi za watoto. Mapitio haya yalijifunga katika dhana ya familia kijumla kama tulivyoieleza na zaidi kuangazia upekee wa kifamilia pale unapojitokeza na dhima ya familia na uhusika wake katika makuzi ya watoto katika familia. Maandishi yanayoangazia athari za kiuamili za usawiri wa familia katika fasihi ya watoto yaliweza kujumuishwa pia; maandishi yanayoangazia udhihirikaji, ugeukaji au udumishwaji wa mitazamo mahususi ya kifamilia katika tungo za watoto yalihuishwa pia. Mapitio haya yalilenga vilevile kuonyesha ufaafu na umuhimu wa kuzingatia maendeleo ya kiutunzi na kiusomi yaliyofikiwa katika kulijadili suala la usawiri na ujitokezaji wa familia katika fasihi ya watoto katika fasihi ya Kiswahili.

Baadhi ya masuala ambayo yamewashughulisha watafiti wa fasihi ya watoto ni pamoja na suala la familia na mifumo ya kifamilia kwa kadri linavyojitokeza katika tungo za watoto. Kimsingi tafiti zilizochukua mwelekeo huu ziliazimia kuonyesha umuhimu wa familia katika kukuza maudhui yanayowiana na kuakisi uhalisi wa maisha ya watoto. Hata hivyo, ni sharti ielewewe kwamba dhana ya familia ni dhana pana na changamano na kwa hivyo baadhi ya tafiti zilizoko zilihiari kuangazia baadhi ya vipengele vya familia. Utafiti wa Mpresa (1996) ulihusu fasihi ya watoto nchini Tanzania. Mpresa alichunguza ukuaji na maendeleo ya fasihi ya watoto nchini Tanzania kwa kurejelea vitabu vya hadithi za watoto vilivyoandikwa kwa Kiswahili kutoka nchini Tanzania. Katika utafiti wake, Mpresa alitambua dhima ya fasihi ya watoto katika jamii. Utafiti wa Mpresa uliufaa huu kwa vile ulithibitisha kuwa vitabu vya hadithi za watoto husawiri hali halisi ya jamii na vile vile kuwa hadithi zile si ngano tu bali ni usawiri wa jamii ambamo familia huwa. Hata hivyo utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa wake ulihusu ukuaji na maendeleo ya fasihi ya watoto ilhali huu unahuusu usawiri wa familia katika fasihi ya watoto.

Utafiti wa Muthubi (2005) ulitazama mikakati na mbinu za tafsiri katika fasihi ya watoto. Alichunguza vitabu ambavyo vimetafsiriwa na kurahisishwa ili vitumiwe na watoto kama vile *Mkasa wa shujaa Liyongo*. Ingawa utafiti wake ni tofauti kimalengo na huu, utafiti huu uliufaa huu katika kuamua ni sifa gani za kuzingatia katika uteuzi wa vitabu vyta fasihi ya watoto. Karuga (2005) alihakiki vitabu teule vyta hadithi vinavyosomwa katika shule za msingi nchini Kenya kwa kuchunguza fani na maudhui. Utafiti wake uliupatia huu msukumo wa kuchunguza usawiri wa familia kwa maana alidai kuwa vitabu vyta fasihi hii vinasomwa sana shuleni na hivyo vina uwezo wa kuathiri mtazamo wa watoto wanaosoma. Utafiti wa Karuga ni tofauti na huu kwa vile yeye alichunguza fani na maudhui ilhali huu unachunguza usawiri wa familia nzima.

Utafiti wa Kairu (2005) ulihusu uhalisia na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto. Madhumuni yake yalikuwa kuchunguza uzingatiaji wa sifa zinazofaa katika utunzi wa fasihi ya watoto katika hadithi za watoto za Ken Walibora, kuchunguza jinsi uhalisia unavyobainika katika vitabu vyta mwandishi huyu kupitia kwa vipengele vyta wahusika, mandhari yakiwemo yale ya kifamilia, na maudhui pamoja na kubainisha mtindo alioutumia mwandishi katika kuwasilisha ujumbe wake na uwiano wake katika fasihi ya watoto. Mtafiti huyu alidai kuwa kazi za watoto za Ken Walibora zinaakisi uhalisia wa maisha ya watoto katika mazingira yao yakiwemo yale ya kifamilia. Kairu alichunguza mtindo na uhalisia ilhali utafiti huu unachunguza fasihi ya watoto katika misingi ya usawiri wa kifamilia. Hata hivyo utafiti wake ulisaidia huu katika kudondoa sifa za fasihi ya watoto na usawiri wa kifamilia.

Utafiti wa Matundura (2007) ulihusu taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Utafiti huu ulichunguza ni kwa kiwango na kwa namna gani waandishi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto wanaendeleza taswira dumifu za uana zinazoendeleza ubaguzi wa kijinsia na iwapo uendelezaji huu ni jambo linalofanywa kimakusudi au kisadfa. Utafiti huu ulionyesha watoto katika familia wamebaguliwa kwa misingi ya jinsia zao. Lengo kuu la utafiti wake lilikuwa kuthibitisha kwamba kutosawiriwa kwa watoto kwa njia ya usawa katika fasihi ya watoto kunaweza kuchangia katika kuendeleza taswira dumifu za uana katika familia na jamii pana. Kutokana na utafiti huu iligunduliwa kuwa waandishi wa fasihi ya watoto wanaendeleza

taswira dumifu za uana. Matundura (2007) aligundua kuwa katika vitabu alivyovichunguza, mhusika wa kike amesawiriwa kama dhaifu, mtegemezi wa mwenzake wa kiume na aliyebaguliwa katika familia; mhusika wa kiume amesawiriwa kama jasiri na aliye na nguvu na uwezo. Utafiti huu utaufaa huu katika kuchunguza usawiri wa familia ya kisasa katika fasihi ya watoto, kwa kuhoji kwamba athari hasi za kijinsia zinazomkumba mtoto wa kike zina mahusiano ya moja kwa moja na miundo na mifumo ya kifamilia.

Utafiti wa Ngugi, P. M. (2009) ulihusu hali ya fasihi ya watoto katika Kiswahili nchini Kenya. Utafiti huu ulihusu tabia za usomaji za watoto shulenii na hata nyumbani. Baadhi ya masuala muhimu ambayo utafiti wake uliangazia ni mitazamo ya watoto kuhusu kusoma, idadi ya vitabu vya kusoma walivyokuwa navyo, mazoea ya usomaji kwa ajili ya kujiburudisha na wajibu wa washika dau kama walimu wa Kiswahili na familia katika kukuza mazoea ya usomaji mionganii mwa watoto. Utafiti huu utasaidia katika kubainisha aina za familia ikitazamwa aina za familia zinazorejelewa katika usomaji wa fasihi ya watoto. Ngugi, P. M. (2012) alizungumza kuhusu tafsiri katika fasihi ya watoto na alitoa sifa baadhi ya sifa za fasihi ya watoto. Maeleo yake yalisaidia katika uteuzi wa vitabu vya utafiti huu ili kujua sifa za kuzingatia wakati wa uteuzi. Nao, utafiti wa Ngugi, P. M. na Bakize L. H. (2014) ulihusu fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya mtoto kisaikolojia. Utafiti wake uliusaidia utafiti huu katika kuelewa jinsi usawiri wa familia katika fasihi ya watoto unavyoweza kumwathiri mtoto kisaikolojia.

Utafiti wa Miricho (2015) kuhusu usawiri wa watoto katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi* na ule wa Miricho, M. na E.M. Mbuthia (2017) kuhusu athari ya usawiri wa watoto katika hadithi teule ulikuwa na madhumuni ya kubainisha taswira za mtoto wa kike na zile za mtoto wa kiume, kulinganisha sifa za watoto wa kike na wenzao wa kiume na kuchunguza mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume katika *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*. Usawiri huu ulijumuisha usawiri wa mtoto katika mazingira ya kifamilia. Matokeo ya utafiti huu yalithibitisha kuwa katika jamii ya mwandishi, mtoto wa kike alisawiriwa kwa njia chanya zaidi kuliko mtoto wa kiume. Msichana alichorwa kama aliye mwema kuliko mvulana. Ilithibitishwa pia kuwa katika karne ya ishirini na moja hakuna majukumu wanayotengewa wasichana ama wavulana pekee katika familia bali wavulana na wasichana wanashirikiana kufanya kazi zote. Mapendekezo yalitolewa kuwa kuna haja ya kuchukua hatua

za dharura kushughulikia maslahi ya mtoto wa kiume katika jamii. Jambo hili lingemwokoa kutokana na hatari ya kubaki nyuma kwa mtoto wa kiume katika elimu na shughuli nyingine za kijamii. Utafiti huu kwa kiasi fulani ni maendelezo ya utafiti wa Miricho kwa kuwa yeze alijihuisha na usawiri wa watoto ilhali huu unapiga hatua kuchunguza usawiri wa familia za kisasa nchini Kenya na jinsi mifumo ya kifamilia inavyomhusu mtoto. Utafiti huu uliuwekea huu misingi kwa vile mwishowe ulitoa mapendekezo ya kwamba utafiti zaidi ufanywe kuhusu vipengele vingine vya fasihi ya watoto ya Kiswahili kama vile masuala ibuka katika fasihi ya watoto ambayo ni msingi wa utafiti huu. Utafiti huu hata hivyo, haukujihusisha na aina za familia na wasifu wa familia hizo na hivyo utafiti huu unanuia kujaza pengo hilo la kiutafiti.

Utafiti wa Miricho, M. Sheila P. Wandera-Simwa na Nabea Wendo (2019) ambao ulihusu fasihi ya watoto ya Kiswahili na mshikamano wa kitaifa ulisaidia utafiti huu katika kushughulikia masuala ibuka kama vile suala la usawiri wa familia.

1.8 Msingi wa nadharia

Sehemu hii inachunguza maelezo ya nadharia ambayo iliongoza utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia ya uhalisia ni za aina nyingi, kwa mfano kuna nadharia ya uhalisia wa kijamaa, nadharia ya uhalisia ya kijamii, nadharia ya uhalisia nafsi na nadharia ya uhalisiajabu. Utafiti huu uliongozwa haswa na nadharia ya uhalisia wa kijamii. Kwa mujibu wa Swingerwood (1975), mwasisi wa nadharia ya uhalisia ni Taine. Kulingana na Swingerwood (1975), Taine alidai kuwa fasihi huakisi jamii huku akilinganisha fasihi na kioo kuonyesha kuwa fasihi huakisi maisha ya jamii kama vile kioo kinavyoakisi sura ya mtu anayejitazama. Taine mwenyewe alikuwa ameyachukuwa, kuyaunda upya na kuyakuza mawazo ya Germaine de Stael ambaye alidai kuwa kazi ya kifasihi inapaswa ionyeshe uhalisia wa kimaadili, kihistoria, hali ya utamaduni, uchumi na siasa katika jamii ambayo huchipua kazi husika ya fasihi. Kwa kuwa msingi wa jamii ni familia, ni muhimu kutafiti jinsi uhalisia wa kifamilia unavyojitokeza katika fasihi ya watoto hasa ikichukuliwa kuwa familia hubadilika kutokana na hali mbalimbali za kimaisha.

Mtaalamu mwingine aliyechangia pakubwa nadharia hii kiasi cha baadhi ya wasomi kumtaja kama mwaasisi wa nadharia hii ni Georg Lukacs (1979) katikati ya karne ya ishirini. Lukacs alikuwa ameathiriwa na mawazo ya Karl Marx kuhusu maendeleo ya kijamii na migongano ya

kitabaka. Tahakiki nyingi za Ki-marx ni za kijamii na ziliendeleza maisha ya jamii kama yalivyokuwa wakati wake. Warren na Wellek (1973) wanasema kuwa uhusiano kati ya fasihi na jamii umejikita katika kauli aliyotoa De Bonald kwamba fasihi ni kielelezo cha jamii. Kwa hivyo ni muhimu kuichukulia fasihi kama zao la jamii na ambalo huwa limeathiriwa na mazingira ya kijamii. Mtunzi vilevile huwa ni mwanajamii na huwa anashawishiwa na hali halisi ya maisha ya wakati wake na kuizingatia katika uandishi wake. Hivyo, fasihi huwa na ufungamano mkubwa na asasi za kijamii na hivyo masuala mengi ya kifasihi huwa masuala ya kijamii. Hii inamaanisha kuwa mwandishi huchota maudhui ya kazi yake kutokana na mambo yanayotokea katika jamii ambayo kiini chake ni familia.

Eagleton (1996) anatetea mtazamo wa sosholojia ya fasihi akirejelea istilahi yenewe “sosholojia ya fasihi”, ili kuonyesha uhusiano wa fasihi na jamii. Fasihi ni zao la jamii na hivyo inaathiriwa na shughuli za jamii. Hili ni jambo ambalo mhakiki yeoyote hawezu kupuuza iwapo uhakiki wake utakuwa na mashiko. Kutokana na kauli hii tunaweza kusema kuwa mvuto mmoja unaofanya watu wapende kusoma kazi iliyoandikwa ni ikiwa watu hao wanaosoma kazi husika wanajiona katika kazi ile kwa maana kuwa wanaweza kuhusisha yanayotokea katika hadithi na mambo yanayotokea katika jamii yao. Wakati mwingine msomaji atawenza hata kujicheka na kisha kujirekebisha kutokana na matukio ya hadithi. Hii ni kwa kuwa fasihi inamulika jamii kutokana na maudhui yanayoshughulikiwa. Maudhui haya hujitokeza kutokana na vitendo vya wahusika, maneno wanayosema au yanayosemwa kuwahuusu na hata wakati mwingine kutokana na majina waliyopewa. Maudhui aghalabu huibuka kutokana na matukio halisi yanayotokea katika jamii. Suala hili la kujiona katika fasihi linajibainisha sio tu katika misingi ya kimaudhui bali pia katika mambo mengine muhimu ya kifasihi kama vile usawiri wa mifumo ya kifamilia. Warren na Wellek (1973) wanafafanua kuwa maudhui mengi ambayo huibuka katika uchunguzi wa kifasihi hutokana na masuala ya kijamii. Wanasema:

“Fasihi imeibuka kutokana na uhusiano wa karibu na jamii ambayo imejengwa na asasi za kifamilia ... fasihi pia ina dhima katika jamii ambapo asasi moja yapo katika jamii ni familia.” (uk 94)

Wamitila (2002), anasema kuwa nadharia hii hutumiwa na wahakiki ili kuthibitisha jinsi kazi fulani ilivyoathiriwa na vitengo fulani vya mazingira kama vile tabaka la mwandishi, jinsia yake, matamanio yake, hisia, muktadha wa kiuchumi, aina ya familia ya mwandishi na imani za

familia hiyo. Wamitila (2008) anaeleza kuwa fasihi kama sehemu ya utamaduni wa jamii yoyote ile huhusiana, huingiliana na huathiriana na nyanja tofauti za kijamii. Anafafanua kuwa fasihi ni asasi ya kijamii kwa kuwa inatumia lugha ambayo ni zao la jamii na kwa kuwa inachota malighafi ya maudhui kutokana na jamii. Mwandishi anayetunga kazi ya fasihi anafanya hivi katika muktadha wa jamii maalum na kwamba anapaswa kuonyesha uelewa na utambuzi wa matukio ya jamii hiyo. Mtafiti huyu anasema kuwa fasihi ni kama mwigo au kiwakilishi cha maisha ya jamii. Sifa moja ya fasihi inayohusishwa na mtazamo huu wa nadharia ya mwigo ni kuwa fasihi na jamii zina uhusiano wa uhalisi ambao unafanana na ule wa kioo kumaanisha kuwa maudhui na wahusika katika kazi ya fasihi huakisi mambo yaliyoko kwenye jamii inayohusika, ikizingatiwa kwamba jamii ni jumla ya mkusanyiko wa familia. Hii ina maana kuwa wahusika wa fasihi huwa wanawakilisha watu fulani halisi katika jamii na katika familia, lakini kwa njia ya kiubunifu. Mambo wanayotenda, wanayosema au yanayosemwa kuwahuusu wahusika hao na jinsi wanavyosawiriwa huchangia katika kukuza maudhui ambayo ni kielelezo cha maisha ya jamii husika.

Katika utafiti huu, ufanuzi huu unamaanisha kuwa tunapozitathmini kazi tulizoziteua za fasihi ya watoto, tunapima ni kwa kiasi gani wasifu na sifa za familia zinazopatikana katika vitabu vinavyochunguzwa zinafungamana na uhalisi wa jamii ambao watoto wanaosoma kazi hizo wanaweza kujitambulisha nao. Nadharia ya uhalisia iliufaa utafiti huu katika kushughulikia kazi hii hasa kutokana na mihimili yake mikuu ambayo mosi ni matukio yenyе kuakisi maisha halisi ya familia katika jamii, na pili ni wahusika wanaotenda vitendo vinavyowakilisha matendo halisi ya watu katika familia na katika jamii. Mihimili yote miwili iliufaa utafiti huu katika kutathmini usawiri wa familia ya kisasa katika hadithi zitakazoteuliwa.

1.9 Njia za utafiti

Sehemu hii ilishughulikia mbinu za uteuzi wa sampuli, ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Mbinu mahususi zilitumika katika kukusanya na kuchanganua data za utafiti, kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti na msingi wa nadharia iliyoongoza utafiti.

1.9.1 Mbinu za uteuzi wa sampuli

Vitabu nya hadithi nya fasihi ya watoto viliteuliwa kwa kutumia sampuli lengwa kwa kuongozwa na maswali na madhumuni ya utafiti. Vitabu hivyo ulikuwa katika migao miwili; vitabu nya hadithi za watoto vilivyotungwa kati ya 2000 hadi 2010 ambavyo ni *Mwepesi wa Kusahau* katika mfululizo wa Hadithi za Kikwetu (Phoenix, 2005) na *Nampenda Mama wa Kambo* katika mfululizo wa Adili (JKF, 2006) na *Madalala Abadilika* katika mfululizo wa Early Learners (Queenex 2009). Vilevile kuna vitabu nya hadithi za watoto vilivyotungwa kati ya 2011 hadi 2018 ambavyo ni *Cheupe na Cheusi* katika mfululizo wa mradi wa kusoma (Oxford 2013), *Likizo ya Mkosi* katika mfululizo wa Nasaha Zetu (KLB, 2014) na *Ahaa! Roda* katika mfululizo wa *Early Learners* (Queenex 2017). Mgao huu wa kiuteuzi unalenga kutaka kuangalia ni kwa jinsi gani tungo hizi zinaakisi uhalisi wa wakati katika kusawiri familia.

1.9.2 Ukusanyaji wa data

Utafiti huu ni wa kimaelezo na ulikuwa wa maktabani. Vitabu vilivyoteuliwa vili somwa kwa makini na data inayohusu usawiri wa familia, aina za familia, mifumo ya kifamilia ya kisasa kuchukuliwa kwa kujibu maswali ya utafiti. Maswali hayo ni: Je ni familia za aina gani zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto? Je, familia kama taasisi inaakisika vipi katika fasihi ya watoto? Je, uhalisi wa kifamilia unaakisika kwa kiasi gani katika hadithi za watoto? Sifa za wahusika zilidondolewa ili kupata usawiri wao kwa kuzihusisha na usawiri wa kifamilia. Sifa hizo za kifamilia zilibainishwa na kuchanganuliwa kuititia mtazamo wa nadharia ya uhalisia.

1.9.3 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data

Baada ya kuvisoma vitabu vilivyoteuliwa, muhtasari wa kila hadithi ultolewa na data kudondolewa kwa kuzingatia madhumuni na maswali ya utafiti. Kila kifungu katika hadithi kinachohusiana na madhumuni ya utafiti kilipoonekana, kilinukuliwa na kuchanganuliwa huku maelezo yakitolewa kujibu swali mahususi la utafiti. Kwa hivyo, data ya utafiti huu ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Mbinu hii huwa mwafaka hasa katika kuchambua data za kazi za kinathari kama vile fasihi andishi kwa kuzitolea maelezo. Maelezo ya kina yalitolewa kuhusu data zilizokusanya. Uchanganuzi wa data kuhusu aina za kifamilia ulifanywa katika kila hadithi. Mwisho, maelezo kuhusu fasihi na aina za kifamilia yalitolewa na hatimaye matokeo na mapendekezo kuwasilishwa.

1.9.4 Mbeko za utafiti

Mbeko ni maadili au kaida ambazo utafiti huhitaji kuzingatia. Utafiti huu ulizingatia taratibu maalum za maadili. Kwanza mtafiti alipata idhini ya kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi. Utafiti huu ulifanywa maktabani kwa kumwomba mkutubi ruhusa na ushauri kuhusu namna ya kupata vitabu vilivyo hitajika.

SURA YA PILI

UMUHIMU NA UAMILI WA KUSOMA, KUTAFITI NA KUFUNDISHA FASIHI YA WATOTO

2.1 Utangulizi

Katika sehemu hii mmejadiliwa kwa kina mambo ya kimsingi kuhusu fasihi ya watoto, lakini kwa kuangazia na kuweka kipaumbele katika umuhimu, manufaa na uamili wa kusoma, kutafiti na kufundisha fasihi ya watoto. Miongoni mwa mambo muhimu ambayo yamejadiliwa ni umuhimu na uamili wa kusoma fasihi ya watoto, historia na maendeleo ya fasihi ya watoto, sifa bainifu za fasihi ya watoto, dhima ya fasihi ya watoto na wasifu wa muundo katika fasihi ya watoto. Mambo haya ni muhimu kwa kuwa ni ya kimsingi kuhusu utafiti huu na yanachangia uelewa wa fasihi inayoshughulikiwa. Mathalani, historia na maendeleo ya fasihi ya watoto ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa vitabu vilivyoteuliwa vilikuwa katika migao miwili ya kiwakati, sifa za fasihi ya watoto zilikuwa muhimu kwa kuwa ndizo zilizozingatiwa kuainisha vitabu vilivyoteuliwa na kuvitambua vitabu hivyo kama vitabu vya fasihi ya watoto. Aidha, sifa za fasihi ya watoto, hasa kuhusu aina na uwasilishaji wa maudhui, zilichukuliwa kuwa muhimu katika kubainisha usawiri wa familia kwenye hadithi zilizoteuliwa. Dhima ya fasihi ya watoto katika jamii ni muhimu katika utafiti huu hasa katika kuangazia umuhimu wake katika kuipa jamii mielekeo inayoakisi kihalisi usawiri wa familia katika upana na urefu wake wa kiuchangamano. Kadhalika, dhima hii ilikuwa muhimu katika kuwezesha kutathmini hadithi zilizoteuliwa kwa mtazamo wa nadharia ya uhalisia.

2.2 Umuhimu na uamili wa kusoma fasihi ya watoto

Fasihi ya watoto imepata kutolewa ufanuzi na fasili za aina mbalimbali, jambo linaloashiria kuwa hapana maafikiano ya kijumla juu ya ufanuzi wake wa kijumla. Kwa mfano, Ngugi (2012) katika utafiti wake anaeleza kuwa fasihi ya watoto ni fasihi iliyoandikwa kwa minajili ya kusomwa na watoto. Kwa upande wake Bakize (2014) anaeleza kuwa fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayowahusu watoto. Fasili ya Bakize inaboresha ile fasili ya Ngugi kwa kuwa Ngugi alirejelea fasihi iliyoandikwa ilhali Bakize amechukua mtazamo mpana kwamba fasihi ya watoto yaweza kuwa imeandikwa au inasimuliwa kwa mdomo. Tanzu za fasihi simulizi ya watoto ni kama vile nathari nyepesi, mashairi mepesi yanayoweza kuimbwa na watoto, nyimbo za watoto,

hadithi simulizi za watoto na maigizo mepesi ya watoto. Nayo fasihi andishi ya watoto inajumuisha hadithi zilizoandikwa za watoto, vitabu vyta picha vyta watoto, vitabu vyta vibonzo, mashairi mepesi yaliyoandikwa na tamthilia nyepesi zilizoandikwa. Ngugi (2012) anasema kuwa fasihi hii huwa fupi na mhusika mkuu ni mtoto japo si kila wakati.

Katika hadithi hizi za watoto huwa mna mambo mengi ya kifasihi kama vile uwepo wa mandhari, mpito wa wakati na wahusika, mionganoni mwa mengine. Kuhusiana na wahusika, Wamitila (2008) anaeleza kuwa wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Msanii huwaweka wahusika katika mazingira yanayomwezesha kuwasilisha maudhui yake kutokana na vitendo, maneno na maingiliano yao. Miricho (2015) anafafanua kuwa ingawa wahusika wa fasihi ya watoto waweza kuwa wanyama, mazimwi na watu wazima kama vile wazazi na walimu wa watoto, wengi wao huwa watoto wenyewe ili kuweza kuvutia hadhira yake. Hali hii hufanya kazi ishawishi mtoto kusoma kwa kuwa atajitambulisha na mhusika mtoto mwenzake katika msuko wa hadithi nzima hasa iwapo mhusika yule ni shujaa na mwenye maadili.

Si hoja fasihi ya watoto inafafanuliwa kwa njia gani, tajriba ya kwanza inayojitokeza kwa mtoto katika kusoma hadithi za watoto inahusiana na kukutana na wahusika wa hadithini wanaoweza kuwa watu, wanyama, picha, vibonzo au mambo ya kimaumbile kutokana na kusoma visa vyta kiajabu, hadithi za wanyama, mizimu na hadithi nyingine sawia na hizo. Hadithi hizi licha ya usahili na ubanifu wao kiubunifu na kiuwasilishaji, zina wasifu wote wa kifasihi na zinasaidia kuongoza na kwa njia zisizo dhahiri kushawishi watoto kuanza kutambua na kujifunza jinsi ya kufikiri, kufasiri mambo na matukio, na zaidi kutangamana na sio tu wahusika wa hadithini bali pia wahusika wanajamii katika ulimwengu razini. Hadithi hizi zinasaidia kuasiisi akilini mwa watoto, hatua za mwanzo za kuandika na kupanga mawazo. Pamoja na kwamba hadithi za watoto zinaweza kuonekana kuwa nyepesi, sahili na ambazo hazikukuzwa kwa kina, bado hadithi hizi huwa na vipengele na wasifu wote wa kifasihi—mandhari, ploti, mpito wa wakati na mambo mengine ya kifasihi, japo katika kiwango kidogo. Hadithi za watoto zinaweza kuwa na ubora wa kudumu kimaudhui na hata kiubunifu, na wakati mwingine ubora unaopita mipaka ya kiwakati.

2.3 Historia fupi na maendeleo ya hadithi za watoto wa shule za msingi

Ngugi (2009), anaeleza kuwa hali ya fasihi ya watoto inatofautiana katika mataifa mbalimbali. Mtafiti huyu anaeleza kuwa katika mataifa mengi ya Kimagharibi, kwa mfano, fasihi ya watoto imeimarika zaidi kuliko katika mataifa ya Kiafrika. Katika mataifa hayo asilimia kubwa ya watoto ina elimu na uwezo wa kusoma fasihi iliyoandikwa. Katika nchi za Afrika, Kenya ikiwemo, ukuaji wa fasihi ya watoto umepitia mikondo mingi. Kairu (2005) anasema kuwa katika kipindi cha kabla ya ukoloni fasihi hii ilikuwa simulizi. Fasihi hii ilitokana na tajriba za watu katika maisha na mahusiano yao pamoja na maingiliano katika jamii zao. Hadithi ziliwapa watoto picha halisi ya jamii zao na falsafa yao. Hadithi hizi ziliwafunza watoto maadili kama vile kuwatii wazazi na watu wengine katika familia. Zilihimiza watoto ku waheshimu wazazi wao. Hadithi nyingi simulizi za kipindi hicho zilisawiri familia pana zenye zaidi ya mke mmoja na ambapo wakati mwingine mume akijaribu kutathmini ni mke yupi aliyempenda zaidi. Kwa mfano, katika hadithi simulizi ya *Mke asiye Upendo afunzwa adabu* katika Ngure (2003).

Katika kipindi cha ukoloni, fasihi ya watoto ilikuwa ikiandikwa na wakoloni wazungu. Kairu (2005) akimrejelea Mpeshu (1996) anasema kuwa kipindi cha ukoloni kililetu mabadiliko ya kifasihi katika fasihi iliyosomwa na watoto. Fasihi iliyoandikwa ilihusu utamaduni wa kigeni. Fasihi hii pia ilidunisha fasihi ya Kiafrika na kuipuuza. Nia yake ilikuwa kumsawiri Mwfrika kama mtu mjinga aliyeishi kama mnyama na aliyekosa maendeleo yoyote yale. Nia yake ilikuwa kumshawishi Mwfrika kuwa utamaduni wake ulikuwa duni. Mwishoni mwa kipindi cha ukoloni, walizuka waandishi wa Kiafrika ambao waliandika hadithi za watoto zilizosomwa shuleni. Hadithi za kipindi hiki zilijaribu kuinua hadhi ya Mwfrika kupitia mtazamo wa Kiafrika. Vilevile, hadithi za kipindi hiki zinasawiri familia za aina mbalimbali. Kimsingi, maadili mionganoni mwa wanafamilia yanaonekana kuhimizwa. Kwa mfano, hadithi ya *Adili na Nduguze* (Shaaban, 1952) ambayo inahusu mtu anayeitwa Adili ambaye aliwapenda ndugu zake wawili- Hasidi na Mwivu na aliyefanya jitihada kuishi vizuri na ndugu zake ingawa walikuwa wasaliti. Ndugu wasaliti wanaonekana kuadhibiwa kutokana na njama zao za kujaribu kumuua Adili. Mwishowe ndugu wote watatu wanaungana na kuishi kwa furaha. Mfano mwingine ni hadithi ya *Alipanda Upepo na Kuvuna Tufani* (Somba, 1969). Familia inayorejelewa na Somba katika *Alipanda upепо na Kuvuna Tufani*, ni familia ya mzazi mmoja ambaye ni mama. Mama huyu ana kijana mmoja aitwaye Mulei ambaye anaonekana akifanya juhudzi za kumtafuta baba

yake lakini mama yake anakataa kumfichulia siri kuhusu baba yake. Jambo hili linaonyesha kuwepo kwa familia ambayo ina mzazi mmoja ambaye ni mama na ambapo mama hataki kumfichulia mwanaye wa kiume kuhusu baba yake wakati anapodadisi kumhusu. Mwishowe, Mulei anapuuza ushauri wa mama yake na kuharibika kitabia. Hii inaelekea kuonyesha kuwa kutokuwepo kwa baba katika malezi ya watoto huenda kukaathiri ukuaji na tabia za mtoto.

Miricho (2015) anafafanua kuwa maendeleo ya elimu yamechangia kukua kwa fasihi ya watoto kwa njia kubwa nchini Kenya hasa baada ya uhuru. Kumekuwa na sera mbalimbali zinazotolewa na serikali kuhusu elimu. Baadhi ya sera hizo zimekuwa na taathira kubwa zaidi katika maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya. Sera ya mfumo wa elimu wa 8 - 4 - 4 ambayo ilipendekeza Kiswahili kiwe somo la lazima shulenililipanua usomaji wa vitabu vya hadithi za watoto. Nayo sera ya elimu bila malipo imechangia pakubwa maendeleo ya fasihi ya watoto kwa kuwa kutokana na sera hii serikali ilitengeta shule pesa za kununua vitabu ikiwemo vitabu vya hadithi. Mwaka wa 2015 ulikuwa mwaka muhimu katika maendeleo ya watoto kujua kusoma hadithi. Kuanzia mwaka huo serikali ilianzisha mradi uliojulikana kama ‘Tusome.’ Chini ya mradi huu, uliodumu miaka minne hadi mwaka wa 2019, watoto katika madarasa ya chini katika shule za msingi walifunzwa kusoma kwa kutumia mbinu mpya. Ubora wa vitabu vya fasihi ya watoto vinavyochapishwa umeimarika miaka ya hivi karibuni. Ngugi (2009) anasema kuwa Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa Kenya imechangia ubora huu kwa kuwa inakagua ufaafu wa vitabu vinavyochapishwa ili kuidhinisha vile vinavyofaa kusomwa na watoto shulenil. Jambo hili linafanya waandishi na wachapishaji kujitahidi kutimiza viwango vya ubora vinavyowekwa na taasisi hiyo. Mbali na ongezeko katika uandishi na usambazaji wa vitabu vya fasihi ya watoto, fasihi hii imekua na kuendelea kimaudhui kuanzia kwa maudhui ya maadili na maudhui ya kibunifu yaliyojengwa katika fantasia hadi kufikia kiasi cha kuwasilisha maudhui yenye uhalisia wa kijamii kama vile usawiri halisia wa kifamilia.

2.4 Sifa bainifu za fasihi ya watoto

Hadithi za watoto zina sifa maalum zinazozitambulisha. Kimsingi, huwa sahili na zina ubanifu wa kiubunifu na kiuwasilishaji licha ya kuwa na wasifu wote wa kifasihi. Sifa za hadithi za watoto husaidia kuongoza kwa njia zisizo dhahiri kushawishi watoto kuanza kutambua na

kujifunza jinsi ya kufikiri, kufasiri mambo na matukio. Kwa mfano, mtoto anaposoma hadithi kama ile ya *Mwepesi wa Kusahau* anaweza kuvutiwa na tabia nzuri ya Maria na kama alikuwa na tabia mbaya kama ile ya mhusika Juma akaamua kuiacha na kuwa kama Maria sawa na uamuzi uliofanywa na Juma. Hivyo, Hadithi za watoto zinaweza kuwa na ubora wa kudumu kimaudhui na hata kiubunifu, na wakati mwingine ubora unaopita mipaka ya kiwakati.

2.4.1 Sifa bainifu za fasihi ya watoto kuhusu ujenzi wa wahusika

Katika sehemu iliyotangulia hapa juu tumetaja kuwepo kwa wahusika ainati katika fasihi ya watoto. Bakize (2014) anaeleza kuwa wahusika wakuu katika fasihi ya watoto aghalabu huwa ni watoto. Hali hii inachangia mtazamo chanya unaotawala kazi husika kuwa na mvuto kwa watoto. Kwa mfano, vitabu vilivyoteuliwa kwa utafiti huu kama vile *Mwepesi wa Kusahau, Nampenda Mama wa Kambo, Madalala Abadilika, Cheupe na Cheusi* vina wahusika wakuu amba ni watoto wanaotangamana na watu wengine katika familia kama wazazi na ndugu. Lakini katika hadithi nyingi zinazojumuishwa katika utafiti huu, mhusika baba haonekani kwa wingi na hii huenda ikachangia mtazamo kuwa familia nyingi zinasimamiwa na kufadhiliwa kihali na mali na mama bila baba kuonekana akitekeleza majukumu muhimu. Kwa upande mwingine, wahusika wanyama wanapotumiwa katika hadithi za watoto huvutia watoto kwa sababu mara nyingi wanyama huwakilisha sifa fulani zinazojulikana katika jamii. Wakati mwingine baadhi ya wanyama wanaweza kusawiriwa kwa njia chanya zinazowafanya kupendwa ilhali wanyama wengine wanasawiriwa kwa kubebeshwa wasifu hasi wa kuchukiwa. Kwa mfano, sungura katika jamii nyingi za Uswahilini hutambuliwa kama mnyama mjanja na mwerevu. Wahusika wanyama waliotumiwa aghalabu husawiriwa kwa njia zinazoakisi utangamano changamano wa kutenda vitendo vinavyowakilisha tabia ambazo watoto wanaweza kuzinasibisha na tabia wanazoziona miongoni mwa wanajamii katika jamii zao. Kwa jumla, wahusika katika fasihi ya watoto ni kitovu na kichocheo kwa watoto kujifunza mambo mengi.

Kwa njia mbalimbali katika usomaji ulio na wahusika kama walijotajwa hapa juu, hadithi za watoto huwafundisha na kuwashawishi watoto kugundua na kuvumbua uchangamano wa mambo katika hadithi ambazo zinaweza kuchukuliwa kuwa nyepesi na rahisi kueleweka. Kwa mfano, watoto huanza kugundua na kubainisha na kutenga tabia chanya na tabia hasi. Kwa mtazamo wa watoto, kila kitu hasa kinachojitokeza katika hadithi wanazosoma, huwa ni kitu kipyaa kinachostajabisha na kilicho na uwezo wa kusisimua, lakini zaidi kila kitu kwa mtazamo wa

watoto kina uwezo wa ajabu. Kwa mfano, hadithi ya watoto inaweza kuanza kwa kusifia ua la aina fulani, usawiri wa wasifu huu unaweza kuibua aina nyingi za maswali, kuchochea upekuzi, kuasisi utafiti hata kama ni katika kiwango cha utoto. Kwa jumla, hadithi hiyo moja ya ua inaweza kuwa mwanzo wa safari ndefu ya kiekolojia akilini mwa mtoto kutaka kuliona ua hilo katika ulimwengu razini na kisha kuvumbua uwepo wa maua mengine. Vilevile, pale hadithi inapotokea kuwa na wahusika walio marafiki si hoja kama ni wahusika wanyama au binadamu, wasifu chanya wa urafiki wa hadithini unaweza kuangaliwa kadri unavyoakisika katika urafiki wa kweli katika ulimwengu razini; au michakato ya ubainikaji wa urafiki wa hadithini inaweza ikawa ni mwanzo wa kugundua urafiki ni nini. Hadithi za watoto si hoja zinazungumza juu ya nini au zinajishughulisha na kitu gani, hadithi hizi zina uwezo wa kumwelekeza mtoto katika undani na uchangamano wa uhalisia wa ulimwengu na uhalisia wa kimahusiano katika jamii. Hadithi hizi za watoto hata katika usahili na ufupi wao wa kiuwasilishi, ni hadithi zilizo na upana mkubwa wa kiufasiri, ni hadithi ambamo mnaweza kugundulika uchangamano wa maisha unaolandana au unaoakisi uchangamano wa maisha ya mtoto anayesoma hadithi hizo. Na moja ya mambo yanayoweza kugunduliwa hivyo ni usawiri wa mifumo ya kifamilia.

2.4.2 Sifa bainifu za fasihi ya watoto mkabala wa matumizi ya lugha

Kuna maafikiano ya kijumla miongoni mwa watafiti na wasomi wa fasihi ya watoto kuwa lugha katika fasihi ya watoto huwa nyepesi kwa kuzingatia kiwango cha masomo na umri wa watoto wanaolengwa ili mtoto msomaji aweze kuifuatilia hadithi inavyosimuliwa, kuifurahia na kuupata ujumbe au maudhui yaliyoko katika hadithi husika. Mathalani, hadithi zinazolenga watoto wa madarasa ya chini katika shule za msingi zina lugha nyepesi kuliko vitabu vya hadithi zinazolenga watoto wa madarasa ya juu katika shule za msingi. Sentensi mara nyingi huwa fupi na zenye miundo sahili ili ujumbe uweze kuelewaka wazi na bila utata kwa kuwa urazini wa wasomaji chipukizi huwa mdogo. Vitabu vilivytumia sentensi sahili ambazo nyingine ni za neno moja, mawili au matatu na zilizo na msamiati mwepesi humvutia mtoto kwa kuwa huwasilisha ujumbe kwa haraka. Msamiati unaotumika wahitajika kuwa na wepesi unaolingana na kiwango cha watoto wanaolengwa. Lugha ngumu inaweza kuathiri uelewekaji wa hadithi na watoto wanaosoma huenda wasiupate ujumbe uliokusudiwa. Hata hivyo, Ngugi (2014) anaeleza kuwa katika kutunga au kuandika hadithi za watoto, ni muhimu kuzingatia kuwa kwa kutegemea umri na kiwango cha utambuzi cha watoto wanaolengwa, watoto huhitaji ujitekezaji wa

msamiati mpya ili kupanua uwezo wa kuwasiliana. Lugha huhitajika ilingane na kiwango cha mtoto kwa upande wa msamiati, aina na miundo ya sentensi na ujumbe kwa jumla.

Pamoja na kwamba kauli hizi za kiushauri ni muhimu katika kuwaelekeza watanzi wa baadaye, uhalisi wa hadithi za watoto zilizoko katika fasihi nyingi za watoto, ni kwamba hadithi za watoto zinaweza kuwa tata, sio katika misingi ya matumizi ya lugha tata au ngumu, bali kwa misingi ya ufasiri wa yaliyomo katika hadithi mahususi. Mara nyingi waandishi wa hadithi za watoto huandika na kuwasilisha hadithi zao kwa lugha ya moja kwa moja. hadithi zilizoteuliwa katika utafiti huu ambazo ni *Mwepesi wa Kusahau*, *Nampenda Mama wa Kambo*, *Madalala Abadilika*, *Cheupe na Cheusi*, *Likizo ya Mkosi na Ahaa!* Roda zote zina lugha nyepesi na mtiririko wa moja kwa moja. Yaani waandishi wake wanahadithia hadithi kwa njia ambazo watoto wanaweza kuelewa, wanaweza kubaini mawazo yaliyo katika hadithi hizo, wanaweza kubaini kiini cha hadithi hizo—mwanzo na mwisho wa hadithi, maudhui na maadili yaliyomo, n.k. Kwamba waandishi wanaweza kutumia lugha sahili; hakuna maana kwamba hadithi hizo haziwezi kuwa na undani wa kiuwasilishi unaoweza kuibua hisia, migongano au mivutano inayoakisi uhalisia wa maisha ya mtoto anayesoma hadithi hizo. Haya yanahusiana na jinsi hadithi inavyoanza, inavyokuzwa na inavyohitimishwa, vilevile jinsi hadithi inavyosawiri wahusika, inavyokuza mpito wa wakati kihali na kipahali na inavyosawiri mandhari yakiwemo mandhari ya kifamilia. Katika misingi hii, hadithi inapokuwa na mwisho mwema au chanya, inaweza kuashiria kwa mtoto kwamba siku zote wema unashinda ubaya, ukweli unashinda uongo au wema unashinda hila. Kwa hivyo, katika utafiti huu, kuna haja ya kusisitiza kwamba, kwa kuangazia mada iliyo katika hadithi na mtindo unaotumika kuiwasilisha hadithi hiyo, ni sharti hadithi za watoto ziwasilishwe kwa njia zinazoaminika. Ni sharti waandishi wabainikiwe tangu awali kwamba maneno mepesi na machache yanaweza kubeba ujumbe mzito na wenye kina cha fikira. Hadithi hizi zinaweza kuamsha katika akili za watoto mafunzo yanayoweza kudumu maishani mwao.

2.4.3 Sifa bainifu za fasihi ya watoto na ujitokezaji wa maudhui

Maudhui yanayowasilishwa katika hadithi za watoto, kwa kila hali huwalenga watoto na kwa kiasi kikubwa huwa ni maudhui ya kimaadili au maudhui ya kumdokezea mtoto uhalisi fulani wa maisha katika jamii. Wamitila (2002) anaeleza kuwa maudhui ni jumla ya masuala na mambo yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi. Hadithi kama vile *Mwepesi wa Kusahau* ina maudhui ya bidii; *Nampenda Mama wa Kambo* ina maudhui ya upendo na *Likizo ya Mkosi* ina maudhui

ya ushirikiano na uwajibikaji ambayo yote kwa jumla yanahusu maadili. Ujumbe wa hadithi ambayo mtoto anasoma unahitaji kumlenga na kumhusu mtoto msomaji na ujumbe huo unahitaji kujaribu kwa kila hali kuakisi tajriba ya mtoto huyo ili aweze kufaidi kutokana na hadithi anayosoma. Kuna matarajio ya kijumla mionganini mwa wasomi wa fasihi ya watoto kwamba, waandishi wa hadithi za watoto hawana budi kujikita kihalisi katika ulimwengu wa mtoto na kazi zao kuakisi tajriba za watoto kama vile nafasi, wajibu na majukumu yao katika familia, maadili na shughuli zao shulenii na nyumbani. Hadithi za watoto huwa na mada au wazo kuu linalolenga na linalonuiwa kuwavutia watoto. Kwa misingi hii kuna chukulizi kwamba maudhui ya hadithi hizi ni sharti yawe rahisi kujitokeza na kueleweka na watoto.

Tunaweza kusema kwamba misingi hiyo ya ujitokezaji wa maudhui na dhamira za aina mbalimbali ni baadhi ya sababu za kimsingi zinazohalalisha ufundishaji wa fasihi ya watoto. Hii ni kwa sababu, fasihi ya watoto ina uwezo wa kuasisi na kuchangia kubainika kwa uhalisi wa maisha kwa misingi ya maudhui yanayoendelezwa katika hadithi mahususi, yaani fasihi ya watoto haielezi tu juu ya uhalisi wa maisha kama unavyobainika katika hadithi, bali pia inaonyesha uchangamano wa maisha halisi kwa misingi ya maudhui yaliyoko katika hadithi na fasihi ya watoto kwa jumla. Kwa hivyo, fasihi ya watoto inatajirisha na kuimarishe uwezo wa watoto kuona, kumaizi, kufasiri na kutathmini mambo ya maisha ya kawaida. Kwa mfano, kunaweza kuwa na hadithi ambapo mtoto mhusika anatokea kuwa na mzazi mmoja, haikosi watoto wanaosoma hadithi kama hiyo watajiuliza kwa nini katika familia hii kuna mzazi mmoja. Kwa hivyo, fasihi ya watoto inaweza kuangaliwa kuwa inawasilisha mambo mengi licha ya uwasiri wa uhalisia wa hadithini, kwa maana kwamba inaongeza thamani katika kile kinachosawiriwa. Hii ni kwa sababu hadithi zinazojumuishwa katika fasihi ya watoto zinawasilisha na kuashiria mifumo na taratibu za kifamilia, mandhari anuwai ya kifamilia, mipangilio ya kuishi na mipangilio ya malazi katika familia, michakato ya utangamano katika familia na zaidi ya hayo, zinawasilisha kaida tawala katika familia na hatimaye katika jamii.

Uwasilishaji na usawiri wa mambo haya yote huchangia kuanza kubainika kwa mifumo ya kufikiri, kupanga mawazo na kuwasilisha hoja. Hii ni kwa sababu kutokana na maudhui yajitokezayo katika fasihi ya watoto, hadithi za watoto zinawasilisha nyuso au vipengele tofauti tofauti vyta maisha ya kila siku ya binadamu wa kawaida. Bakize (2014) aneleza kuwa hadithi za watoto ni kitovu cha fikira, mawazo na mitazamo ya maisha hivi kwamba mtoto anaposoma

hadithi chanya za watoto zinamwezesha kukuza mawazo chanya juu ya maisha na hata katika mustakabali wake wa maisha. Kinyume chake pia ni kweli kwamba mtoto akisoma hadithi zilizo na usawiri au mitazamo hasi ya kimaisha, mitazamo hiyo inaweza kuakisika katika maisha yake ya baadaye. Mbali na kwamba usomaji wa hadithi za watoto ni hatua ya mwanzo katika kuwaingiza watoto katika mchakato wa kutambua mikakati ya kusoma na kuandika, kuimarisha ufasaha wao wa kusoma, kukuza msamiati, kukuza stadi za ufahamu kama vile kuweza kukumbuka matukio, kutambua uteuzi wa msamiati, kubaini maudhui makuu katika hadithi fulani, wahusika na hata jinsi wanavyokuzwa. Vinginevyo hadithi za watoto ni hatua ya mwanzo katika kuimarisha stadi zao za maendelezo ya maneno. Hali kadhalika, hadithi za watoto ni muhimu pia katika kuwasilisha habari, maarifa, elimu, undani wa masuala ya maisha pamoja na burudani. Fasihi ya watoto ina uwezo wa kuwawezesha watoto kupata njia na maarifa ya kutatua matatizo yao wenyewe.

2.4.4 Sifa bainifu za fasihi ya watoto katika mkabala wa matumizi ya michoro na picha

Licha ya kuwepo kwa ushauri wa kutumia lugha nyepesi katika fasihi ya watoto, Matundura (2007) anaeleza kuwa michoro na picha hutumiwa kwa wingi katika fasihi ya watoto ili kuwasilisha ujumbe kwa mtoto kwa njia ya kutazama na kubaini matukio yaliyoko katika mchoro au picha badala ya kusoma masimulizi. Michoro na picha ni mikakati ambayo waandishi wa hadithi zote yaani *Mwepesi wa Kusahau, Nampenda Mama wa Kambo, Madalala Abadilika, Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda* wametumia. Mikakati hii imetambuliwa kwamba inamsaidia mtoto kukumbuka kisa alichosoma na kueleza ile hadithi kwa kifupi. Michoro hii inaweza kuwa inasawiri hafla za kifamilia, makutaniko ya kifamilia au hata matekelezo ya majukumu katika familia miongoni mwa mambo na shughuli nyingi za kifamilia. Si hoja michoro au picha zitakuwa ni juu ya kitu gani, kimsingi hii ni mikakati ambayo ni muhimu kwa kuwa inasaidia watoto wenyewe uwezo tofauti tofauti kuelewa haraka matini wanayosoma. Michoro hutakiwa izingatie mada ya hadithi na inase wazo kuu linalopatikana katika ukurasa ambamo picha inapatikana. Picha inapaswa kuwa katika ukurasa wenyewe matini inayorejelewa au karibu nayo, kwa mfano, ukurasa ulio mkabala na ukurasa wa picha. Picha yafaa kuwa ya kuvutia na rangi zilizotumiwa ziwe na uhalisia. Kwa mfano, kitabu cha watoto wa miaka kumi kiwe na picha za watoto wanaonekana kuwa katika kiwango hicho cha umri. Masuala ya kijinsia katika michoro ni muhimu ili isije ikawa jinsia ya kike au ya kiume imesawiriwa isivyofaa, kwa mfano, kwa njia ya kuchukiza au kuidunisha jinsia fulani. Hata

hivyo, ni muhimu kukumbuka kwamba kauli hizi zote zilizotolewa hapa juu ni kauli za kiushauri, si sheria kwa sababu kuna njia nyingi mbadala za kutumia michoro na picha; kuna njia mbadala za usawiri wa michoro na picha, inategemea mambo mengi yakiwemo uwezo na ubunifu wa mwandishi.

Wingi wa picha na umuhimu wake ni sharti utumike kwa kuzingatia viwango nya uelewa na utambuzi wa watoto kubaini yaliyo katika michoro au picha husika. Mathalani, vitabu nya watoto wa madarasa ya chini katika shule za msingi huwa na picha nyingi na kubwa kuliko vile nya watoto wa madarasa ya juu. Kwa hakika, katika kiwango hiki cha chini, picha huchukua sehemu kubwa ya kitabu kuliko maandishi. Maandishi katika ukurasa mmoja huwa machache mno kama vile sentensi moja au mbili na sehemu nyingine nzima kuchukuliwa na picha. Inadhaniwa kuwa watoto katika madarasa ya juu wanaweza kusoma na kuilewa hadithi bila msaada wa vielelezo vingi. Picha huvutia watoto kusoma hadithi, hutoa taswira kusaidia weledi na umaizi wao wa yaliyomo, huwawezesha kukumbuka hadithi wakiisoma, huipatia hadithi uhalsia na husaidia kuondoa uchovu kwa mtoto anaposoma. Picha na michoro ni njia muhimu ya kupitisha ujumbe katika hadithi za watoto. Picha huwa zinalingana na ujumbe unaopitishwa na huwa ni njia ya kueleza wazo kuu kwa muhtasari. Vitabu vilivyoteuliwa kwa utafiti huu vina picha zinazosawiri watoto katika mazingira mbalimbali ya kifamilia.

Kufikia hapa imebainika kwamba hadithi za watoto au fasihi ya watoto kwa jumla, iwe ni kwa njia ya maandishi au michoro na picha, inaweza kuwasilishwa kwa njia nyingi mbadala. Hii ina maana kwamba kuna msambao mkubwa wa hadithi za watoto na vilevile msambao mpana wa jinsi ya kuziwasilisha. Kwa hivyo, misambao hiyo ya kiuwasilishaji na mitindo ya uwasilishaji inawawezesha watoto kusoma hadithi za aina mbali mbali, na huu ni mkakati chanya wa kuwawezesha kufaulu maishani, kwa maana kwamba wanawezeshwa kubuni mbinu na mikakati ya kukabiliana na hali changamano za maisha. Kwa mfano, hali za maisha zinazowiana na hali zilizowasilishwa katika michoro na picha zinawawezesha watoto kufanya ulinganishaji. Licha ya kwamba usomaji unaimarisha stadi za utambuzi zinazohitajika katika miktadha ya masomo na baadaye katika miktadha ya ajira na utendaji kazi kwa jumla, usomaji wa hadithi za watoto una manufaa mengine mengi. Kimsingi usomaji wa hadithi za watoto unawapa watoto fursa ya kutambua hekima, busara na maadili yanayowasilishwa na fasihi katika jamii mahususi na kwa

njia hiyo kuwawezesha kujenga uelewa wa mambo na kukuza maoni yao binafsi juu ya masuala mahususi ya kijamii na kimaisha. Hii ina maana kwamba hadithi nzuri na chanya kimaudhui haiwaelezi watoto kuhusu kila kitu bali inachochea kwa njia kadha wa kadha uwezo wa watoto kukuza mitazamo ya kibinafsi juu ya masuala katika maisha yao yanayowiana na yale yanayosawiriwa katika hadithi wanazosoma. Kwa njia hii, watoto wanajifunza mbinu na mikakati ya kuhakiki, kuchanganua na kutathmini fasihi.

2.4.5 Sifa bainifu za fasihi ya watoto kwa mkabala wa mvuto na ujitokezaji wa utamaduni

Ngugi (2014) anafafanua kuwa mvuto na upokezi wa hadithi wa watoto ni jambo linalohusiana na uwepo wa utamaduni wa usomaji kwa upande mmoja na utamaduni wa utunzi na matumizi ya fasihi kwa upande mwingine. Hii ina maana kwamba mvuto unachochea upokezi wa yaliyomo katika hadithi na hii ni sifa muhimu sana katika hadithi za watoto inayochangia kujenga ile hamu ya kupenda kusoma hadithi hadi mwisho. Kwa hivyo, mwandishi wa fasihi ya watoto hana budi kuijiliza kama mada anayoandikia imekolezwa vishawishi vyta kuweza kuwavutia watoto kwa misingi kadha wa kadha kama vile kuibaini mada yenewe na kuakisika kwa uhalisia wa maisha ya mtoto katika mada hiyo. Aidha, lazima mwandishi ajilize kama mtindo anaotumia utambainikia mtoto na kama utampendeza mtoto. Kuhusiana na dhana hii ya mvuto, Wamitila (2002) anaeleza kuwa mvuto ni hisia alizonazo msomaji kumhusu mhusika fulani, tukio fulani, usawiri wa mandhari fulani au hata uwasilishaji wa mtazamo fulani. Kwa kawaida ikiwa msomaji amevutiwa na mhusika fulani atapatwa na hamu ya kutaka kujua yatakayompata. Dhana ya mvuto ni dhana changamano kwa sababu katika hadithi inaweza kuashiria vipengele vingi. Kwa hivyo, ujenzi wa mvuto katika hadithi za watoto ni sharti uwe na mtazamo wa watoto. Watoto hufikiria kwa njia tofauti na watu wazima na si lazima wafurahishwe na mambo yanayowafurahisha watu wazima. Wao basi hutekwa na kazi iliyoandikwa kwa matarajio na matamanio yao kulingana na wakati wanamoishi.

Ngugi (2014) anaeleza kuwa umbo la kitabu na michakato ya utoaji wa kitabu kilicho na hadithi za watoto ni dhana inayokita kuwili, katika utamaduni wa kisanaa na utamaduni wa kibidhaa au utamaduni wa vifaa vya kijamii. Mambo kama vile ukubwa wa kitabu cha hadithi, muundo wa kitabu, umbo la kitabu, taipografia au aina ya maandishi, ubora wa karatasi, mvuto wa jalada na anwani ya kitabu huwavutia watoto kukipenda kitabu mahususi. Katika fasihi ya watoto jalada

aghalabu huwasilisha kwa ufupi dhamira ya mwandishi. Taswira au ujumbe ambao mtoto anapata kwenye jalada unaweza kumpa msukumo wa kuisoma hadithi yenyewe. Karatasi inayotumiwa katika vitabu vya hadithi za watoto yafaa kuwa ngumu ili isiraruke kwa urahisi. Karatasi ziwe zimeunganishwa kwa njia imara. Hii ni kwa sababu watoto huweza kukunja vitabu wanapovisoma au pengine kuvirusha na hata kuvichezea. Kiasi cha ukubwa wa maandishi kilingane na kiwango cha watoto wanaokusudiwa kusoma. Kwa mfano, maandishi ya watoto wadogo yawe makubwa kuliko ya watoto wakubwa. Maandishi au taipografia ya hadithi za watoto huwa na ukubwa unaolingana na kiwango cha watoto wanaolengwa. Kazi za watoto wa madarasa ya chini, ambao ndio wanaanza kujifunza kusoma, huwa na maandishi makubwa sana ili kumwezesha mtoto atambue herufi haraka na kuweza kusoma. Zile za watoto wa madarasa ya kati pia huwa na maandishi makubwa kiasi kuliko zile za watoto wa madarasa ya juu katika shule za msingi. Anwani ya kitabu na picha ya jalada ni muhimu kutiliwa maanani katika fasihi ya watoto. Anwani fupi ni bora kuliko anwani ndefu kwa vile hukumbukika kwa urahisi. Mtoto atawea kukumbuka hadithi aliyosoma haraka ikiwa atakumbuka anwani. Ni muhimu tena kukumbuka kuwa hizi ni kauli za kiushauri, hazikiti katika misingi ya sheria ikizingatiwa kuwa kuna njia nyingi mbadala za ujenzi wa mvuto, ubunifu wa umbo na aina ya kitabu kinachoweza kutolewa.

Usomaji wa hadithi za watoto kwa misingi hii ya kuzingatia mvuto, umbo na masuala mengine ya utolewaji wa vitabu unawapa fursa kutambua na kutathmini urithi wao wa kitamaduni, kwa mfano, utamaduni wa kusoma, utamaduni wa sanaa na mambo mengine ya kitamaduni yanayowezeshwa na usomaji wa fasihi ya watoto. Mbali na utamaduni huu wa kibidhaa unaoonekana, kuna pia uwezekano wa uwasilishaji wa mila, desturi, imani na michakato ya kitamaduni ndani ya hadithi zinazowasilishwa katika vitabu hivyo, ambapo mtoto anaposoma hadithi hizo anaweza kutambua utamaduni unaowiana na utamaduni wake na pia kutambua urithi wa utamaduni wa watu wengine. Hii inaweza kufasiriwa kuwa inachangia watoto kukuza mitazamo chanya inayotambua utamaduni wa watoto, upekee walionao na vilevile kutambua uchanya na upekee wa tamaduni nyinginezo. Hizo ni nguzo muhimu za maisha ila haziwezi kukuzwa ikiwa vitabu vya fasihi ya watoto au hadithi za watoto zenyewe zinawasilisha usawiri wa dhana za kibaguzi, dhana dhalilishaji au shutma na bezo dhidi ya tamaduni fulani mahususi. Dhana hizi chanya au hasi zinaweza kujitokeza sio tu katika usawiri wa tamaduni bali pia katika

usawiri wa aina na mifumo ya kifamilia. Kwa mfano, iwapo hadithi katika mkusanyiko fulani inabeza aina fulani ya familia, kuna uwezekano wa watoto kukua wakiwa na mitazamo hiyo ya kubeza au kuathirika pale familia inayobezwa inaakisika katika maisha ya mtoto anayesoma hadithi kama hiyo.

Masuala yanayohusiana na mandhari katika hadithi za watoto kwa namna fulani yanahusiana na hali fulani fulani za kitamaduni. Aghalabu uwasilishaji na usawiri wa mandhari huwa ni wa aina nyingi japo kwa kiasi kikubwa mazingira ambayo yanahusishwa na shughuli au matendo ya watoto na maisha yao kama watoto, huhitaji uhalisi wa kiuwasilishi hivi kwamba wanaposoma hadithi husika waweze kujitambulisha nazo. Mazingira haya ni kama vile mazingira halisi ya shulen i kama vile katika *Mwepesi wa Kusahau*; mazingira ya kifamilia nyumbani kama vile katika *Nampenda Mama wa Kambo* na *Cheupe na Cheusi* na njiani kama vile katika *Likizo ya Mkosi* kuakisi uhalisi wa watoto watokapo katika miktadha ya kifamilia na warudipo katika miktadha hiyo. Haya yanaweza kuwa ni mandhari yanayofahamika kwa urahisi na watoto kwa kuwa watoto mara nyingi huwa katika shughuli za nyumbani au za shulen. Majina ya watoto hawa pia yanawakilisha jamii maana ni majina yanayofanana na yale yanayopewa watoto halisi katika mandhari yanayotambulikana kijamii. Mandhari ni mahali na kipindi cha wakati kinachohusishwa katika hadithi.

Inaweza kudaiwa kwamba hadithi za watoto sawia na zilivyo hadithi za watu wakubwa huwa na mgogoro, lakini migogoro hiyo hubainika na kueleweka inapokitwa katika miktadha maalum. Mgogoro unaweza kufafanuliwa kuwa ni mvutano baina ya pande mbili au zaidi ambazo zina misimamo inayotofautiana juu ya jambo mahususi. Ili hadithi iweze kuwa na mvuto sharti kuwe na migogoro baina ya wahusika. Migogoro hii huchangia maudhui na hufunuka tokea mwanzo na kufikia pahala ikawa ina upeo na pengine utatuzi wake. Migogoro, kwa mfano, yaweza kutokana na mvutano baina ya watoto katika familia au kati ya watoto na wazazi wao kama vile mgogoro wa Juma na mama yake katika *Mwepesi wa Kusahau* au mogogoro wa Cheupe na mama wa kambo katika *Cheupe na Cheusi*. Uwepo wa migogoro na utatuzi wa migogoro hiyo katika hadithi za watoto ni kipengele muhimu katika kuwawezesha watoto kujifunza mambo mengi. Katika kuwakutanisha watoto na migogoro aina mbalimbali katika hadithi, fasihi ya watoto inawawezesha watoto kukuza maarifa ya kihisia na ubunifu wa kuwaza, inachangia

kukuza hulka ya mtoto pamoja na kumwezesha kutambua stadi chanya za mahusiano ya kijamii. Hii inatokana na ukweli kwamba hadithi nyingi za watoto zina nyakati, matukio na vipindi vyamizozo, ugomvi, mapambano na mahangaiko ambapo wahusika hushurutika kufanya maamuzi, kwa mfano, kufanya maamuzi katika misingi ya kimaadili na kuhalalisha sababu za kufanya maamuzi hayo. Maamuzi haya yanaweza kutokea katika miktadha ya kifamilia, kwa mfano, kama vile kukabiliana na hali za uhaba wa chakula, ugawanyaji wa mali katika familia, kuugua na kuuguza mwanafamilia au hata kutokea kwa kifo katika familia. Kwa misingi hii, jinsi hadithi inavyosawiri mianzo, sababu na utatuaji wa mizozo katika familia kunaweza kuchangia kukuza watoto kihisia. Kwa vyovyyote vile, hadithi za watoto ni nguzo muhimu katika kuwawezesha watoto kufikiria mambo na matukio kwa undani.

2.5 Dhima ya fasihi ya watoto

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuangazia uamili na dhima ya fasihi ya watoto katika miktadha ya aina mbalimbali. Hunt (2002) katika utafiti wake anaeleza kuwa fasihi ya watoto ni muhimu kwa kuwa inaweza kutumika kuwaelimisha na kuwafahamisha watoto juu ya mambo mbalimbali katika jamii yao na kwamba ina uwezo na imekuwa na uamili na ushawishi wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja kuhusiana na makuzi ya watoto kimaadili, kilugha, kitamaduni na kisiasa. Hunt anatoa mfano kuwa watu wengi wazima walio mamlakani walisoma vitabu vya hadithi za watoto walipokuwa wadogo na bila shaka itikadi zinazotokana na vitabu walivyosoma vilikuwa na ushawishi fulani katika ukuaji na maendeleo yao. Miricho (2015) anatoa maoni kuwa hadithi za watoto si maandishi ya vichekesho na vituko visivyo na uhusiano na maisha ya kawaida katika jamii ambamo familia huwemo. Hadithi hizi hubuniwa kutokana na mambo halisi yanayoendelea katika jamii zikilenga kuifahamisha jamii mambo yaliyo mazuri na yale mabaya. Matukio na mandhari huwa ya kweli au yenyewe uhusiano na hali halisi ya ulimwengu unaomzunguka mtoto. Hivyo basi, hadithi za watoto ni sanaa inayoelezea maisha ya watoto kwa njia bunifu inayojikita katika misingi na kaida zinazotawala maisha halisi ya jamii kisosholojia.

Kama fasihi nyingine, lengo kuu la fasihi ya watoto ni kuburudisha. Watoto husoma kama njia ya kujistarehesha. Fasihi ya watoto huburudisha kupitia kugusa hisia za watoto wakafurahi na pengine kucheka. Maudhui ya hadithi pamoja na fani zilizotumiwa huibua hisia za furaha na

kuchangamsha. Warren na Wellek (1973) wanaeleza kuburudisha huku kama kuburudisha kwa udhati kwa kuwa burudani ya kazi ya kifasihi ni burudani inayolelimisha. Maudhui ya hadithi pamoja na fani zilizotumiwa huibua hisia za burudani na kustarehesha. Waandishi hutumia lugha teule inayogusa hisia za mtoto anayesoma na kumfanya ahisi kutosheka au kuridhika anapoisoma ile hadithi. Picha na michoro iliyomo huweza kuchangamsha na kuleta burudani wakati wa kusoma. Kimsingi, watoto hupata hamu ya kusoma hadithi kama njia ya kutimiza mahitaji yao ya kiudadisi na shauku. Msukumo wa kusoma aghalabu hutokana na mwalimu kuwapa vitabu fulani wasome au kutokana na kuvutiwa na jalada la kitabu na hivyo kuwa na hamu ya kujuu hadithi iliyomo.

Fasihi ya watoto hukuza stadi ya kusoma. Lengo moja la kuwaandikia watoto fasihi ni kuwasaidia kumudu kusoma, kutambua mipangilio ya kimaandishi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na kusoma. Kupitia vitabu hivi wataweza kutambua herufi na sauti za herufi hizo na kisha kuunganisha sauti za herufi kusoma silabi na hatimaye kuunganisha silabi kusoma maneno. Mtoto kama huyu anapotambua kuwa amepiga hatua na kufanikiwa katika usomaji ataridhika kisaikolojia na jambo hili litampa motisha ya kuendelea kusoma hadithi zaidi.

Fasihi ya watoto pia hukuza stadi ya kuandika. Miricho (2016) anaeleza kuwa kusoma vitabu vya hadithi hukuza stadi ya kuandika mbali na kumjenga mtoto kilugha kwa kuwa kutokana na hadithi anazosoma atawenza kupata mawazo atakayoweza kutumia anapoandika insha shulenii na hivyo kukuza ubunifu wake. Vitabu vya hadithi za watoto huwakuza kimawazo na kuchochea fikira za ubunifu mionganii mwao huku vikiwapa hamu ya kutaka kujuu mengi. Watoto hukuza lugha na kujenga msamiati wanaposoma hadithi. Kwa hakika, katika shule za msingi ni muhimu watoto kusoma vitabu vya hadithi ili waweze kujenga lugha watakayotumia katika uandishi wao wa insha. Usomaji wa vitabu vya hadithi utawasaidia kujiimarisha kisarufi, kimsamiati na kujifunza uakifishaji ili kukuza uwezo wao wa kuandika. Miricho (2016) anaendelea kueleza kuwa usomaji wa hadithi pia humpa mtoto ujuzi wa kuendeleza maneno, ujuzi wa kutumia viakifishi mbalimbali katika maandishi, ujuzi wa miundo mbalimbali ya sentensi, matumizi ya fani mbalimbali za uandishi na ujuzi wa sarufi na msamiati. Usomaji wa vitabu vya hadithi utawasaidia kujiimarisha kisarufi, kimsamiati na kujifunza kutumia alama za uakifishaji kama vile vituo, vinukuu, viulizi na herufi kubwa. Jambo hili hukuza uwezo wao wa kuandika. Kwa

hakika, waandishi wengi wenye sifa wamekiri kuwa walisoma vitabu vingi vya hadithi katika shule za msingi na hivyo wakakuza stadi ya usomaji na uandishi. Walimu walio na hamu ya kuona wanafunzi wao wakiandika insha za kiwango cha juu ya wastani hawana budi kuhakikisha wanafunzi wanasoma vitabu vingi vya hadithi.

Fasihi ya watoto ina dhima ya kuelimisha na kupanua mawazo ya watoto. Kusoma humsaidia mtoto kuuelewa ulimwengu wake vyema na kupanua muono ulimwengu wake. Hadithi za watoto huwaelimisha na kuwafunza jinsi ya kukabiliana na matatizo ya ulimwengu au ya jamii. Mwandishi wa hadithi huweza kuelimisha ama kimakusudi au kisadfa kutokana na maudhui yaliyomo. Licha ya hayo, mtoto shulen i anaposoma hadithi ataweza kupata mawazo atakayoweza kutumia anapoandika insha na hivyo kukuza ubunifu wake. Vitabu vya hadithi za watoto huwakuza kimawazo na kuchochea fikira za ubunifu mionganoni mwao huku vikiwapa hamu ya kutaka kujuu mengi. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuelimisha huku hutokana na yanayosimuliwa kwenye hadithi. Hadithi hizi hufunza jinsi ya kukabiliana na matatizo katika familia na jamii pana. Kwa mfano, katika *Mwepesi wa Kusahau* mwandishi anapomwangazia mama zaidi kuliko baba katika shughuli za kifamilia kama vile malezi ya watoto ya kila siku, anaishia kumsawiri baba kama mtu aliyewekwa pembeni katika ulezi wa watoto. Vilevile, baba na mama wanapofanywa na mwandishi waonekane kushirikiana katika malezi ya watoto na pia kuhusisha babu na nyanya kama vile katika *Likizo ya Mkosi*, mwandishi anatusawiria familia pana iliyo na ushirikiano.

Fasihi ya watoto ina jukumu la kuadilisha kwa kutoa mawaidha, maonyo na maelekezo. Huonya, kwa mfano, dhidi ya upumbavu au vitendo vinavyoolekeana na hali za upumbavu. Ngugi (2014), akimnukuu Cass (1967) anapendekeza kuwa hadithi za watoto zinahitaji kuonyesha wema unashinda uovu. Watoto huvutiwa na hadithi ambazo wavulana, wasichana na wanyama watundu huadhibiwa kwa sababu ya vitendo viovu. Watoto huridhika kuona haki imetendeka maovu yanapoadhibiwa. Watoto huamini kuwa mtu akitenda ubaya anafaa kuadhibiwa. Hadithi za watoto aghalabu huangazia masuala ibukayanayoikabili jamii na wakati mwingine hutoa suluhisho. Hivyo basi, watoto wanapozisoma hupata ufanuzi wa masuala yanayowatatiza katika maisha yao. Hadithi hizi hutuchorea taswira ya uhalisi wa maisha ya jamii kwa njia ya ubunifu.

Miricho na Mbuthia (2017) wanaelezea kuwa usomaji wa fasihi ya watoto unaweza kuwaathiri kwa njia chanya au hasi watoto wanaposoma. Hivyo, ni muhimu kutilia maanani usawiri wa kifamilia unaojitokeza katika hadithi za watoto. Kwa jumla, hadithi za watoto huathiri hisia na matarajio yao katika jamii wanamoishi. Usawiri wa wahusika watoto unaweza kuathiri uamuzi watakaota watoto wanaosoma vitabu vya hadithi. Hii ni kwa sababu wanapokea ujumbe wanaoandikiwa na wanaweza kukumbuka kwa urahisi yale waliyosoma hasa ikiwa ujumbe huo una ukweli fulani kuhusu maisha yao katika jamii. Hivyo basi, ipo haja ya kuhakiki vitabu vya hadithi za watoto ili kuhakikisha kwamba watoto watasoma yale yanayofaa kwa ajili ya kuwajenga kimaadili na kuwapa mielekeo inayofaa katika familia ili jamii iwe na vizazi bora vya siku za usoni.

Hapana shaka kwamba hadithi za watoto zina uwezo wa kuchochea na kuchangia kukuza ubunifu kwa maana kwamba zinapowasilisha hadithi chanya, hadithi hizo zinaweza kuwa miigo, hali zinazochochea kupanua mawazo ya watoto na pengine hali zinazochochea kubuni mambo kihalisi. Mbali na kukuza uwezo wa kiubunifu na kiutambuzi, fasihi ya watoto inaweza na kwa kweli huwa inachangia kukuza hulka ya watoto pamoja na ukuaji wao kijamii. Kwa sababu ya urahisi wa kuathirika na kukubali yanayowasilishwa katika hadithi wanazosoma watoto, hadithi hizo zinaweza kuchangia kuwakuza kuwa watoto na hatimaye watu wazima wanaojali wenzao, watu walio na akili razini, werevu na wepesi wa kujenga urafiki na watu wengine. Fasihi ya watoto inaweza kuchangia kupiga vita tabia za ubinafsi, ubahili, choyo na tabia nyinginezo zinazokataliwa na jamii. Haya ni mambo ambayo sio tu yanajitokeza katika familia bali yanaathiri makuzi ya watoto. Kukua kijamii kunaweza kutokana na watoto kusoma hadithi zinazowawezesha kuona jinsi watu wanavyohusiana katika miktadha ya kijamii, hasa pale ambapo watoto wanawezeshwa kutambua hali tofauti za watoto wenzao. Kwa mfano, katika misingi ya maumbile—jinsia, ulemavu na misingi ya hali—utajiri na umasikini. Hadithi za watoto zina uwezo wa kukuza thamani ya kudumu kwa maana kwamba baadhi ya hadithi wanazosoma zinasalia akilini mwao katika maisha yao yote. Miricho, Sheila na Nabea (2019) wanaeleza kuwa fasihi ya watoto ina nafasi muhimu katika kumwezesha mtoto kuelewa masuala yanayomzingira. Hivyo, thamani ya fasihi ya watoto haishii na kusalia katika miktadha ya shule bali ina manufaa nje ya mipaka ya shule.

2.6 Wasifu wa muundo katika fasihi ya watoto

Katika misingi ya kiuelekezi, urefu wa hadithi za watoto katika fasihi ya watoto wafaa uwe wa kiasi kinachoweza kudhibitiwa na akili ya watoto kwa kuwa watoto hupenda vitabu ambavyo watasoma na kuvimaliza katika kikao kimoja. Kisa katika hadithi za watoto aghalabu huchukua kipindi kifupi kiwakati kusimuliwa. Hivyo, hadithi za watoto huwa fupi na za kiutendaji. Hii ni kwa sababu hadithi ikiwa ndefu itawachosha watoto wanaosoma na watakosa hamu ya kuisoma na kuimaliza. Msuko wa hadithi za watoto wafaa kuwa mwepesi na wa moja kwa moja. Kwa mfano, mbinu rejeshi huepukwa ili wasomaji wa umri mdogo wanaolengwa waweze kufuata kisa kwa wepesi kutoka mwanzo, kilele hadi mwisho na kuelewa bila kuchanganyikiwa wala kuchoka. Kitabu kizuri cha mtoto ni kile ambacho mwandishi amefaulu kuwasiliana moja kwa moja na mtoto anayelengwa. Watoto mara nyingi huvutiwa na mtindo unaotumia usemi halisi kwa wingi. Mtindo wa usemi halisi huipa hadithi uhai zaidi kuliko maandishi ya kimaelezo. Hizi ni sifa zinazojitokeza kwa uwazi katika kazi zilizoteuliwa katika utafiti huu.

Fantasia yaweza kutumika katika hadithi za watoto. Fantasia ni dhana inayotumiwa kuelezea kazi ya fasihi ambayo ina sifa ambazo zinakiuka hali halisi. Sifa hii inamaanisha kuwa huwepo mambo mengi ya ajabu ajabu ambayo kwa kawaida hayatokei katika maisha ya kila siku. Jasira au vitendo vya kishujaa pamoja na mapambano yanayotokea huvutia watoto. Wamitila (2008) anasema kuwa mhimili mkubwa katika fasihi ya watoto ni tendo kuu, jasira na usimulizi wa jasira hiyo pamoja na mapambano yanayotokea. Ngugi (2012) anaeleza kuwa hadithi za kijasira ni zile ambazo huonyesha ujasiri katika kukabiliana na hali mbalimbali zilizo ngumu. Tukio la kijasira, kwa mfano, ni safari inayokumbwa na matatizo. Usimulizi wa hadithi unaweza kujengwa kwenye maelezo ya jinsi mhusika mkuu anavyokabili vikwazo njiani na hatimaye kutumia mbinu za uvumbuzi na kuishia kufanikiwa, kwa mfano, katika safari ya kutoka kwenye msitu fulani, uwindaji msituni, maisha bila wazazi au changamoto shulen. Mbatia (2016) anatoa mfano wa jasira kwa kuzungumzia hadithi mashuhuri ya *Elisi katika Nchi ya Ajabu (Alice's Adventures in Wonderland)*. Hadithi hii inatokana na ndoto ya Alice ambayo inahusu jinsi anavyopitia jasira kadha za ajabu. Kwa mfano, anamkimbiza sungura hadi shimonii mwake na kujikuta akiwa katika ulimwengu wa ajabu. Kinachohitaji kukumbukwa ni kwamba hata katika misingi ya fantasia kunaweza kusawiriwa mifumo kadha wa kadha ya kifamilia.

Hadithi zilizoandikiwa watoto huwa na tataruki. Miricho (2016) anaeleza kuwa tataruki ni hali ya kutarajia kwa hamu kujua kitakachotokea baadaye. Ili kusababisha tataruki, tukio laweza kuwa linadokezwa kidogo kidogo hadi baadaye ambapo litatokea kama lilivyotarajiwa au tofauti na ilivyotarajiwa. Watoto wanaposoma hadithi huwa na hamu ya kutaka kujua zaidi kuhusu yatakayotokea mwishoni. Waandishi wa hadithi za watoto huhusisha watusika wanaotaka kupata kitu fulani lakini wanaokabiliwa na vikwazo mbalimbali. Hali hii ya tataruki humpa mtoto hamu ya kusoma ili ajue hadithi itakavyoishia. Mwanzo wa hadithi lazima uwe wa kuvutia ili kumteka msomaji na kumtosa katika ulimwengu mpya. Hadithi imalizikapo iache msomaji na athari kama vile mshangao, funzo au wazo fulani. Mwanzo na mwisho wa hadithi hizi kwa kawaida huibua hisia za burudani. Funzo kuu la hadithi hujitokeza kwa urahisi mwanzoni au mwishoni mwa hadithi huku likimshajiisha mtoto msomaji na kujenga uadilifu ndani yake. Watoto huvutiwa na hadithi zinazoathiri hisia na matarajio yao katika jamii na familia.

2.7 Hitimisho

Katika sehemu hii mumejadiliwa sababu na uamili wa kusomwa na kufundishwa kwa fasihi ya watoto, historia na maendeleo ya fasihi ya watoto, hali kadhalika kumebainishwa sifa bainifu za fasihi ya watoto, dhima ya fasihi ya watoto na wasifu wa muundo katika fashi ya watoto. Kutohana na utafiti huu imebainika kuwa hadithi za watoto zina sifa maalum ambazo zinazitambulisha. Sifa hizo zinahusisha dhana kadhaa zikiwemo watusika watoto, ufupi, lugha nyepesi, picha, ukubwa wa maandishi, msoko mwelesi, maudhui yanayolenga watoto, fantasia, mvuto, tataruki na mwisho wa kusisimua. Dhima ya fasihi ya watoto katika jamii ya sasa imejadiliwa na ni kama vile kuburudisha, kuadilisha, kuelimisha, kukuza lugha, kuchochea fikira na hata masuala ya kifamilia. Sehemu hii inaonyesha kwamba misingi hiyo ya ujitokezaji wa maudhui na dhamira za aina mbalimbali, ni baadhi ya sababu za kimsingi zinazohalalisha ufundishaji wa fasihi ya watoto. Hii ni kwa sababu, fasihi ya watoto ina uwezo wa kuasi na kuchangia kubainika kwa uhalisi wa maisha kwa misingi ya maudhui yanayoendelezwa katika hadithi mahususi, yaani fasihi ya watoto haielezi tu juu ya uhalisi wa maisha kama unavyobainika katika hadithi, bali pia inaonyesha uchangamano wa maisha halisi kwa misingi ya maudhui yaliyoko katika hadithi na fasihi ya watoto kwa jumla. Kwa hivyo, fasihi ya watoto inatajirisha na kuimarisha uwezo wa watoto kuona, kumaizi, kufasiri na kutathmini mambo ya maisha ya kawaida. Kwa hivyo, fasihi ya watoto inaweza kuelezea kuwa inawasilisha mambo

mengi kiuhalisia. Hii ni kwa sababu hadithi zinazojumuishwa katika fasihi ya watoto zinawasilisha na kuashiria mifumo na taratibu za kifamilia, mandhari anuwai ya kifamilia, mipangilio ya kuishi na mipangilio ya malazi katika familia, michakato ya utangamano katika familia na zaidi ya hayo, zinawasilisha kaida tawala katika familia na hatimaye katika jamii. Uwezo wa fasihi ya watoto kuwasilisha na kusawiri uhalisia wa masuala ibuka katika jamii huifanya iwe kitovu cha fikira, mawazo na mitazamo ya maisha hivi kwamba mtoto anaposoma hadithi chanya za watoto zinamwezesha kukuza mawazo chanya juu ya maisha na hata katika mustakabali wake wa maisha. Fasihi ya watoto ina uwezo wa kuwawezesha watoto kupata njia na maarifa ya kutatua matatizo yao wenyewe.

SURA YA TATU

**USAWIRI WA FAMILIA YA KISASA KATIKA MWEPESSI WA KUSAHAU,
NAMPENDA MAMA WA KAMBO NA MADALALA ABADILIIKA**

3.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa hadithi zinazojumuishwa katika utafiti huu za kipindi cha mwaka 2000 – 2010 ambazo ni *Mwepesi wa Kusahau* (2005), *Nampenda Mama wa Kambo* (2006) na *Madalala Abadilika* (2009). Pili sura hii inaibua na kujadili aina za familia zinazosawiriwa katika *Mwepesi wa Kusahau*, *Nampenda Mama wa Kambo* na *Madalala Abadilika*. Vilevile, inajadili usawiri wa familia kama taasisi katika *Mwepesi wa Kusahau*, *Nampenda Mama wa Kambo* na *Madalala Abadilika* na mwisho mjadala unatamatishwa kwa kuangazia jinsi uhalisi wa kifamilia katika miktadha razini unavyoakisika katika *Mwepesi wa Kusahau*, *Nampenda Mama wa Kambo* na *Madalala Abadilika*.

3.2 Muhtasari wa vitabu vya hadithi vilivyoteuliwa vya kipindi 2000 - 2010

Katika sehemu hii kunatolewa muhtasari wa hadithi zilizoteuliwa. Muhtasari huu unasaidia kuangazia japo kwa ufupi maudhui yanayojitokeza katika hadithi hizi, vilevile kuangazia sifa za wahusika na usawiriwa familia kwa nia ya kuweka msingi wa kuchunguza aina za familia zinazosawiriwa katika kipindi cha mwaka 2000-2010. Aidha, muhtasari huu wa hadithi unaangazia jinsi uhalisi wa kifamilia katika hadithi teule unavyoakisika.

3.2.1 Muhtasari wa *Mwepesi wa Kusahau*

Mwepesi Wa Kusahau ni hadithi ambayo ina wahusika binadamu. Wahusika wakuu ni watoto ambaeo ni Juma na Maria. Juma ni mvulana na Maria ni msichana. Watoto hawa walifanana kama shilingi kwa ya pili. Baba yao aliitwa Hamisi Akida ambaye alikuwa tabibu wa mifugo wilayani Kericho. Naye mama yao aliitwa Lilian Mokeira na alikuwa muuguzi mkuu wa hospitali ya wilaya hiyo. Wazazi hawa waliwapenda sana watoto wao na walihakikisha waliwapa malezi bora na elimu kwani waliamini ya kwamba elimu ndiyo ufunguo wa maisha.

Juma na Maria walikuwa wanafunzi wa darasa la nne katika shule ya msingi ya Jengahekima. Ingawa wote walipenda kwenda shuleni, tabia zao zilitofautiana. Maria alikuwa mwanafunzi msafi na mwenye bidii za mchwa masomoni. Hakusahau jambo lolote kwa urahisi. Alipendwa mno na walimu na wazazi wake. Kwa upande mwingine Juma alikuwa na matatizo mengi. Yaani hakutilia masomo maanani alikuwa na tabia ya kusahau mambo haraka. Pia alikuwa mwanafunzi mchafu kwa njia nyingi. Maria aliiga mambo yote mazuri kutokana na wazazi wake, walimu na wanafunzi wenzake. Wakati mwingine Maria aliyaandika maagizo yote aliyopewa na walimu wake kwenye shajara ili asije akasahau jambo lolote. Tabia hii ya kuandika ilikuwa imetokana na alivyo kuwa anamwona baba yake Bw. Akida alivyo andika kumbukumbu zake kwenye shajara. Siku moja Maria aliamka kama kawaida aliposikia jogoo akiwika. Alianza kujitayarisha ili aende shuleni. Alimuita ndugu yake Juma ambaye alikuwa amelala fofofu ili aamke. Licha ya kumwamsha alijinyoosha kisha akarudi kulala kwani alikuwa na usingizi mzito. Alilala na kukoroma mithili ya chura. Mama yao Juma na Maria alihakikisha kila wakati amewashughulikia wanawe asubuhi na mapema kwa kuwatayarishia kiamsha kinywa na mambo sawia na hayo. Hili jambo linaonekana wazi tunapoeleza hivi:

Maria alipokuwa anatoka nje kwenda kupaka viatu vyake rangi,
alimkuta mama yake amekwisha tayarisha kiamsha kinywa.
Alikuwa sasa anaandika meza (uk. 18).

Juma alipoamka Maria alikuwa anamalizia kunywa chai. Ilikuwa saa mbili kasorobo asubuhi. Matayarisho kamili ya kuwa tayari kwenda shuleni hayangefanyika kwa muda wa nusu saa tu. Hii ni kwa kuwa Juma hakuwa amekunywa chai, kutandika kitanda, kuchana nywele na mambo mengine yanayohusiana na kuijandaa asubuhi. Juma alikuwa pia amesahau ni wapi alipokuwa ameiweka kalamu yake ilhali kulikuwa na mtihani siku hiyo. Mama yake ndiye aliyemwokoa kwa kumwambia ashike nywele zake kichwani ili kuipata kalamu aliyokuwa ameidunga nyweleni na kisha kusahau ilipokuwa. Juma aliondoka shoti kama farasi kuelekea shuleni. Tayari alikuwa amechelewa na mwalimu Madenge alimwona na kumwita. Juma alijifanya hasikii na kuendelea kukimbia ambapo alikimbizwa na mwalimu mpaka akamkamata. Mwalimu alimpeleka mpaka hapo mbele ya wanafunzi wote. Maria alii twa na mwalimu na pamoja na Juma wakasimamishwa mbele ya wanafunzi kwenye paredi. Kwa kuwalinganisha, wanafunzi hawa wawili Juma na Maria walikuwa tofauti kabisa. Maria alikuwa nadhifu wa kutamanika ilhali Juma alikuwa mchafu kama fuko. Siku hiyo Juma alihai bika vya kutosha hadi akaamua

kuzika tabia zake mbaya na kuiga mfano mwema kama wa dada yake Maria. Maudhui muhimu yanayojitokeza katika hadithi hii ni yale ya maadili kama vile ushirikiano, upendo, bidii na uwajibikaji. Maudhui mengine ni elimu ya watoto. Haya yanatoa mafunzo yatakayowafaa watoto wasomaji.

3.2.2 Muhtasari wa *Nampenda Mama wa Kambo*

Nampenda Mama wa Kambo ni hadithi ambayo wahusika wake ni binadamu. Wahusika hawa ni wengi katika familia moja lakini mhusika mkuu ni mtoto anayeitwa Naliaka. Naliaka ni msichana ambaye anaishi na baba yake na mama wa kambo. Anasoma darasa la nane katika shule ya msingi ya Ebuchinga karibu na mji wa Kakamega. Baba yake Naliaka anaitwa Peter Weswa na mama yake wa kambo anaitwa Ann Achieng; ingawa watu wamezoea kumwita mama Wafula. Katika familia ya Naliaka, wako wana wanenye. Naliaka ndiye mkubwa na ana umri wa miaka kumi na mitano, Wekesa aliye darasa la pili ana umri wa miaka saba na wako katika shule moja. Wafula ana umri wa miaka mitano na anasomea katika shule ya malezi karibu sana na nyumbani. Naye kitinda mimba anaitwa Nasimiyu ambaye ana miaka miwili.

Naliaka ndugu yake wa toka nitoke ni Wekesa. Ndugu zake wa kambo ni Wafula na Nasimiyu. Wote wanapendana kama chanda na pete. Mama yake Naliaka alikuwa wakati alipoenda kujifungua Wekesa. Usiku huo mama yake alipelekwa hospitali akiwa na maumivu makali ya uzazi. Alipelekwa na baba yake Naliaka. Naliaka alibaki na shangazi yake ambaye ni dada mdogo wa baba yake. Baba yake Naliaka hakurudi nyumbani jioni hiyo wala mchana wa siku iliyofuata. Alirudi jioni yake akiwa ameishiwa na raha. Naliaka alimuuliza habari ya mama yake.

Hapo ndipo aliambiwa kuwa mama yake aliaga dunia. Aliendelea kumwambia kuwa ndugu yake yu hai ambaye ni wa kiume na alizaliwa kabla mama yake kufariki. Naliaka alisema kuwa kwa kweli maisha bila mzazi mmoja huwa magumu. Alihuzunika sana na kuanza kuijuliza maswali. Jambo hili linadhahirika vyema katika ukurasa wa 4 ambapo Naliaka alijiuliza wangeishi vipi bila mama. Alishangaa ni nani angewapikia na kuwafulia nguo na kumsimulia hadithi za kale.

Shangazi yake Naliaka alimkumbatia Naliaka bila kusema chochote. Baadaye alimpangusa machozi, akatulia na usingizi ukamchukua. Mazishi yaliandaliwa na mama yake Naliaka

akazikwa. Baadaye baba yake Naliaka na shangazi yake walikwenda kumchukua mtoto Wekesa hospitalini. Nyumbani walisaidiana kumlea Wekesa. Kazi ya kumlea Wekesa ikawa ngumu. Siku moja babake Naliaka alimwita Naliaka na akamweleza anataka kuoa tena. Hii ni kwa sababu baba yake alihitaji mtu wa kusaidiana naye maishani. Naliaka alinyamaza kisha akasema kuwa yeche huwa anasikia mama wa kambo ni wabaya sana. Baba yake Naliaka akamjibu sio mama wa kambo wote ni wabaya wengine ni wazuri. Mwishowe Naliaka akakubali shingo upande na kumwahidi baba yake kwamba huyo mama wa kambo akimtesa hatanyamaza atamwambia. Siku iliyofuata huyo mwanamke Ann Achieng akahamia kwa akina Naliaka. Naliaka mwanzo alimchukia mama huyo wa kambo kulingana na alivyokuwa amewasikia rafiki zake wanaoishi na mama wa kambo wakisema jinsi wanavyoteswa na mama wa kambo. Naliaka akiambiwa afanye jambo alikataa na kusema anateswa. Akifanyiwa mema hakuwa na shukurani kwa sababu aliyachukulia ni utani. Baadaye, mama wa kambo alimweleza Naliaka kwamba pia yeche alifiwa na mama yake akiwa na umri wake na mama wa kambo hakumtesa. Alimwahidi ambavyo atampenda hata atamrekebisha akikosa. Jambo hili linaonekana wazi Naliaka anapokiri hivi:

“Polepole nikaanza kusahau mama yangu na kumpenda
(mama wa kambo). Marafiki hawakuamini nilipowaambia
mama Wafula alikuwa tofauti kabisa na mama wengine
wa kambo” (uk. 11).

Kimsingi maudhui yanayojitokeza katika hadithi hii vilevile, ni yale ya maadili kama vile upendo, ushirikiano, elimu, bidii na uwajibikaji. Maudhui kama haya hujitokeza sana katika hadithi za watoto ili kuwapitisha mafunzo fulani.

3.2.3 Muhtasari wa *Madalala Abadilika*

Madalala Abadilika ni hadithi ambayo ina wahusika binadamu. Wahusika hawa ni wengi lakini mhusika mkuu ni Madalala. Madalala ni mvulana ambaye jina lake halisi lilikuwa Madalala Muungwana lakini wanafunzi wenzake walimwita Madalala bin Mchafu. Yeye ni mvulana wa umri wa miaka kumi na alikuwa mweusi, mfupi na mnene kiasi. Madalala alisomea shule ya msingi ya Mandungulu na alikuwa darasa la nne. Alikuwa na sifa mbaya sana. Kwani alikuwa mjeuri, mkorofsi na mchokozi. Zaidi ya hayo yote alikuwa mchafu sana. Alichukiwa na wanafunzi kwa sifa zake mbaya. Wakati mmoja, Madalala alimchokoza mwanafunzi mwenzake aitwaye Alividza. Mwalimu Shigogodi aliwaona wakipigana akawaita ofisini mwake.

Walipojielezea, Madalala alipatikana na makosa. Yaani yeye ndiye alikuwa mchokozi na pia mwalimu aligundua kuwa akinuka uchafu. Mwalimu alimwambia Madalala aende darasani achukue vitabu vyake aende nyumbani na siku iliyofuata aende shuleni na wazazi wake ili mwalimu azungumze nao kuhusu hali yake ya usafi. Madalala hakuenda nyumbani lakini alienda madukani kucheza “bano”. Mchana alijiunga na watoto wengine wakitoka shuleni na kwenda nyumbani kama kawaida. Alipofika nyumbani, mama yake akifikiria alikuwa ametoka shuleni kama kawaida. Mama yake alimwambia katika ukurasa wa 8 kuwa aende akanawe mikono kwa kuwa alikuwa mchafu. Alimkumbusha atumie sabuni na kisha kubadilisha mavazi yake. Baada ya hayo ale chakula ambacho alikuwa ameandalowi mezani. Chakula chenyewe kilikuwa ni ugali kwa sukuma wiki.

Madalala alinawa ovyo, akala chakula kisha akasema ameenda kufanya kazi ya hisabati waliyopewa shuleni ingawa ulikuwa uongo mtupu. Baadaye Mama Madalala alitayarisha chakula cha jioni. Kisha akamchemshia Madalala maji ya kuoga mwili. Madalala alipofika bafuni, alijimwagilia maji ovyo ovyo mwilini ili aonekane ameoga lakini ng'o, aliogopa maji sana. Baada ya chakula kuiva Madalala alikula kisha akaenda chumbani mwake akiogopa mama yake anawenza kujua kuwa hakuoga, amemdanganya. Akiwa kitandani alisokotwa na tumbo, kichwa kikamuumma kama kwamba kingepasuka. Hakuwa na la kufanya ila kumwita mama yake kwani alidhani angeshikwa na wazimu kama hangetibiwa.

Mama yake alipoingia chumbani alimuuliza mwanawе shida yake. Madalala alimjibu huku machozi yakimtiririka kuwa alikuwa anaumwa na kichwa, tumbo na mwili wote wamwasha. Mama alimshika kichwa, kisha akamwambia afungue mdomo. Madalala alikuwa ananuka kwani mwili wake wote ulikuwa mchafu. Mavazi yake pia yalitoa harufu mbaya. Mama yake alimchukua akampeleka bafuni akamsugua mwili kila sehemu akang'ara. Baadaye wote waling'oa nanga kuelekea hospitali iitwayo Madiagala iliyokuwa karibu na maduka. Zamu yao ilipofika Madalala alimwelezea daktari shida yake. Alitibiwa na kupewa dawa. Mama alituma ujumbe shuleni Madungulu kusema kuwa Madalala hangeweza kufika shuleni kwani alikuwa mgonjwa. Mwalimu Shigogodi Jumamosi jioni alienda nyumbani kwa kina Madalala kumjulia hali. Pia alimwambia mamaye kwamba alitaka kumwona kuhusu kijana wake. Alimweleza kuwa Madalala huchukiwa na wanafunzi wote kwa kuwa mchafu. Mama alimpattia mwalimu chai

akanywa na baadaye akaondoka. Juma lililofuata Madalala alirudi shulen ikiwa msafi. Madalala alijihisi kuwa na furaha sana. Jina Madalala bin Mchafu lisahaulika na akaitwa jina lake halisi Madalala bin Mungwana. Katika hadithi hii, kuna maudhui kama vile afya na usafi wakati Madalala anapolazwa hospitali kutokana na kuuguakwa sababu ya tabia yake ya kutonawa mikono wakati anapokula na kutoosha matunda kwa mfano maembe kabla ya kula. Maudhui mengine ni mabadiliko kwa mfano mabadiliko ya tabia ya Madalala kutoka kuitwa Madalala bin mchafu hadi kuitwa Madalala bin Muungwana baada ya kubadilika na kuepukana uchafu.

3.3 Aina za familia zinazosawiriwa katika *Mwepesi wa Kusahau*, *Nampenda Mama wa Kambo* na *Madalala Abadilika*

Katika mapitio yanayozalisha muhtasari wa hadithi hizi tatu, kumebainika usawiri wa familiaza aina mbalimbali katika vitabu vilivyoteuliwa kwa utafiti huu. Kimuundo, aina za familia zinazojitokeza ni pamoja na familia kiini, familia pana na familia ya ulezi. Kuna mwegemeo mkubwa wa familia za sehemu za nyanjani lakini zilizo na mahusiano ya mjini na mashambani. Karibu kila hadithi ina aina tofauti ya familia kama inavyobainika katika maelezo na mijadala ifuatayo.

3.3.1 Aina ya familia inayosawiriwa katika *Mwepesi wa Kusahau*

Katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau*, familia iliyojitekeza ni familia kiini. Hii ni familia iliyo na wazazi wote wawili na watoto wao. Familia hii inadhihirika vyema katika maneno yafuatayo:

Wazazi wa Juma na Maria walifurahia sana walipobarikiwa na kupata watoto mapacha. Baba yao Hamisi Akida, alikuwa tabibu wa mifugo wilayani Kericho. Mama yao Lilian Mokeira alikuwa muuguzi mkuu katika hospitali ya wilaya hiyo. Wote waliwapenda sana wanao. Walijitahidi kwa mali na hali kuwapa malezi bora na elimu. Waliamini kuwa elimu ndiyo ufunguo wa maisha siku hizi (uk.7).

Maelezo yanayotolewa kuhusu wasifu wa familia hii yanadhihirisha kuwa baba yake Juma na Maria alikuwa Hamisi Akida, na mama yao Lilian Mokeira. Mwandishi anadhihirisha ya kwamba katika familia hii wazazi ni wafanyakazi walioajiriwa na kwa hivyo wana kipato. Ni familia ambayo imepuuza misingi ya ukabila ikizingatiwa kwamba wanandoa hawa wametoka katika jamii tofauti na kuunda familia yao isiyotawaliwa na misingi ya kikabila. Familia hii ni ithibati ya aina mbalimbali za familia za kisasa zinazopatikana nchini Kenya. Ni familia ambayo ina na baba, mama na watoto. Wazazi hawa halisi huwalea wana wao vilivyo kadri ya uwezo

wao wa kihali na kifedha. Ni familia iliyo na mahusiano ya kimji na kishamba ikizingatiwa kwamba mama ni muuguzi katika hospitali ya wilaya na baba ni daktari wa mifugo. Kwa kweli Juma na Maria waliishi na wazazi wao. Wazazi wao waliwapenda wote hata kama walikuwa na tabia tofauti. Katika familia kiini watoto wanaonekana kupendana na kuhurumiana kama Maria anapomhurumia ndugu yake na kumsaidia kurekebisha tabia yake. Juma hata kama alikuwa na matatizo mengi kama vile kusahau mambo kwa wepesi, kuwa mchafu na mzembe aliweza kubadilika na kuiga mfano mwema wa Maria. Juma alianza kuiga mambo yote mazuri ya Maria kama vile kukumbuka mambo na kuwa safi na mwenye bidii.

3.3.2 Aina za familia zinazosawiriwa katika *Nampenda Mama wa Kambo*

Katika hadithi *Nampenda Mama wa Kambo*, familia inayojitokeza mwanzoni ni familia kiini ambapo kuna baba, mama na watoto. Baba anaitwa Peter Weswa lakini mama hajatajwa kwa jina. Mama anayetajwa pasina jina alikuwa na watoto Naliaka na Wekesa. Mama aliaga ndunia wakati alipokuwa akijifungua Wekesa. Kwa sababu ya upweke, baba yake Naliaka alioa bibi mwingine aliyeitwa Anna Achieng. Huyu bibi akawa mama wa kambo wa Naliaka na Wekesa. Kutokana na hali ya kuwepo kwa mama wa kambo, familia kiini ikapanuka na kuwa familia pana ambayo ilihuisha mama wa kambo na watoto wa kambo. Watoto wa kambo walikuwa Wafula na Nasimiyu ambao Anna Achieng aliwapata baadaye na baba yake Naliaka. Katika hadithi hii, mama wa kambo anadhihirika kuwa na sifa njema katika familia ya Peter Weswa. Alichukua majukumu ya mama mzazi wa Naliaka na kuyatekeleza vilivyo. Kwa mfano alimwambia Naliaka hivi: “Nitakuadhibu ukikosa. Nitajaribu kukupenda kadri ya uwezo wangu. Nakusihi usisikie maneno ya watu. Yatakufanya unichukie bure (uk. 10).

Katika hadithi hii mama wa kambo anadhihirika kuwa na sifa njema katika familia ya Peter Weswa. Peter Weswa alikuwa akifanya kazi kama karani katika mji wa Kakamega na mama wa kambo Anna Achieng' naye alikuwa anauzia nyumbani omena na mboga. Mbali na haya hii ni familia katika sehemu za mashambani, ina kipato kidogo, ina uwezo wa kufikia huduma za afya ikizingatiwa kwamba mama aliyekufa alikuwa hospitalini akijifungua. Ni familia inayojali masomo maana watoto wanaelezwa kuwa wanakwenda shulenii.

3.3.3 Aina ya familia inayosawiriwa katika *Madalala Abadilika*

Katika hadithi *Madalala Abadilika*, familia inayojitokeza ni familia kiini. Kuna wazazi wote wawili na mtoto mvulana aliyeitwa Madalala. Mama alionekana akitekeleza wajibu wake kama mzazi. Baba alitajwa tu kwa jina na kuelezewa ya kwamba alienda safari. Kurudi kwake hakukutajwa na pia hakuna wajibu alionekana akitekeleza kuhusiana na familia. Mama alimshughulikia mwanawe katika mahitaji yake yote, kwa mfano chakula, mavazi afya bora na hata elimu. Jambo hili linaleezewa vyema katika ukurasa 8 ambapo mama anapoonekana kujali maslahi ya mtoto kwa kumshauri akanawe kwa sabuni kwa kuwa alikuwa mchafu. Mama vilevile alikuwa amempikia mtoto wake na alimshauri ale baada ya kunawa. Isitoshe, mama alionekana kumjali mwanawe zaidi kiafya wakati Madalala alilia kwa sauti juu ya maumivu. Alipomwuliza shida yake, mwanawe alisema kuwa alikuwa anaumwa na tumbo, kichwa na pia mwili wote ulikuwa unamuumua. Mama aliamua kumtayarisha mwanawe ampeleke hospitalini atibiwe. Ni dhihirisho kamili ya kwamba mama yuajitokeza akijaribu kutimiza majukumu yake kama mzazi. Hapa mama anaonekana kutekeleza majukumu ya ulezi bila ya baba kuonekana akishughulika. Kwa misingi hii inaweza kutolewa hoja kwamba hii ni familia iliyo na wazazi wote wawili japo mmoja hayuko karibu na mwandishi hajatoa maeleo yoyote kama baba huyu licha ya kusafiri anachangia mahitaji ya familia yake. Kutokuwepo kwake hakujahalalishwa kimantiki.

3.4 Usawiri wa familia kama taasisi katika *Mwepesi wa Kusahau, Nampenda Mama waKambo na Madalala Abadilika*

Katika sehemu hii, utafiti huu unachunguza na kuibua mijadala juu ya usawiri wa familia kama taasisi kwa kurejelea vitabu vilivyoteuliwa. Familia kama taasisi inachunguza maisha ya kifamilia na mahusiano ya wanafamilia kama kundi la kijamii. Sehemu hii vilevile inachunguza namna hadithi za kipindi cha 2000–2010 zinavyoangazia familia ambamo watoto wanalelewa. Fauka ya haya, sehemu hii hali kadhalika inachunguza jinsi watoto wanavyoathiriwa kwa njia chanya au hasi na maisha katika familia hizo.

3.4.1 Usawiri wa familia kama taasisi katika *Mwepesi wa Kusahau*

Familia katika *Mwepesi wa Kusahau*imesawiriwa kama familia iliyoipa elimu kipaumbele. Awali wazazi wa familia hii wamesawiriwa kuwa ni watu waliosoma na wanataaluma,

wanafanya kazi ya ajira, wana kipato, wametoka katika jamii tofauti, hawakufungika katika ada ama itikadi za jamii moja, ni wazazi wa kisasa.Uthamini wao wa masomo unaonekana wazi wakati Juma na Maria walipohitimu umri wa kwenda shule. Katika (uk, 8) tunaelezewa kuwa wazazi wao waliwatimizia mahitaji ya shule kwa kuwanunulia sare, vitabu vyatya kusoma, madaftari na kalamu pamoja na mikoba ya kubebia vitabu vyao. Wazazi wao walikuwa kielelezo kizuri kuhusu elimu. Baba yao aliyeitwa Hamisi Akida alikuwa amesoma na kuwa tabibu wa mifugo. Mama yao naye alikuwa amesoma hadi akawa muuguzi mkuu katika hospitali ya wilaya hiyo.

Usawiri mwengine unaojitokeza katika familia ya *Mwepesi wa Kusahau* ni kuwa mvulana anapewa sifa hasi ilhali msichana anasawiriwa kwa njia chanya. Juma anachukuliwa kuwa mtepetevu ilhali Maria anasawiriwa kama mwenye kuwajibika. Kwa mfano, katika ukurasa 9 tunaelezewa kuhusu tabia ya Juma ikilinganishwa na ya Maria kuwa Juma hakutilia masomo maanani ilhali Maria alikuwa akifanya vizuri shulen. Juma pia alikuwa na tabia ya kusahau haraka mambo mbalimbali aliyoambiwa afanye huku Maria akiwa anakumbuka mambo kwa wepesi. Kwa upande mwengine, familia ya *Mwepesi wa Kusahau* inasawiriwa kama iliyo na ushirikiano na mshikamano mzuri baina ya wazazi na watoto na watoto kwa watoto. Mama anaonekana kuwaelewa watoto wake vizuri na kuwasaidia ifaavyo bila kugombana nao. Ushirikiano unajitokeza kwenye familia kati ya watoto na wazazi wao. Watoto walikuwa wakiwasaidia wazazi wao wakati wa likizo katika kazi mbalimbali. Mifano ya kazi walizowasaidia wazazi wao kuzitekeleza zinaelezewa katika (uk, 12-13). Juma na Maria wakiwa nyumbani wakati shule zimefungwa waliwasaidia wazazi katika kazi ya kuwalisha kuku, kuwapa maji ya kunywa pamoja na kukusanya mayai kutoka kwenye viota na kuyatia vikapuni ili yakauzwe.

Familia ya *Mwepesi wa Kusahau* inasawiriwa kwa njia mbalimbali kutegemea sifa za wahusika na nafasi zao katika shughuli za kifamilia, lakini kimsingi inasawiriwa kama familia kielelezo. Katika familia hii kila jambo linalotarajiwa katika familia lipo linapostahili kuwa, majukumu yanayotarajiwa kutekelezwa yanatekelezwa, kipato kinachotakikana kuiendeleza familia kipo, mazingira yanayochangia makuzi mazuri ya watoto yapo, alimradi kila jambo lipo mahali pake. Kimsingi baba alitajwa tu na hakuonekana tena katika familia akitekeleza majukumu muhimu

katika kuendeleza familia. Mama ndiye anayeonekana kushughulikia mahitaji ya watoto na maendeleo ya familia tangu mwanzo hadi mwisho. Mathalani, mama ndiye anayewaanda watoto kabla ya kuenda shulenii (uk. 19), ndiye ambaye watoto wanatafuta ushauri kwake wanapohitaji msaada (uk. 20) na ndiye anayechukua majukumu ya kumsaidia Juma ili aweze kuboresha mienendo yake na kutilia maanani masomo (uk. 30). Pamoja na ukamilifu huu wa kifamilia kuna masuala ibuka katika usawiri wa familia hii. Juma, mtoto wa kiume inasawiriwa kwa njia kinzani kwamba japo ni mwelesi wa kusahau anachangia katika kazi za kifamilia wakati wa likizo. Suala lingine ambalo linaweza kuhusishwa na usawiri wa Juma linaweza kuhusishwa na utelekezwaji wa watoto wa kiume ikingatiwa kwamba hadithi hii imetungwa katika kipindi ambapo masuala ya utetezi wa hali za mtoto msichana yaliwekwa mbele zaidi kuliko ya mtoto mvulana. Suala hili hata hivyo, mtunzi hakulikuza kwa ukamilifu. Suala ambalo mtunzi ameelekea kukuza kwa ukamilifu ni usawiri chanya wa mtoto wa kike kama mtoto safi, mwenye kuwajibika, mwenyewe bidii na mfano mwema kwa jumla wa kuigwa na watoto wengine.

3.4.2 Usawiri wa familia kama taasisi katika *Nampenda Mama wa Kambo*

Katika hadithi ya *Nampenda Mama wa Kambo*, familia yenye ilijitokeza kuwa na bidii kati ya wazazi ili waweze kukimu mahitaji ya wana wao. Kazi walizozifanya zinaelezewa vyema katika (uk. 1) ambapo tunaelezwa kuwa wazazi walikuwa na bidii. Baba alikuwa karani katika mji wa Kakamega. Mama naye alikuwa akiuza vyakula kama njugu karanga, omena na mboga. Familia pia inasawiriwa kuwa yenye upendo na amani ambapo baada ya kifo cha mamaye Naliaka na kumuacha mtoto mchanga wa kiume aliyeitwa Wekesa. Shangazi yake Naliaka alisaidiana na baba yake Naliaka kumlea Wekesa. Jambo hili linadhihirika vyema katika (uk. 5–6) tunapoelezewa kuwa shangazi na baba walisaidiana kumtunza na kumlea Wekesa. Vilevile, upendo na amani unadhihirika kati ya Naliaka na mamake wa kambo. Mama wa kambo Anna Achieng alimpenda Naliaka na kumtunza sawa na wanawe hadi Naliaka akakiri maneno katika (uk. 11) anapoeleza kwamba alianza kumsahau mama yake na kumpenda mama wa kambo. Marafiki hawakuamini alipowaambia mama Wafula alikuwa tofauti kabisa na mama wengine wa kambo. Akikosa hamwambii babake mara moja humrekebisha na hata humuaadhibu mwenyewe. Familia hii inasawiriwa kuwa na ushirikiano na kutekeleza majukumu ya nyumbani baina ya watoto na wazazi. Kwa mfano, Naliaka anaelezea mifano ya kazi ambazo hufanya nyumbani

kumsaidia mama wa kambo. Akitoka shulen ikuwa anateka maji mtoni halafu anakusanya kuni na hata kutayarisha chakula cha jioni. Mwishoni mwa wiki alimsaidia mama wa kambo zaidi kufanya kazi za nyumbani.

Kimsingi hii ni familia katika mazingira ya nyanjani na iliyo katika tabaka la chini linalojikimu kwa kazi na kipato kidogo. Licha ya hayo hii ni familia inayojitahidi kujiendeleza ndio maana elimu ilipewa kipaumbele katika familia hii. Kila mtoto aliyelekwa shule kusoma. Katika ukurasa wa 11 watoto katika familia wanaonekana wakifanya kazi ya ziada ya shule nyumbani wakisaidiwa na mama wa kambo. Katika familia hii dini imetiliwa mkazo na katika (uk. 11) Naliaka anasema kuwa siku ya Jumapili mama wa kambo alikuwa anawafunza biblia na kuwashauri wawe watoto wa Mungu na watiifu. Hata kama Naliaka alielezwa mengi na wanafunzi shulen ikuhusu walivyoteswa na mama zao wa kambo, Naliaka hakuyapitia hayo mateso. Wakati mmoja Naliaka alimwambia mama wa kambo vile wanafunzi shulen walikuwa wanasema kuhusu dhuluma walizopata kwa mama zao wa kambo. Naliaka alimwambia kuwa yeche ni tofauti na mama wa kambo wengine. Naye Anna Achieng alimjibu Naliaka katika (uk. 12) kuwa ingawa yeche na Wekesa hawakuwa damu yake aliwapenda kama alivywapenda Wafula na Nasimiyu.

3.4.3 Usawiri wa familia kama taasisi katika *Madalala Abadilika*

Katika familia ya hadithi ya *Madalala Abadilika*, mtoto Madalala anajitokeza kuwa na tabia mbaya. Jambo hili la dhihirika vyema katika (uk. 1) tunapoelezwa kuwa Madalala alikuwa na ujeuri, ukorofi na uchokozi. Aidha, alikuwa hazingatii usafi. Tabia zake mbaya zilifanya asipendwe na wanafunzi wenzake. Katika familia hii mama anasawiriwa kama mwenye kutekeleza majukumu yote nyumbani kwa kuwa baba hayuko. Baba yake Madalala alitajwa tu mwanzoni kwamba alikuwa ameenda safari. Hakuweza kutajwa tena wala kuonekana akitekeleza majukumu yoyote. Kwa hivyo, hadithi inasawiri familia ya kisasa kama ambayo inaendeshwa na mama aliyeachiwa kila jukumu. Familia hii inaonekana kuwa na ushirikiano hasa baina ya mama na mwanaye. Inaonekana kujali maslahi ya jirani wakati mama yake Madalala anapoenda kumjulia hali jirani yake mgonjwa aliyeitwa mama Ateka (uk. 9). Nidhamu pia inajitokeza katika familia ya Madalala. Hata baada ya Madalala kuugua na kutibiwa, mama

yake alichukua hatua kutuma ujumbe shuleni Madungulu kusema kuwa Madalala ni mgonjwa. Jumamosi jioni mwalimu Shigogodi alienda kwa kina Madalala kumjulia hali katika (uk. 7).

Elimu ilipewa kipaumbele kwenye familia. Madalala alipohitimu umri wa kwenda shuleni, alipelekwa na wazazi wake ukurasa wa 1, tunapoelezewa kuwa Madalala alisoma katika shule ya msingi ya Madungulu, katika darasa la nne. Hata hivyo hajaelezwa wazazi wa Madalala walisoma kufika kiwango kipi kwa sababu baba ametajwa tu kuwa alienda safari bila kufafanuliwa ni safari ya shughuli gani na mama alifanya tu shughuli za nyumbani, walimhimiza mtoto wao asome kama watoto wengine katika jamii. Hii inaonyesha walitilia maanani elimu ya watoto wao hata kama wao wenyewe hawakusoma sana.

3.5 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika *Mwepesi wa Kusahau*, Nampenda Mama wa Kambo na Madalala Abadilika

Katika sehemu hii, utafiti huu unachunguza uhalisia wa kifamilia katika vitabu teule vilivyoshirikishwa katika utafiti huu. Uchunguzi huu ulifanywa kwa uzingatifu wa mihimili ya nadharia ya uhalisia wa kijamii. Katika utafiti huu uhalisia wa kifamilia ulijitokeza kuwa suala tata na familia katika vitabu vilivyoteuliwa zinaakisika kwa njia mbalimbali kama zilivyo za aina mbalimbali na zilizo changamano. Hadithi hizi zimejengwa katika misingi ya familia kielelezo na uhalisia tofauti umeweza kuonekana.

3.5.1 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika *Mwepesi wa Kusahau*

Kulingana na nadharia ya uhalisia, familia inayoakisika katika *Mwepesi wa Kusahau* ina uhusiano mkubwa na hali halisi ya maisha katika jamii hasa nchini Kenya ambapo hadithi hii imeandikiwa. Kikatiba nchini Kenya kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Familia nyingi nchini huthamini elimu ya watoto wao kama ilivyo jamii katika *Mwepesi wa Kusahau* ambayo iliipa elimu kipaumbele. Kihalisia pia jamii halisi ya mwandishi ina sera nyingi zinazompendelea mtoto wa kike. Mifano ya sera zinazowapendelea watoto wa kike ni sera iliyotumiwa na Wizara ya Elimu Kenya kuwachukua wasichana vyuoni wakiwa na alamaza chini kuliko alama za wavulana katika mtihani wa kitaifa. Vilevile katika siasa huwa kuna wawakilishi wa wanawake lakini hakuna wawakilishi wa wanaume. Kadhalika sera ya thuluthi mbili katika maongozi ya serikali kimsingi inalenga kuhakikisha wanawake hawabaki nyuma. Aidha, kumekuwa na maoni

kupitia vyombo vya habari kuwa mtoto wa kiume amesahaulika na kutelekezwa (Miricho, 2015). Uhaliisa huu unaodhahirika katika familia ya *Mwepesi wa Kusahau* ambapo mvulana anapewa sifa hasi ilhali msichana anasawiriwa kwa njia chanya. Juma anachukuliwa kuwa mtepetevu ilhali Maria anasawiriwa kama mwenye kuwajibika. Hili linadhirikira katika (uk. 9). Kihalisa vilevile ripoti za vyombo vya habari kama vile magazeti ya *Daily Nation* katika makala yanayozungumzia siku ya kina baba ulimwenguni June mwaka wa 2018 na 2019 yaliaandika makala kuhusu suala la familia nyingi kukosa kuwepo kwa baba mzazi. Kwenye makala yenye kichwa ‘Missing in action; Why Kenya is in the grip of a fatherhood crisis’ *Daily Nation* June 18, 2019, inaelezea kukosekana kwa baba katika familia kutokana na sababu kama vile baba kupuuza majukumu yake, kutengana na mama, shughuli za kikazi na kifo. Katika familia ya *Mwepesi wa Kusahau* baba alitajwa tu na hakuonekana tena katika familia akitekeleza majukumu muhimu katika kuendeleza familia. Mama ndiye anayeonekana kushughulikia mahitaji ya watoto na maendeleo ya familia tangu mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano, katika (uk. 19) mama ndiye anayewaanda watoto kabla ya kwenda shulen, katika (uk. 20) ndiye ambaye watoto wanatafuta ushauri kwake wanapohitaji msaada na katika (uk 30) ndiye anayechukua jukumu la kumsaidia Juma ili aweze kuboresha mienendo yake na kutilia masomo maanani.

3.5.2 Uhaliwa kifamilia unavyoakisia katika *Nampenda Mama wa Kambo*

Kihalisa katika jamii ya kisasa, elimu imepewa kipaumbele kama ilivyo katika familia ya hadithi ya *Nampenda Mama wa Kambo*. Watoto hupelekwa shule kusoma na ni kawaida watoto kuketi nyumbani jioni wakifanya kazi ya ziada ya shule wakisaidiwa na wazazi wao kama ilivyo katika hadithi hii. Kihalisa vilevile, katika jamii ya kisasa dini imetiliwa maanani na jamii nyingi jambo ambalo linadhirikira katika *Nampenda Mama wa Kambo*. Ni kawaida kuwaona watu katika jamii halisi wakihudhuria ibada katika mahali pao pa kusali siku maalum wanazositambua. Kihalisa, katika baadhi ya jamii nchini Kenya hasa kutoka magharibi mwa nchi ambako ni kawaida mwanamume kuoa bibi mwingine pengine wa kwanza akifa na inakubalika. Mama wa kambo wengi huwa wema kwa kuwa jamii inawakubali nao wanakubali watoto wa wake wenzao kama watoto wao (maoni ya mtafiti). Aidha, kutokana na majina ya wahusika Anna Achieng na Peter Weswa walioana wakiwa makabila tofauti. Jambo hili laweza kuhusishwa na ndoa kati ya makabila nchini Kenya. na ambao ni uhaliwa unaokubalika.

3.5.3 Uhaliwa kifamilia unavyoakisika katika *Madalala Abadilika*

Katika jamii halisi hasa jamii ya mwandishi ambayo ni jamii ya Kenya, elimu imetiliwa mkazo kisera ambapo kuna sera ya elimu bila malipo na kuwa elimu ya msingi ni ya lazima mionganii mwa sera nyingine za elimu. Uhaliwa huu unajitokeza katika hadithi hii wakati elimu inapopewa kipaumbele kwenye familia. Madalala alipohitimu umri wa kwenda shulenii, alipelekwa na wazazi wake (uk. 1). Kwa mujibu wa nadharia ya uhaliwa, familia ya Madalala ni kiwakilishi cha baadhi ya familia halisi katika jamii kwa kuwa sawa na ilivyokuwa katika hadithi ya *Madalala Abadilika*. Watu katika jamii halisi mara kwa mara hushauriwa kujali maslahi ya wenzao. Jambo hili linadhahirika katika hadithi hii wakati mama yake Madalala anaposema kuwa anaenda kumjulia hali mama Ateka kutokana na habari aliyopata kuwa alikuwa mgonjwa (uk 9).

3.6 Hitimisho

Sura hii imetua muhtasari wa hadithi za utafiti huu za kipindi cha mwaka 2000–2010 ambazo ni *Mwepesi wa Kusahau* (2005), *Nampenda Mama wa Kambo* (2006) na *Madalala Abadilika* (2009) na kisha kujadili aina za familia zinazosawiriwa katika *Mwepesi wa Kusahau*, *Nampenda Mama wa Kambo* na *Madalala Abadilika*. Aina za familia zilizojitokeza ni familia kiini. Imebainika kuwa familia nyingine huanza kama familia kiini hasa zaweza kuchukua mikondo mingine na kuwa familia pana hasa kutokana na mambo kama vile kifo cha mzazi mmoja ambapo mzazi anayebaki huoa au huolewa na mtu mwingine na mtoto kulelewa na mzazi asiye wake wa kumzaa kama vile katika *Nampenda Mama wa Kambo*, *Cheupe na Cheusi na Ahaa! Roda*. Katika hadithi zilizochunguzwa familia nyingi zinaiishi mashambani na ambapo inakuwa ni rahisi kutangamana na familia pana. Kwa mkabala wa watoto wasomaji, na kutokana na ukweli kuwa hadithi hizi zinaangazia zaidi mandhari ya sehemu za mashambani, watoto wa sehemu za mashambani wataweza kujitambulisha na hadithi hizi zaidi ya wenzao wa sehemu za mijini. Hii ni kwa kuwa wanajihusisha na shughuli nyingi zinazofanywa na watoto wahusika katika hadithi kama vile kutunza kuku na kukusanya mayai (katika *Mwepesi wa Kusahau*); kufulia nguo mtoni na kuchuma matunda msituni (katika *Cheusi na Cheupe*). Vilevile, imejadili usawiri wa familia kama taasisi katika *Mwepesi wa Kusahau*, *Nampenda Mama wa Kambo* na *Madalala Abadilika* na kubainika kuwa wanafamilia kama kundi la kijamii wanaishi kwa utangamano hasa katika familia kiini. Katika familia pana wakati mwingine migogoro hutokea lakini imebainika kuwa maridhiano mwishowe hupatikana katika familia. Familia nyingi za

kisasa zilione kana kutilia maanani masomo ya watoto wao. Baadhi ya familia zinaoa watu hata kutoka makabila tofauti na wanaishi maisha ya utulivu. Wengi wao wanapata watoto wachache kama mmoja au wawili. Palipo na kifo wanaoathirika sana ni akina mama. Mwishowe kutamatisha kwa kuangazia jinsi uhalisi wa kifamilia unavyoakisisi katika *Mwepesi wa Kusahau, Nampenda Mama wa Kambo na Madalala Abadilika*. Imebainika kuwa familia zinazoakisiwa katika hadithi zilizoteuliwa ni kiwakilishi halisi cha familia za kipindi cha kiwakati kinachowakilishwa na vitabu vilivyoteuliwa. Vilevile, kwa mkabala wa watoto wasomaji, imebainika kuwa kutokana na ukweli kuwa hadithi hizi zinaangazia zaidi mandhari ya sehemu za mashambani, watoto wa sehemu hizo wanaweza kujitambulisha na hadithi hizi zaidi ya wenzao wa sehemu za mijini.

SURA YA NNE

USAWIRI WA FAMILIA YA KISASA KATIKA *CHEUPE NA CHEUSI, LIKIZO YA MKOSI NA AHAA! RODA*

4.1 Utangulizi

Sura hii imetua muhtasari wa hadithi za utafiti huu za kipindi cha mwaka 2011–2018 ambazo ni *Cheupe na Cheusi* (2013), *Likizo ya Mkosi* (2014) na *Ahaa! Roda* (2017) na kisha kujadili aina za familia zinazosawiriwa katika *Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda*. Imejadili usawiri wa familia kama taasisi katika *Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda* na hatimaye kuchunguza uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika *Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda*.

4.2 Muhtasari wa vitabu vya hadithi vilivyoteuliwa vya kipindi 2011 - 2018

Katika sehemu hii muhtasari wa hadithi za vitabu vilivyoteuliwa umetolewa kwa nia ya kuangazia kwa muhtasari maudhui ya hadithi na sifa za wahusika ili kuweka msingi wa kuchunguza aina za familia zinazosawiriwa. Vilevile muhtasari huu wa hadithi unaangazia jinsi uhalisi wa kifamilia katika hadithi teule za kipindi hiki unavyojitokeza.

4.2.1 Muhtasari wa *Cheupe na Cheusi*

Wahusika wakuu katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi* ni watoto waitwao Cheupe na Cheusi ambao walikuwa ni dada wa kambo. Katika hadithi hii pana mhusika anayeitwa Maliki na mkewe Nikisha. Waliishi kwa muda mrefu bila kupata mtoto kisha baadaye wakabarikiwa mtoto wa kike aliyekuwa mweupe sana hadi akapewa jina Cheupe. Cheupe alikua vizuri akiwa msichana mwenye bidii aliyependwa na kila mtu. Baadaye mamaye Cheupe aliaga dunia na kumwacha Cheupe na baba yake. Upweke ulipowazidua, Maliki aliamua kuo a bibi mwingine. Huyo bibi aliitwa Bititi. Maliki na Bititi walibarikiwa mtoto wa kike aliyekuwa mweusi tititi hadi wakampa jina Cheusi. Bititi alijaribu kumwosha kwa maziwa mwilini na kumnywesha maziwa kwa wingi akifikiri ya kwamba atakuwa mweupe lakini aliambulia patupu. Hakujua ya kwamba uzuri na urembo wa mtu si ngozi ila tabia. Alimchukia Cheupe akapanga njama ya kumtuma msituni usiku ili aweze kuliwa na wanyama wakali. Jambo hili linadhahirika wazi katika ukurasa 4 ambapo usiku mmoja Maliki alipokuwa ameondoka kwenda safari ya mbali,

Bititi alimwamsha Cheupe usiku wa manane uliokuwa na mvua nyingi na kumwamrisha atoke gizani aende shambani usiku kuchuma maembe. Nia yake ilikuwa aliwe na wanyama wakali wa mwitu. Cheupe alitembea msituni akitetemeka kwa baridi na hofu nyingi. Cheupe alitembea kwa muda mrefu kisha akaona nyumba na kuamua kwenda kujikinga mvua. Alipobisha mlango, sauti kutoka ndani ilisema “karibu ndani”. Cheupe alipoingia ndani aliwapata mbilikimo watatu. Walimhurumia sana kwa kunyeshewa. Walimkaribisha jikoni apike chakula ale na awapakulie. Cheupe alifanya alivyoagizwa. Baada ya kula aliambiwa kuosha vyombo na kusafisha sakafu. Alifanya mambo hayo yote bila wasiwasi. Mbilikimo walifurahishwa sana na vitendo nya Cheupe. Walimwuliza Cheupe alikuwa anaenda wapi usiku kuitia kwenye msitu wenye wanyama wakali. Aliwajibu alikuwa ametumwa na mama yake mlezi kwenda kumtundia maembe. Hao mbilikimo walimpa maembe mengi sana katika gunia, kisha wakamwongeza zawadi nyingine. Kwanza atakuwa akitoa dhahabu kutoka mdomoni mwake kila wakati akiongea, pili urembo wake utazidi kila siku na tatu ataolewa na mfalme. Cheupe aliwashukuru na kuondoka kwenda nyumbani.

Cheupe alipofika nyumbani, Cheusi na Bititi walishuka kumwona kwa vile walikuwa wanafikiria aliliwa na wanyama msituni. Pia walishuka kumwona akitoa dhahabu mdomoni. Cheupe aliwahadithia kila kitu kilichotendeka msituni. Bititi alitamani mwanawe Cheusi pia atoe dhahabu mdomoni kila wakati alipoongea. Alimtuma Cheusi aende msituni usiku hadi atakapoiona nyumba ya mbilikimo. Alimwambia akifika aanze kupika mara moja. Cheusi alipoiona nyumba ile aliingia bila kubisha mlango akaenda jikoni mara hiyo na kuanza kupika bila kuongea na mbilikimo. Chakula kilipoiva alijipakulia na kula peke yake. Mbilikimo walishangazwa na jambo hili. Alipomaliza kula wale mbilikimo walimwambia aoshe vyombo na afagie nyumba akakataa. Akawaambia wampe maembe yake na baraka zake na kama hawampi wamwambie aende nyumbani. Wale mbilikimo walikasirika sana na Cheusi hadi wakaanza kumsema kwamba anaujeuri mwingi sana. Wote wakasema ya kwamba watamfanya atapike vyura kila wakati anapozungumza. Cheusi alipofika nyumbani Bititi alikasirika sana kumwona mikono mitupu na kila wakati alipozungumza alitoa vyura. Jambo hili lilimfanya Bititi kumchukia Cheupe zaidi na zaidi ya hayo kumfanya kijakazi wao.

Siku moja, Bititi alimtuma Cheupe kufua nguo mtoni ambapo huwa na ngwena wengi. Sababu ya kumtuma ilikuwa aliwe na ngwena hao. Cheupe alipokuwa akifua nguo, mfalme alipita karibu na mto. Alimuona msichana mrembo akatamani kumwoa awe mke wake. Baada ya siku chache alimchukuwa msichana yule yaani Cheupe na kumwoa kwa harusi kubwa sana. Hatimaye Cheupe akawa malkia na baadaye wakabarikiwa na mtoto mmoja mvulana. Baadaye Bititi na Cheusi walienda kumtembelea Cheupe kwenye Kasri lake. Waliposalimiana, mfalme aliondoka na kuwaacha wakizungumza. Bititi na Cheusi walichukua nafasi hii kumrusha Cheupe nje dirishani na akazama katika mto uliopitia nyuma ya kasri lao. Kisha Cheusi alilala kwenye kitanda cha Cheupe na kujifanya Cheupe. Mfalme aliporudi jioni Bititi alimwambia Cheupe alienda kulala kwa kuwa alishikwa na homa. Jambo la kushangaza ni ambavyo mfalme alivyomwona mkewe akitoa vyura anapozungumza. Bititi alimkuliza roho kwamba homa ikiisha ataacha kutoa vyura aanze kutoa dhahabu. Usiku huo mpishi wa mfalme alimwona bata mtoni. Bata akamsalimu kisha akamwuliza kama akina Bititi na Cheusi walienda akamjibu wamelala. Akamwuliza mtoto wake yuko wapi, akamwambia pia yeye amelala. Ndipo basi bata aligeuka kuwa Cheupe akakimbia chumbani akamnyonyesha kisha akageuka kuwa bata tena. Alimwambia mpishi aende amwambie mfalme amzungushie upanga mara tatu juu yake naye atapona na kuwa kawaida tena.

Mpishi alimfikishia mfalme ujumbe huo na mfalme akafanya alivyoagizwa na Cheupe akarudia hali yake ya kawaida. Asubuhi yake mfalme alimwuliza Bititi hukumu ya mtu aliyemtupa mwenzake kutoka ghorofani ni nini? Naye akamjibu ni kufungiwa kwenye pipa na kutupwa mtoni bila huruma. Mfalme akamjibu hivyo ndivyo watafanywa yeye na Cheusi, kwa kutaka kumuua Cheupe. Bititi alipiga magoti na kuomba msamaha kwa mfalme na Cheupe. Kwa kweli Cheupe aliwasamehe na kuwakumbusha kuwa ni vyema kuishi kama familia moja bila kuchukiana. Tangu wakati huo mfalme na Cheupe waliishi raha mustarehe. Hadithi hii inaibua maudhui mengi yasiyojenga maadili hasa kutokana na vitendo vya mama wa kambo wa Cheupe. Maudhui hayo ni kama vile chuki, wivu, unyanyasaji, ukatili na ubaguzi wa watoto. Hata hivyo mtoto msomaji anajifunza maadili kutokana na ukweli kwamba kuna adhabu inayotokana na unyama ambao Cheupe alitendewa na mama yake wa kambo na ambapo nia mbaya ya mama wa kambo haikufanikiwa kamwe. Mwishowe Cheupe alimsamehe mama wa kambo na hapo panaibuka maudhui ya usamehevua na maridhiano.

4.2.2 Muhtasari wa *Likizo ya Mkosi*

Likizo ya Mkosi ni hadithi ambayo wahusika wake wakuu ni wawili. Nao ni Otambo na Kerubo. Otambo ni mvulana na Kerubo ni msichana. Hawa watoto wawili ni ndugu wa toka nitoke. Walitaka sana kwenda kuwasalimia babu na nyanya yao mashambani shule zikifungwa muhula wa tatu. Baba yao Dkt. Stephen Ogato ambaye alikuwa mtafiti katika kampuni ya majani chai ya Bubondi wilaya ya Chorike kila wakati alikuwa akiwaahidi kuwa angewapeleka mashambani wangeibuka wa kwanza katika mitihani ya mwisho wa muhula. Kerubo na Otambo walisomea shule ya msingi ya Majimazuri. Otambo alisoma darasa la tano Kerubo darasa la sita. Watoto hawa walitia bidii sana ili ndoto yao ya kwenda mashambani itimike. Muhula huo waliibuka washindi katika madarasa yao na wakatuzwa zawadi. Otambo alituzwa zawadi ya kitabu cha picha za wanyama pori naye Kerubo kitabu cha hadithi fupi. Baada ya sherehe za kufungwa shule kumalizika Otambo na dada yake waliandamana kwenda nyumbani. Walipofika nyumbani, walimpata mama yao akitayarisha chakula cha mchana. Walimwelezea vile walivyokuwa wamefanya vizuri katika masomo yao huku wakitoa ripoti zao. Mama yao aliwapa hongera kwa kazi yao nzuri. Aliwaambia baba yao atafurahia sana kwa kufuzu kwao. Zaidi ya hayo walimwonyesha zawadi walizotuzwa kwa kazi yao nzuri shulenii.

Kerubo na Otambo walienda chumbani mwao wakabadilisha sare zao na kuvaan nguo za nyumbani. Chakula kilipoiva, mama yao aliwaambia kwamba ye ye atabaki akichunga nyumba naye baba yao atawapeleka mashambani kisha arudi mjini kwa vile alikuwa na safari ya kwenda Tanzania kuhudhuria mkutano muhimu wa tawi la kampuni aliyoifanyia kazi. Waliabiri gari aina ya Toyota Landcruiser na kung'oa nanga. Wakiwa njiani Otambo na Kerubo walikumbuka hawakumnunulia babu zawadi. Baba yao aliwaahidi ya kwamba wakifika mahali ambapo panaitwa Keumbu, atanunulzia zawadi ya babu. Baada ya muda wa nusu saa hivi, walifika katika kijiji cha Mesesi. Humo ndimo kijiji cha babu na nyanya. Walipofika nyumbani kwa nyanya na babu walikaribishwa kwa furaha, vifijo na taadhima kubwa. Walichinjiwa kuku na wakati wa kula Dkt. Ogato aliwaeleza kuhusu safari ya Tanzania aliyokusudia kufanya (uk 22 - 23). Baada ya kula, Dkt. Ogato aliamua kuondoka. Ilikuwa saa kumi jioni Babu, nyanya, Kerubo na Otambo walimpungia mkono.

Baadaye nyanya aliwatayarishia chakula cha jioni. Baada ya kula, Kerubo alimsihi nyanya awatambie hadithi. Nyanya aliwatambia kuhusu wanyama. Baadaye nyanya aliwaonyesha Otambo na Kerubo chumba cha kulala. Likizo ya Otambo na Kerubo huko mashambani ilikuwa na shughuli nyingi kila siku. Waliwasaidia nyanya na babu katika shughuli za ukulima na ufugaji hodari.

Baada ya wiki tatu kwisha, Otambo na Kerubo walikuwa bado mashambani. Naye baba yao alikuwa amemaliza shughuli za Tanzania na kuanza kujitayarisha kurejea nyumbani. Siku hiyo Bi. Ogato alikuwa ameenda sokoni kununua bidhaa za kumpikia Dkt. Ogato. Alipoanza safari ya kurudi nyumbani simu yake ya mkono ilikiriza kutoka kibetini na kabla hajaipokea ikazima. Baada ya muda mfupi, ilikirizwa tena. Wakati huu Bi. Ogato alichukua na kusema hallo, aliambiwa na mtu ambaye hakumjua aende katika hospitali ya Kenyatta haraka sana. Bila kupoteza muda alijitayarisha na kung'oa nanga. Alipofika hospitalini, alipiga ile namba aliyokuwa amepigowi. Dkt. Wesonga aliipokea na kumwelekeza katika chumba alimokuwa. Alipomkuta Dkt. Wesonga alihojiwa kuhusu safari ya bwanake ya Arusha-Tanzania. Kisha wakaandamana katika chumba ambapo mwili ulikuwa umewekwa. Bi. Ogato kufungua kitambaa kilichokuwa kimeufunika mwili, alipiga nduru kwani mumewe hana ndevu nyingi kama za kalasinga. Dkt. Wesonga alimshauri watoke katika chumba hicho ili upelelezi zaidi ufanywe. Pasipoti ya mume wake, kitambulisho chake, simu na hati zake nyingine muhimu zilipatikana kwenye koti la huyo mtu aliyesemekana sio Dkt. Ogato. Siku ya Jumapili asubuhi Otambo na Kerubo walikwenda sokoni Tabaka kumpeleka nyanya yao akauze mayai. Babu yao alikuwa amemtuma nyanya amnunulie gazeti la *Mwananchi* akitoka sokoni. Walipomaliza kuuza mayai, walimnunulia babu gazeti na kuanza kurudi nyumbani. Otambo hupenda kusoma gazeti. Kwa hivyo alipitia kidogo akitembea. Maajabu aliona picha ya baba yake kwenye gazeti. Aliwaonyesha Kerubo na nyanya yake. Habari ilikuwa kuwa baba yao alipata ajali barabarani akitoka Arusha-Nairobi na alikuwa amelazwa hospitali Nairobi.

Walipofika nyumbani walimwonyesha babu habari gazetini. Nyanya alikata shauri ni bora wote waende Nairobi wamjulie hali mwana wao. Alfajiri ya siku ya Jumanne iliwapata babu, nyanya na wajukuze jijini Nairobi. Mafungulia ng'ombe ilipofika iliwapata wamefika katika hospitali ya Nairobi, walimpata mama yao katika wodi, Dkt. Ogato alipokuwa amelazwa. Wote walifurahi

sana kumwona akiwa salama salimini. Jamaa wale walitaka Dkt. Ogato awatatalie kitendawili kile. Yeye alisema aliquwa ameketi na mtu mwenye masharubu kama ya kalasinga. Mara akasinzia akiwa ameshika mkoba wake. Mtu huyo akamwibia mali yake yote. Nyanya na babu waligundua mtu yule alimwekea mwana wao dawa za kulevyia kisha akaibiwa. Kerubo alinyamaza kisha akasema kwamba hiyo ilikuwa likizo ya mkosi ingawa walimshukuru Mungu kwa kumlinda baba yao. Siku chache baadaye Dkt. Ogato alipata nafuu na kuruhusiwa kuondoka hospitalini. Kimaudhui, *Likizo ya Mkosi* ni hadithi iliyo na maudhui mengi ya kimaadili. Maudhui hayo ni kama vile ushirikiano, upendo na uwajibikaji. Maudhui mengine ni elimu ya watoto na uchumi hasa kuhusiana na shughuli za baba yake Kerubo, Dkt. Ogato, kuhusu majani chai.

4.2.3 Muhtasari wa *Ahaa! Roda*

Ahaa! Roda ni hadithi ambayo inasimulia kuhusu msichana mdogo kwa jina Roda ambaye ana ndoto ya kufanikiwa maishani na kuwa jaji lakini anakabiliwa na matatizo mengi katika safari yake ya kutimiza ndoto yake. Roda na mamaye bibi Fatu waliishi katika kijiji cha Tupe. Baba yake Roda alifariki kitambo kutokana na maradhi ya saratani. Alikuwa anaitwa Bwana Gidamu. Bibi Fatu alikuwa mama mwenye mkono wazi, utajiri mwingi na ukarimu. Roda naye alikuwa wembe masomoni. Alikuwa akitaka kuwa jaji katika siku za usoni. Rafiki yake wa karibu alitaka kuwa mhandisi. Bibi Fatu alikuwa rafiki wa familia ya rafikiye Roda. Baba yake Roda alikuwa na ndugu wawili ambao ni Sumu na Kilemba. Sumu alikuwa mlevi kupindukia na hakuwahi kuoa maishani. Alikuwa mmoja wa wanakijiji waliokuwa wanamuonea wivu Bibi Fatu kutokana na maendeleo yake. Kilemba alikuwa ameoaa. Alikuwa mionganii mwa wanakijiji waliomlinda na kumtetea Bibi Fatu alipojaribu kudhulumiwa.

Bibi Fatu alitoweka kwa muda wa siku mbili akiwa na mwanawe Roda. Siku ya tatu Bwana Mkongojo, bibi Fatu na bwana Kilemba walienda nyumbani kwa rafikiye Roda kuwaona wazazi wake. Mwana Mkongojo aliwaeleza ambavyo bibi Fatu na Roda walitekwa nyara na baada ya pilkapilka za kuwatafuta, wakampata bibi Fatu lakini wakamkosa Roda. Aliendelea kusema ya kwamba walitaka usaidizi wa kumtafuta Roda. Baada ya muda wa siku moja hivi, kelele za wanakijiji zilisikika wakisema Roda amepatikana kwenye shimo. Alikuwa ameishiwa na nguvu bila kujijua wala kujitambua. Mamaye rafiki yake Roda ndiye aliyekimbia dukani akamletea

Roda pakiti tatu za maziwa na akamnywesha pakiti moja polepole. Kisha walimbeba na kumpeleka nyumbani ambapo bwana Kilemba alimwita daktari akaja kumpa huduma ya kwanza. Roda alipatiwa vidonge kadhaa nya kumeza. Muda si muda alianza kurejewa na fahamu. Hapo ndipo alianza kuelezea namna walitekwa nyara. Alimtaja ami yake Sumu kuwa mmoja kati ya wale waliotaka kumficha. Bwana Sumu alitoroka katika kijiji cha Mabatini kwa muda mrefu sana akiogopa kunaswa na mkono wa sheria. Roda pia alirudi shulen na kuendelea na masomo yake kama kawaida. Alipofika darasa la nane, alifanya mtihani pamoja na rafiki yake wa dhati. Roda ndiye aliongoza huku rafiki yake akimfuata unyounyo. Wote walijiunga na shule moja ya upili iitwayo Mkazo ambayo si ya bweni.

Siku moja kulisikika kamsa ambayo haingemruhusu ye yeyote kuketi na kusubiri. Wanakijiji walikimbia kueleke ambako kamsa ilitokea ambako ilikuwa nyumbani mwa bibi Fatu. Bibi Fatu alikuwa amelala chini akiwa amekufa. Aliyemuua alitumia shoka kumchinja. Roda alibaki yatima akiwa na umri mdogo. Mwili wa bibi Fatu ulipelekwa katika mochari kuhifadhiwa huku uchunguzi ukifanywa. Baadaye sajenti Kizito na askari wake walirudi kijijini kuwapa ripoti kuwa bwana Sumu na wenzake watatu ndio walihusika na kifo cha Bibi Fatu na washatiwa mbaroni kwa uhalifu walioutenda. Bwana Kilemba aliwaahidi wanakijiji kuwa baada ya mazishi atamchukua Roda na kuishi naye na pia alisema atamshughulikia sawa na watoto wake. Wakati wa mazishi ulipofika, bibi Fatu alichukuliwa kutoka ufuoni na kusafirishwa hadi kwake nyumbani ili aweze kuzikwa. Roda alipoona jeneza lile alilia sana na kuanza kujzungumzia. Maswali aliyojiuliza yanadhihirisha ambavyo Roda aliona maisha yakiwa magumu baada ya kuwa yatima. Alilia akiuliza ameachwa mikononi mwa nani, angeishi vipi na kwa nini alikufa mapema vile (uk 61).

Baada ya mazishi, bwana Kilemba alione kana akimshika Roda mkono na kutembea naye kama alivyokuwa amewaaahidi wanakijiji. Bibi Mnuna alimfanya Roda kijakazi wao. Yeye na wanawe kazi yao ilikuwa kupumzika tu. Ahadi ya bwana Kilemba kwenye mazishi ilivunjwa bila hisia. Siku moja baba yake rafikiye Roda alimfumania bibi Mnuna akimchapa Roda kinyama. Alimjulisha mkewe ambaye alishtuka sana na kumwambia amjulische bwana Kilemba jambo hilo. Bwana Kilemba alikuwa amehamishwa kazi na kupelekwa mjini Mwang'ombe. Alipopata habari, siku iliyo fuata alisafiri mashambani. Kabla ya kufika kwake alipitia kwa wazazi wa

rafikiye Roda. Alimchukua baba yake rafikiye Roda wakaenda nyumbani kwake. Baada ya mazungumzo kati ya bwana Kilemba, bibi Mnuna na baba yake rafikiye Roda. Bibi Mnuna alitoka mbio chumbani akiwa amebeba virago vyake juu ya kichwa. Alitembea kwa kasi hadi akatoweka. Siku iliyofuata, bwana Kilemba alirudi mjini Mwang'ombe pamoja na wanawe pamoja na Roda. Miaka kadhaa ilipita tangu kifo cha bibi Fatu. Watoto waliokuwa wakisoma wakati huo walitamatisha masomo yao na kupata ajira. Roda alikuwa amehitimu kuwa jaji. Wakati wa likizo moja ya Disemba, bwana Kilemba aliwaalika wanakijiji kwa mkutano wa dharura. Akaja na bibi Mnuna, Roda na wanawe. Alitaka jamii yake isameheane machoni mwa wanakijiji ili maisha kama familia yaendelee sawa. Mwishowe wote walikuwa wamesameheana. Hadithi hii ina maudhui kama vile mali na urithi, afya hasa kuhusiana na magonjwa yanayotokana na mitindo ya maisha, uhalifu kama vile mauaji na utekaji nyara na ushirikiano wa wanakijiji wakati wa mikasa kijiji. Maudhui haya yanachangia mafunzo kwa mtoto msomaji kuhusu maisha katika familia.

4.3 Aina za familia zinazosawiriwa katika *Cheupe na Cheusi*, *Likizo ya Mkosi na Ahaa!*

Roda

Kuna aina mbalimbali za familia zinazosawiriwa katika vitabu vilivyoteuliwa kwa utafiti huu. Katika vitabu vilivyoteuliwa vya kipindi cha 2011–2018 aina za familia ni kama vile familia kiini na familia kiini mwanzo ambazo zinaishia katika familia pana mwishowe. Kinachodhihirika pia ni kwamba suala la aina za familia laweza kuwa tata kwa kuwa familia yaweza kuanza kama familia kiini na baadaye kupanuka na kuchukua mkondo wa aina tofauti ya familia.

4.3.1 Aina za familia zinazosawiriwa katika *Cheupe na Cheusi*

Katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi*, familia inayojitokeza mwanzoni ni familia kiini inayoishi mashambani ambako kuna mazingira yenye miti ya maembe na msitu na mto wanakofulia nguo na kuchota maji. Ni familia kiini inayohusisha mama na baba wazazi pamoja na mtoto wao. Baba aliiwa Maliki naye mama Nikisha na mtoto wao Cheupe. Baadaye, mama yake Cheupe alikufa. Kwa sababu ya upweke, Maliki baadaye alioa mke mwininge aliyeitwa Bititi na wakabarikiwa na mtoto mmoja aliyeitwa Cheusi. Bititi akawa mama wa kambo wa Cheupe. Cheupe alilelewa na mama yake wa kambo pamoja na Cheusi. Kutokana na hali ya kuwepo kwa mama wa kambo, familia kiini ikapanuka na kuwa familia pana ambayo ilihuusisha mama wa

kambo na dada wa kambo. Cheupe alichukiwa na mama huyo wa kambo kutokana na urembo wake. Mama yake wa kambo alikuwa na dhana dumifu kuwa weupe ni bora kuliko weusi na hivyo akamchukia Cheupe kwa sababu mtoto wake aliyemzaa alikuwa mweusi na hakupenda watoto weusi bali angependa yeze apate mweupe kwa vyovyyote vile. Basi, Bititi alikuwa anaumia moyoni na alitamani Cheupe apotee abaki na Cheusi. Familia katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi* inaonekana kukumbwa na hali mbalimbali za kimiujiza. Mojawapo wa miujiza hiyo inawakutanisha binadamu wa hulka mbalimbali kwa mfano Cheupe anakutana na mbilikimo watatu msituni katika nyumba aliyoenda kujikinga mvua. Kukutana huku kulimwokoa kukampa baraka za zawadi tele na hatimaye akarudi nyumbani kinyume na alivyotarajia Bititi, mama yake wa kambo ambaye alidhani angeliwa na wanyama wakali huko mwituni. Katika hadithi hii inajitokeza pia familia ya mbilikimo watatu amba ni wanaume. Familia nyingine inayojitokeza ni familia ya kifalme ambapo Cheupe aliolewa na Mfalme akawa Malkia na wakabarikiwa na mtoto mmoja ambaye alikuwa mvulana.

4.3.2 Aina za familia zinazosawiriwa katika *Likizo ya Mkosi*

Katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi*, familia inayojitokeza ni familia kiini. Familia hii inajumuisha watoto na wazazi wao kama inavyoelezewa katika ukurasa wa 1 tunapoelezewa kuhusu baba yao kuwa aliiwa Dkt. Stephen Ogato na alikuwa mtafiti katika kampuni ya majani chai ya Bubondi katika sehemu iliyoitwa Chorike. Mama yao hajatajwa kwa jina lakini anatambulika vyema katika mazungumzo yake na watoto wake katika ukurasa wa 5 baada ya Otambo na Kerubo kufunga shule na kurudi nyumbani kwa likizo. Familia hii kiini inajihuisha na kushirikiana na familia pana inayohusisha babu na nyanya na watoto wa familia kiini. Familia kiini inaishi mjini lakini mara kwa mara hutembea mashambani ambapo wanajiunga na babu na nyanya na kuwa familia pana. Kama inavyoelezewa katika (uk. 22) kuwa, walipofika kwa babu na nyanya na walikaribishwa kwa furaha. Familia kiini inaonekana kuwa na maisha ya kisasa ambapo watoto wanashughulika na masomo shulen i wakati baba yao anafanya kazi ya kuajiriwa katika miji mbalimbali mbali na nyumbani. Familia hii kiini na familia pana zinaonekana kuwa na uhusiano wa karibu sana huku kila mmoja akimjali mwenzake kama inavyoonekana baba yake Kerubo anapohusika katika ajali ya barabara. Wanafamilia kutoka familia kiini na familia pana walikutana hospitalini Nairobi kumwona.

4.3.3 Aina za familia zinazosawiriwa katika *Ahaa! Roda*

Katika hadithi ya *Ahaa! Roda*, familia ilijojitokeza ni familia kiini ambapo kuna wazazi na mtoto. Baba anaitwa bwana Gidamu, mama bibi Fatu na mtoto wao Roda. Baba yake Roda alifariki kutokana na maradhi ya saratani ambayo yanatokana na mitindo ya maisha hasa ya kisasa. Hii inaashiria kuwa bwana Gidamu alikuwa tajiri. Hii inathibitika hasa kutokana na maelezo katika (uk wa 1) ambapo tunaelezewa kuwa Bibi Fatu alikuwa na mali nyingi na ambayo inaonekana kuwa iliachwa na bwana Gidamu alipokufa. Mama yake Roda alikuwa mama mwenye mkono wazi, utajiri mwangi na ukarimu. Kwa bahati mbaya, mama huyu wa Roda aliaga dunia baadaye kwa kuuawa. Roda alibaki yatima. Ndugu yake babake Roda aliyeitwa bwana Kilemba alijitolea kumlea Roda pamoja na watoto wake. Hapo Roda akawa ameingia katika familia pana ambayo inahusisha ami ambaye ni bwana Kilemba na shangazi ambaye anaitwa bibi Mnuna. Bwana Kilemba anasema katika (uk wa 5) kuwa atamchukua Roda kwake nyumbani waishi naye baada ya mazishi ya mama yake. Atamshughulikia sawa na watoto wake ambao baadhi yao ni rika lake na pia walisoma katika darasa sawa naye. Hata hivyo, maisha katika familia ya pili ya Roda yalikuwa na mateso mengi. Bibi Mnuna hakumpokea Roda kwa dhati katika nyumba yake. Walimfanya kijakazi na watoto wake bila bwana Kilemba kujua. Roda alifanya kazi zote za nyumbani.

4.4 Usawiri wa familia kama taasisi katika *Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda*

Katika sehemu hii, utafiti huu ulichunguza usawiri wa familia kama taasisi kwa kurejelea vitabu vilivyoteuliwa vya kipindi cha 2011–2018 vinavyoangazia familia ambamo watoto wanalelewa. Uchanganuzi wa hadithi hizi ulichunguza jinsi watoto wanavyoathiriwa na maisha ya familia kama kundi la kijamii ambamo mna watu mbalimbali wanaouna hiyo familia. Uchunguzi huu ulisaidia kubainisha tofauti katika usawiri wa familia za vipindi viwili vinavyorejelewa katika utafiti huu.

4.4.1 Usawiri wa familia kama taasisi katika *Cheupe na Cheusi*

Familia inayosawiriwa katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi* ni familia iliyokumbwa na matatizo mengi yatokanayo na hali ya kuwepo katika familia pana. Mama wa kambo wa Cheupe anatawaliwa na hisia za chuki dhidi ya Cheupe. Anafanya kila njama ili kumdhuru Cheupe akiwa

na nia ya kumuua. Hata hivyo kila Cheupe anapotiwa kwenye mtego wa kuuawa anaibuka akiwa mshindi kwa kupata mafanikio fulani kimiujiza. Hatimaye Cheupe anafanikiwa na kuolewa na mfalme. Katika hadithi hii, familia yene mama wa kambo inasawiriwa kama iliyo na changamoto nyingi kutokana na mama wa kambo kutompenda mtoto aliyepanga hasa ikiwa watoto hao wanafanikiwa zaidi ya watoto wake aliowazaa. Jambo hili laelezewa vyema katika (uk wa 3 na 13) ambapo Bititi alifanya njama kumdhuru Cheupe. Njama ya kwanza alimtuma Cheupe msituni ili aliwe na wanyama na njama ya pili alipanga tena kumwangamiza Cheupe kwa kumtuma mtoni, ambao wenyewe ulijaa ngwena na viboko waliokuwa hatari sana ili aweze kuuliwa na wanyama hao.

Katika familia hii mama wa kambo anamwonea wivu mtoto asiyé wake wa kuzaa na kumpendelea mtoto alimyezaa kwa jina Cheusi. Mama wa kambo akiwa na mtoto wake Cheusi walimwonea Cheupe wivu kwa sababu ya baraka alizopata kila walipojaribu kumwangamiza. Waliamua kumfanya Cheupe kijakazi wao. Jambo hili la dhihirika katika (uk wa 13). Baadaye wawili hawa walijaribu kumwangamiza wakati alipoolewa na mfalme. Walitembea kwa mfalme na kumrusha Cheupe nje ya dirisha akaanguka mtoni (uk. 15). Hata hivyo juhudí zao hazikufanikiwa kumwangamiza Cheupe na hatimaye waliposhindwa ikabidi wamwombe msamaha Cheupe ambapo Cheupe alikubali kuwasamehe. Hapa suala la makuzi linazuka kwamba mamake Cheusi anamfundisha bintiye kujenga chuki, kisasi na wivu. Kimaadili, jambo hili ni kinyume na mifumo ya kifamilia na jinsi inavyotarajiwa kuhusika katika kujenga au kuendeleza tabia za kimaadili mionganoni mwa watoto wanaolewa.

4.4.2 Usawiri wa familia kama taasisi katika *Likizo ya Mkosi*

Katika hadithi *Likizo ya Mkosi*, familia iliyojitekeza ni familia iliyo na wazazi wote wawili yaani baba na mama ambao walishirikiana vilivyo katika majukumu yote ya kuwalea wana wao. Kwa mfano, katika kuwapa chakula, mavazi, afya bora na hata elimu. Pia familia yote ilipenda kutangamana na jamaa wao wengine wote ndiposa wazazi waliwapeleka wana wao kwenda kuwasalimia nyanya na babu mashambani wakiwa wamewabebéa zawadi. Walimpelekea nyanya zawadi ya ufagio na babu zawadi ya fimbo (uk. 26). Jambo hili la kuwabebéa zawadi linaonyesha maadili ya upendo katika familia. Nyanya na babu walishukuru huku wakisifu zawadi walizopelekewa. Familia hii inasawiriwa kama iliyopenda elimu ya watoto wao. Jambo

hili la dhihirika katika ukurasa wa 1 ambapo baba anawahimiza kutia bidii masomoni kwa kuwaahidi kuwatembeza kwa nyanya na babu ikiwa watafanya vizuri masomoni.

Familia hii pia inasawiriwa kama yenye watoto walio na bidii. Bidii ni maadili muhimu katika makuzi ya watoto. Watoto ambao ni Otambo na Kerubo walitia bidii masomoni. Walijua kibali chao cha kwenda mashambani kuwasalimia nyanya na babu kitatokana na kufanya vyema kwenye mtihani wao wa mwisho wa muhula. Baada ya mtihani wa muhula, watoto hawa walifanya vizuri sana na walifurahia matokeo. Jambo hili la dhihirika vyema katika (uk. 2 na 8) ambapo Otambo na dada yake Kerubo walipigiwa makofi na wanafunzi shule nzima. Walitembea kwa ujasiri kwenda kupokea zawadi zao huku wakivaa tabasamu kwenye nyuso zilizong'ara kwa furaha. Watoto hao walipenda kusaidia nyumbani. Walipomaliza kula, Otambo alimsaidia mama yao kuondoa vyombo mezani. Kerubo naye alipangusa meza hiyo. Otambo na Kerubo walipenda sana kumsaidia mama yao kufanya kazi za nyumbani (uk. 8).

Aidha, familia hii inasawiriwa kama yenye maadili ya umoja na ushirikiano. Ushirikiano unajitokeza baina ya wazazi wenyewe, kati ya wazazi na wana wao na baina ya watoto wenyewe katika familia. Mama alikuwa anaamka mapema kuwatayarishia wanawe kiamsha kinywa huku baba naye akikubali kuwapeleka watoto mashambani. Watoto nao walikubali kujitayarisha tayari kuondoka. Mfano mwingine wa ushirikiano unapatikana katika (uk 50) wakati ambapo baba alipata ajali na kulazwa katika hospitali ya Nairobi. Nyanya, babu, wajukuu na mama wote walishirikiana kwenda kumjulia hali baba katika hospitali. Hii inaonyesha familia kiini na familia pana kwa jumla zilishirikiana kuendeleza maadili ya familia kama taasisi.

4.4.3 Usawiri wa familia kama taasisi katika *Ahaa! Roda*

Familia katika hadithi ya *Ahaa! Roda* inasawiriwa kama familia kiini. Baada ya kifo cha wazazi wake, Roda anahamia katika familia ya ami na shangazi na inakuwa kwamba ameingia katika familia pana. Bibi Mnuna ambaye alikuwa mama mlezi wa Roda hakufurahishwa na wazo la kumchukua Roda baada ya kifo cha wazazi wake ili kumlea sawa na watoto wake aliowazaa. Hivyo alimchukia na kumtesa. Mgogoro mwingine ilitokana na kuwepo kwa familia pana na suala la urithi wa mali ya babake Roda ambapo bwana Sumu hakutaka mama yake Roda awe ndiye angerithi mali ya mumewe. bwana Sumu alikuwa na nia mbaya ya kumuua mamake Roda

ili kumwondoa katika urithi wa mali ya ndugu yake. Jambo hili la dhihirika kutokana na maneno haya yaliyosemwa na mzee Mkongojo ambaye ni mwanakijiji wa kawaida. Alikuwa anawaambia wazazi wa rafikiye Roda kuhusu kutekwa nyara kwa bibi Fatu na mwanawewe Roda na jinsi walivyofanikiwa kumpata bibi Fatu lakini walihitaji usaidizi wampate Roda ambaye hawakuwa wameweza kumpata (uk. 10). Wakati huo huo kulikuwa na maoni kuwa Roda hangerithi mali ya baba yake kwa kuwa alikuwa msichana. Hata hivyo, mwishowe Roda ndiye aliyerithi mali hiyo kwa mujibu wa sheria. Sajenti Kizito ambaye ni mmoja wa serikali alitoa hotuba kwa wanakijiji na kusema kuwa Roda ndiye atakayekuwa mrithi wa mali ya mama yake. Hii ilikuwa ni kinyume na maoni ya wengi ambao walikuwa wameshikilia mila za kitamaduni kuwa msichana harithi mali ya wazazi wake (uk. 43). Hapa familia inasawiriwa kama ambayo inaweza kuwa mstari wa mbele kuleta mabadiliko ya desturi zilizopitwa na wakati katika jamii ya sasa.

Kwa upande mwengine, ndugu mwengine bwana Kilemba alikuwa na msimamo tofauti na huo kwa kuwa alikuwa na huruma na mama yake Roda alipouliwa. Yeye aliamua kumchukua Roda na kumlea kama mtoto wake. Bwana Kilemba alikuwa mwenye utu. Yeye alikuwa anapendwa na watu na alikuwa mkarimu. Alijitolea kuishi na Roda kwake nyumbani kwa sababu alibaki mtoto yatima. Jambo hili la dhihirika katika (uk. 55) ambapo bwana Kilemba alisema kuwa shemeji yake aliyeaga alikuwa mionganoni mwa wanawake wenye nyoyo safi. Aliahidi kuwa atamlea Roda baada ya mazishi ya mama yake kama anavyowalea watoto wake. Mwishowe wanafamilia hawa wanaamua kusameheana na kuishi kwa umoja. Hivyo, uovu mionganoni mwa wanafamilia unaonekana kushindwa na wema.

4.5 Uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika *Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda*

Katika kijisehemu hiki utafiti huu unachunguza uhalisia wa kifamilia katika vitabu teule vya kipindi 2011-2018. Uchunguzi huu ulifanywa kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia wa kijamii. Katika utafiti huu uhalisi wa kifamilia ulijitokeza kuwa suala tata na familia katika vitabu vilivyoteuliwa zinaakisika kwa njia mbalimbali kama zilivyo za aina mbalimbali na zilizo changamano. Hadithi hizi zimejengwa katika misingi ya familia kielelezo na uhalisia tofauti umeweza kuonekana.

4.5.1 Uhaliwa kifamilia unavyoakisika katika *Cheupe na Cheusi*

Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, familia inayosawiriwa katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi* ni kiwakilishi cha familia halisi ambapo pana mama wa kambo katika baadhi ya jamii. Kunazo baadhi ya jamii ambazo panapokuwepo na mama wa kambo, chuki hujitokeza katika familia. Mathalani, katika jamii ya Wakikuyu pana methali isemayo kuwa wake wawili ni vyungu viwili vya uchawi. Hivyo katika jamii hii inaaminika kuwa mizozo hutokea katika familia panapokuwa na hali sawa na hiyo. Si ajabu kuona kupitia vyombo vya habari mizozo katika familia kama hizo inayosababishwa na chuki na wivu wa mama wa kambo dhidi ya watoto wa mke mwingine kama inavyojitokeza katika hadithi hii.

4.5.2 Uhaliwa kifamilia unavyoakisika katika *Likizo ya Mkosi*

Kwa mtazamo wa nadharia ya uhalisia, familia inayosawiriwa katika hadithi *Likizo ya Mkosi*, inaweza kulinganishwa na familia halisi za watu wa tabaka la kati kiuchumi ambao kwa maoni ya utafiti huu aghalabu huwa na wazazi wanaofanya kazi pengine mijini na watoto wao wanaosoma huku wakihimizwa kufanya bidii masomoni na mara kwa mara familia hizo huwatemebeza watoto wao kuwasalimia nyanya na babu ambao aghalabu husawiriwa kama wanaoishi katika sehemu za mashambani kama ilivyo katika hadithi husika. Familia hizo mara nyingi huishi maisha yanavyojitokeza katika familia ya Dkt. Ogato ambapo familia huwa na uwezo wa kiuchumi wa kiwango fulani cha kuweza kuwa na gari la familia, watoto kuhudhuria shule nzuri ambapo pia wazazi ni kielelezo kizuri cha usomi kama vile baba yao alivyokuwa amesoma kiasi cha kuitwa daktari. Kimatibabu, familia kama hizi huwa na uwezo wa kupata matibabu katika hospitali za kiwango cha juu kama vile hospitali ya Nairobi ambapo Dkt. Ogato, baba yao, alipolazwa baada ya kuumia katika ajali ya barabarani. Familia ya Dkt. Ogato ni kiwakilishi cha familia adilifu ambazo huwajali wanafamilia wao wanapokuwa katika shida kama vile inavyodhahirika familia ya Dkt. Ogato inapofika hospitalini kumwona na kujua kilichotokea pamoja na kutaka kujua kitendawili cha vyeti vyake kupatikana katika mfuko wa mtu aliyekufa.

4.5.3 Uhaliwa kifamilia unavyoakisika katika *Ahaa! Roda*

Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, migogoro inayopatikana katika familia hii inasawiri uhalisia wa maisha katika familia halisi hasa mionganoni mwa familia za watu walio na mali

nyingi kama walivyokuwa wazazi wa Roda. Mgogoro unaotokana na urithi wa mali baada ya kifo cha baba mwenye mali huweza kuripotiwa mara kwa mara kupitia vyombo vyahabari. Jamaa huwa wanazozana kuhusu ni nani atakayemrithi marehemu. Mzozo sawa na huu ndio unaoakisiwa katika hadithi ya *Ahaa! Roda*. Aidha, mzozo mwengine wa kihalisia unaosawiriwa katika hadithi hii ni kuhusu shangazi kutofurahia kumlea mtoto kama Roda aliyeachwa na wazazi walioaga dunia. Jambo la kuridhisha ni kuwa katika hadithi hii panaonekana kuwa na maridhiano mwishowe ambapo wanafamilia wanakubali kusameheana na kuishi kwa amani. Kihalisia, maridhiano huhimizwa katika jamii halisi ya mwandishi. Katika jamii ya Kenya kumekuwa na juhudi nyingi za maridhiano panapotokea mizozo ya kijamii au ya kisasa. Mfano mmoja wa maridhiano kama hayo yenye lengo la kuleta amani ni salamu za kushikana mikono kati ya viongozi waliokuwa na mzozo kama ishara ya kuonyesha kuisha kwa mzozo na nia yao ya kusameheana. Katika baadhi ya jamii halisi ni kawaida ndugu wa baba au wa mama kumchukua mtoto ambaye wazazi wake wamekufa akiwa mchanga na kumlea kama inavyodhahirika katika *Aha Roda!*

4.6 Hitimisho

Sura hii imetua muhtasari wa hadithi za utafiti huu za kipindi cha mwaka 2011–2018 ambazo ni *Cheupe na Cheusi* (2013) *Likizo ya Mkosi* (2014) na *Ahaa! Roda* (2017) na kisha kujadili aina za familia zinazosawiriwa katika *Cheupe na Cheusi*, *Likizo ya Mkosi* na *Ahaa! Roda*. Aina za familia zilizojitokeza ni familia kiini. Imebainika kuwa familia nyingi huanza kama familia kiini kisha zaweza kuchukua mikondo mingine na kuwa familia pana hasa kutokana na mambo kama vile kifo cha mzazi mmoja ambapo mzazi anayebaki huoa au huolewa na mtu mwengine na mtoto kulelewa na mzazi asiyé wake wa kumzaa. Hali hii pia imebainika kusababishwa na kifo cha wazazi wote wawili ambapo baadaye mtoto au watoto wanaobaki yatima huchukuliwa na ndugu za wazazi na kulelewa katika familia nyingine. Katika hadithi zilizochunguzwa familia nyingi zinaishi mashambani na ambapo inakuwa ni rahisi kutangamana na familia pana. Vilevile, sura hii imejadili usawiri wa familia kama taasisi katika *Cheupe na Cheusi*, *Likizo ya Mkosi* na *Ahaa! Roda* na kubainika kuwa familia kama kundi la kijamii wanaishi kwa utangamano hasa katika familia kiini. Katika familia pana wakati mwengine migogoro hutoke la kini imebainika kuwa maridhiano mwishowe hupatikana katika familia. Wengi wa wanafamilia katika utafiti huu walionekana kuwa katika kiwango cha kadri cha kiuchumi. Familia nyingi za kisasa zilionekana

kutilia maanani masomo ya watoto wao. Wengi wao wanapata watoto wachache kama mmoja au wawili. Palipo na kifo wanaoathirika sana ni akina mama na hatimaye kuchunguza uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika *Cheupe na Cheusi*, *Likizo ya Mkosi* na *Ahaa! Roda* kwa kutumia nadharia ya uhalisia. Imebainika kuwa familia zinazoakiswi katika hadithi zilizoteuliwa ni kiwakilishi halisi cha familia za kipindi cha kiwakati kinachowakilishwa na vitabu vilivyoteuliwa.

SURA YA TANO

MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii ya tano, muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti yametolewa. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kubainisha usawiri wa familia ya kisasa katika fasihi ya watoto nchini Kenya. Lengo hili limeweza kuafikiwa baada ya kuchunguza hadithi sita ambazo zimegawanya katika migao miwili. Mgao wa kwanza ni vitabu vyta hadithi za watoto vilivytungwa kati ya miaka ya 2000 hadi 2010 ambavyo ni *Mwepesi wa Kusahau* (2005), *Nampenda mama wa Kambo* (2006) na *Madalala Abadilika* (2009). Mgao wa pili ni vitabu vyta hadithi za watoto vilivytungwa kati ya miaka ya 2011 hadi 2018 ambavyo ni *Cheupe na Cheusi* (2013), *Likizo ya Mikosi* (2014) na *Ahaa! Roda* (2017). Mgao huu wa kiuteuzi ulilenga kuangalia ni kwa jinsi gani tungo hizi zinaakisi uhalisi wa kiwakati katika kusawiri familia.

Muhtasari

Utafiti huu ulihusu usawiri wa familia ya kisasa katika fasihi ya watoto nchini Kenya. Vitabu vilivytumika katika utafiti huu vilikuwa sita ambavyo ni *Mwepesi wa Kusahau*, *Nampenda mama wa Kambo*, *Madalala Abadilika*, *Cheusi na Cheusi*, *Likizo ya Mkosi na Ahaa! Roda*. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni ambayo yalikuwa kubainisha aina za familia zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto, kutathmini usawiri wa familia kama taasisi katika fasihi ya watoto na kuchunguza uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika hadithi za watoto. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamii. Nadharia hii iliufaa utafiti huu katika kulinganisha uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika hadithi za watoto na maisha halisi ya kifamilia. Vitabu sita vilivytoteuliwa vyta hadithi za watoto, vilionekana kuwa na familia kiini na familia pana na ambazo zimeakisika kwa njia zenye uhusiano mkubwa na hali halisi ya maisha katika familia hasa nchini Kenya ambapo hadithi hizi zimeandikiwa.

5.3 Matokeo ya utafiti

Sehemu hii inaangazia matokeo ya utafiti kwa jumla. Matokeo haya yanapania kujibu maswali ya utafiti na hivyo yamepangwa kulingana na maswali hayo ambayo ni: Je ni familia za aina gani zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto? Je, familia kama taasisi inaakisika vipi katika fasihi ya watoto? Je, uhalisi wa kifamilia unaakisika kwa kiasi gani katika hadithi za watoto?

5.3.1 Matokeo kuhusu aina za familia zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto

Aina za familia zinazosawiriwa katika utafiti huu ziligawanywa katika vipindi viwili. Kipindi cha kwanza kilihusu hadithi za fasihi ya watoto zilizoandikwa katika kipindi cha mwaka 2000–2010 ambazo ni *Mwepesi wa Kusahau, Nampenda Mama wa Kambo na Madalala Abadilika*. Mgao wa kipindi cha pili ulihusu hadithi zilizoandikwa katika kipindi cha mwaka 2011–2018 ambazo ni *Cheupe na Cheusi, Likizo ya Mkosi na Aha! Roda*. Katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* na *Madalala Abadilika*, familia iliyojitokeza ni familia kiini ilhali katika hadithi *Nampenda Mama wa Kambo* familia inayojitokeza mwanzo ni familia kiini ingawa baadaye ilichukua mkondo wa familia pana. Katika kipindi cha pili familia inayojitokeza ni familia kiini katika *Likizo ya Mkosi* na familia kiini ambayo baadaye inachukua mkondo wa familia pana katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi* na *Aha! Roda*.

Kwa kulinganisha aina za familia za kipindi cha 2000–2010 na kipindi cha 2011–2018 hakukubainika tofauti kubwa kati ya aina za familia katika vipindi hivyo. Kila kipindi kinaonekana kuwa na aina zilezile za familia ambapo kuna familia kiini na familia pana. Familia kiini katika kipindi cha kwanza inadhihirika katika *Mwepesi wa Kusahau* na *Madalala Abadilika* ilhali katika kipindi cha pili inabainika katika *Likizo ya Mkosi*. Kila familia kwenye vitabu hivi ina baba, mama na watoto wao. Utafiti huu uligundua kuwa kinachosababisha hali ya kuwepo kwa familia pana ni kifo cha mama mzazi ambapo mume anayebaki huoa mke mwingine na hivyo watoto wa mke wa kwanza kulelewa na mama wa kambo. Hali hii inadhihirika katika *Nampenda mama wa Kambo* katika hadithi za kipindi cha kwanza na *Cheupe na Cheusi* na *Aha! Roda* katika hadithi za kipindi cha pili (2011 – 2018). Katika *Aha! Roda* hali hii ilisababishwa na kifo cha wazazi wote wawili na ambapo Roda alibaki yatima. Alichukuliwa na ami yake ambaye ni ndugu mdogo wa baba yake. Tofauti na vifo vyta mama za watoto katika hadithi za kipindi cha kwanza ambao walikufa vifo vyta kawaida kama vile kufa wakati wa kujifungua, kifo cha mama yake Roda kinaonekana kusababishwa na upiganiaji wa mali katika familia za kisasa. Kwa hivyo, kutokana na utafiti huu, ingawa aina za familia zinabaki kuwa zilezile, hali zinazosababisha hali za kuwepo kwa familia pana zinatofautiana katika vipindi hivi kutokana na tofauti za hali za maisha.

5.3.2 Matokeo kuhusu usawiri wa familia kama taasisi katika fasihi ya watoto

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kuwa katika kipindi cha kwanza (2000–2010) familia ilisawiriwa kama ambayo inashughulikiwa na mama zaidi ya baba hasa kuhusu malezi ya watoto na shughuli nyingine za maisha ya kila siku. Baba katika familia zinazopatikana katika hadithi zote tatu za kipindi hicho anatajwa tu lakini haonekani katika maisha ya kila siku ya kifamilia akitekeleza majukumu yoyote. Mfano ni katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* ambapo baba ametajwa katika (uk. 1) pekee kuelezea kuwa alikuwa tabibu wa mifugo wilayani Kericho. Vilevile, katika *Madalala Abadilika*, baba haonekani na ametajwa tu katika ukurasa wa 8 ikielezewa kuwa alikuwa ameenda safari. Hatimaye katika *Nampenda Mama wa Kambo* baba alitajwa tu kwa jina katika ukurasa wa kwanza na baadaye anaonekana tu baada ya mke wake kuaga dunia na wakati tu anapomwoa mke mwingine na kisha kutoweka na haonekani akimsaidia mtoto masomoni wala katika shughuli nyingine katika makuzi yake.

Katika kipindi cha pili (mwaka 2011–2018) hali hii inaendelea kubadilika ambapo baba katika familia anasawiriwa kama anayeshughulikia majukumu yake vilivyo. Kwa mfano, katika *Likizo ya Mkosi* baba anaonekana akishirikiana na mama katika maisha ya kila siku katika malezi ya watoto wake. Katika hadithi ya *Aha! Roda* baba anasawiriwa kama aliyekuwa mwenye bidii na anayeshughulikia familia yake hadi pale alipoaga dunia. Katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi* baba anaonekana mwanzoni mwa hadithi akimfurahia mtoto na pia anasawiriwa kama aliyeshiriki kumlea *Cheupe* hadi pale alipozidiwa na upweke na kuoa mke wa pili ambaye alifanya hali ya utulivu kubadilika katika familia hiyo. Baba haonekani katika malezi ya kila siku na kinachojitokeza ni kuwa yuko katika shughuli zake au za kikazi.

Usawiri mwingine wa familia unaobainika katika kipindi cha kwanza ikilinganishwa na kipindi cha pili ni kuhusu hali ya kuwepo kwa mama wa kambo. Jamii ya kipindi cha hapo awali inayowakilishwa katika hadithi ya *Nampenda Mama wa Kambo* ilionekana kukubali kuwepo kwa mama wa kambo ambapo mama wa kambo anamlea kwa upendo mtoto aliyempata kutoka kwa mama aliyeaga dunia kinyume na jamii ya sasa inayowakilishwa katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi* na *Aha! Roda* ambapo mama mlezi anawatesa watoto aliorithi kutoka kwa mama mzazi. Kwa mujibu wa utafiti huu hali hii ya sasa ya kina mama kutowakaribisha watoto wanaotokana na uhusiano mwingine inaweza kuelezewa kuwa inayotokana na hali ya

mabadiliko ya kiuchumi na ubinafsi ambapo mama anataka yeye na watoto aliowazaa warithi mali iliyochumwa bila kugawana na watoto wa kulea kama ilivyobainika katika hadithi ya *Aha! Roda*.

Usawiri mwengine muhimu wa kifamilia ni kuhusu mitazamo ya kielimu. Katika hadithi zote tatu za kipindi cha kwanza ambazo ni *Mwepesi wa Kusahau, Nampenda Mama wa Kambo* na *Madalala Abadilika*, watoto katika familia wanahudhuria shule lakini hawaelekei kuwa na maono kuhusu wangependa elimu iwatimizie mambo gani. Kinyume na haya katika hadithi za kipindi cha pili watoto katika familia wanasawiriwa wakisoma wakiwa na malengo mahususi. Mfano ni katika hadithi ya *Aha! Roda*, Roda alinua kuwa jaji baada ya kusoma. Hakukata tamaa licha ya matatizo yaliyomkabili na wakati ulipofika aliweza kutimiza ndoto yake ya kuwa jaji. Vilevile, katika familia kwenye hadithi ya *Likizo ya Mkosi* watoto wahusika wanafanya bidii masomoni waweze kufanikiwa kama baba yao ambaye alikuwa amefikia cheo cha udaktari katika chuo kikuu na kuwa mtafiti katika kampuni ya majani chai.

5.3.3 Matokeo kuhusu uhalisi wa kifamilia unavyoakisika katika hadithi za watoto

Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, familia katika hadithi za utafiti huu ni viwakilishi vya familia halisi katika jamii halisi. Mathalani, kuhusiana na usawiri wa familia kama ambavyo inashughulikiwa na mama zaidi kuliko baba, ilibainika katika utafiti huu; au kumekuwa na madai mengi kuitia vyombo vya habari kama vile redio, runinga na magazeti kuwa kina baba wengi wanajulikana tu kwa jina wala hawaonekani wakitekeleza majukumu yao katika familia sawa na ilivyokuwa katika familia hasa za hadithi za kipindi cha kwanza katika hadithi za utafiti huu ambazo zilisawiriwa kama ambazo zinashughulikiwa na mama zaidi ya baba, hasa kuhusu malezi ya watoto na shughuli nyingine za maisha ya kila siku. Baba katika familia zinazopatikana katika hadithi zote tatu za kipindi hicho anatajwa tu lakini haonekani katika maisha ya kila siku ya kifamilia akitekeleza majukumu yoyote. Hata hivyo, uhalisia mwengine unathibitika katika hadithi za kipindi cha pili ambapo kutokana na kuwepo kwa shughuli katika jamii za kujaribu kuwahimiza kina baba kama vile kuwepo kwa siku ya kina baba kila mwaka, kumekuwa na mabadiliko japo ya polepole ambapo kina baba hasa katika familia za kiwango cha kati kiuchumi kama vile inavyoakisika katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi*. Wanaendelea

kuonekana wakitekeleza majukumu yao kikamilifu katika familia katika kipindi cha hivi karibuni.

Kuna uhalisia vilevile kuhusiana na mabadiliko ya kiwakati yanayotokana na hali ya kuwepo kwa mama wa kambo katika familia na mivutano ya urithi wa mali inavyobainika katika hadithi zilizoteuliwa katika utafiti huu. Jamii ya kipindi cha hapo awali inayowakilishwa katika hadithi ya *Nampenda Mama wa Kambo* ilionekana kukubali kuwepo kwa mama wa kambo kinyume na jamii ya sasa inayowakilishwa katika hadithi ya *Cheupe na Cheusi na Aha! Roda* ambapo mama mlezi anawatesa watoto aliorithi kutoka kwa mama mzazi. Kihalisia, katika jamii ya sasa inaaminika kuwa mizozo hutokea katika familia panapokuwa na watoto kutokana na wake tofauti na si ajabu kuona kupitia vyombo vyta habari mizozo katika familia kama hizo inayosababishwa na chuki na wivu wa mama wa kambo dhidi ya watoto wa mke mwingine kama inavyojitokeza katika hadithi hii.

Kuhusu elimu, uhalisia ni kwamba elimu inatiliwa mkazo katika jamii ya sasa. Kwa mfano, serikali nchini Kenya hutengea elimu kiasi kikubwa cha pesa katika bajeti yake. Watoto katika familia nyingi huhimizwa wasome kwa bidii ili waweze kuwa na maisha bora ya baadaye kama inavyodhihirika katika familia zinazosawiriwa katika hadithi za utafiti huu ambazo zina mitazamo chanya kuhusu elimu. Katika hadithi zote tatu za kipindi cha kwanza watoto katika familia wanahudhuria shule na katika hadithi za kipindi cha pili watoto katika familia pia wanasawiriwa wakihudhuria shule na wakisoma kwa bidii huku baadhi yao kama vile Roda na Kerubo na Otambo wakiwa na malengo mahususi. Cheupe na Cheusi hawakuelezewa iwapo walisoma au hawakusoma.

Hitimisho

Kwa muhtasari, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa aina za familia zimebaki kuwa zilezile hata vipindi vyta kiwakati vinapobadilika. Aina hizo ni familia kiini na familia pana. Kimsingi imebainika kuwa familia zote hizi zimeanza kama familia kiini kabla ya nyingine kuchukua mkondo wa familia pana. Kinacho sababisha kuwepo kwa familia pana kimeonekana aghalabu kuwa kuingia kwa mama wa kambo katika familia baada ya kifo cha mama mzazi ambapo baba anaoa mke mwingine kulea mtoto au watoto walioachwa. Matokeo haya hata hivyo

yamebainisha kuwa kinachobadilika kutokana na wakati ni hali zinazosababisha; kuwepo kwa familia pana zenyne mama wa kambo. Kuhusu usawiri wa familia, utafiti huu, ulibainisha kuwa katika kipindi cha awali familia ilisawiriwa kama ambayo inashughulikiwa na mama zaidi ya baba hasa kuhusu malezi ya watoto na shughuli nyingine za maisha ya kila siku. Hali ilitokana hasa na baba kwenda mahali pasipojulikana kwa kile kinachonekan kuwa shughuli za kikazi na mambo sawia na hayo. Hali hii inaendelea kubadilika katika kipindi cha sasa ambapo baba katika familia anasawiriwa kama anayeshughulikia majukumu yake vilivyo. Mabadiliko mengine yanayojitokeza katika usawiri wa familia ni kuhusu mama wa kambo ambao hapo awali alionekana kuishi vyema na watoto aliokuta katika familia lakini katika kipindi cha sasa hali hii imebadilika na chuki kuwepo baina ya mama wa kambo na watoto anaorithi. Familia za vipindi vyote viwili katika utafiti huu vilionekana kuthamini elimu huku watoto wa familia za sasa wakionekana kuwa na malengo fulani wanayotaka elimu iwatimizie. Kwa mtazamo wa nadharia ya uhalisi, usawiri huu ulionekana kuwa na uhusiano mkubwa na familia halisi katika jamii.

5.5 Mapendekezo ya utafiti

Kutokana na matokeo ya utafiti huu inapendekezwa kuwa usomaji wa fasihi ya watoto shulenii usiwe wa burudani tu lakini utilie mkazo ujenzi wa mitazamo chanya mionganii mwa watoto wakiwa wangali wadogo kuhusiana na aina za familia kwa kuwa watoto ni kundi la jamii lililo na umuhimu mkubwa na linaloambatanishwa kwa karibu sana na familia. Makuzi ya watoto na ufunzaji wa maadili ni mambo yawezekanayo sio katika misingi ya familia tu bali pia kuitia mafunzo ya fasihi ya watoto. Ufanisi wa watoto katika maisha yao ya baadaye unategemea kwa kiasi kikubwa uelewa wa aina za familia wanazokulia na kulelewa. Kwa kuwa mafunzo kuhusiana na maadili ya kifamilia huenda yasipatikane nyumbani kwa njia ifaayo, ni muhimu fasihi ya watoto ilenge kuwapa watoto mafunzo haya kutokana na usomaji unaolenga kimakusudi haja ya kulelewa na kuitambua mifumo ya kifamilia na jinsi inavyoathiri makuzi yao na jinsi ya kuishi katika uhalisi changamano wa kifamilia. Jambo hili litawezesha watoto wanaokulia katika aina mbalimbali za familia kujiamini na kufuata ndoto zao licha ya changamoto wanazokabiliana nazo kama zile zinazotokana na mama wa kambo au kutokuwepo kwa baba. Kutokana na matokeo ya utafiti huu inapendekezwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu usawiri wa familia katika nyakati za awali kabisa.

MAREJELEO

- Ayisi. E. O. (1992) *An introduction to the study of African Culture* (2nd ed.). Nairobi: East African Education Publishers.
- Babusa, H. (2013) *Cheupe na Cheusi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Bakize, L.H. (2014) *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.
- Eagleton, T. (1996) *Literary Theory*. London: Blackwell Publishing.
- Hunt, P. (2002) *Understanding children's literature*. Taylor & Francis e-library.
- Kairu, W.M. (2005) Uhali na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Karuga, M.N. (2005) Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule za Msingi nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Kisembo, B (1998) *African Christian Marriage*. Nairobi: Pauline Publications.
- Magoti, E. (2004) "Globalization in Africa: Its Impact on Families and Christian Responses" in Kyomo, A. and Selvan, S. (Eds), *Marriage and Family in African Christianity* pp 29-52. Nairobi: Action Publishers.
- Lukacs, G. (1979) *The Meaning of Contemporary Realism*, London: Merlin.
- Matundura, B. (2005) *Mwepesi wa Kusahau*. Nairobi: Phoenix.
- Matundura, B. (2007) Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Matundura, B. (2014) *Likizo ya Mkosi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mbatiah, M. (2016) *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mbiti, J. (1969) *African Religions and Philosophy*. London: Heinman Education Books Ltd.
- Miricho, E.M. (2015) Usawiri wa Watoto katika Hadithi za "Mwepesi wa Kusahau" na "Likizo ya Mkosi". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Miricho, M. (2016) *Msingi wa Insha*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Miricho, M. na E.M. Mbuthia (2017) The Impact of the Depiction of Children in Selected Swahili Children Stories katika *The International Journal of Contemporary Applied Sciences*. Vol 4, No. 1, January, 2017 (ISSN: 2308- 1365).

- Miricho, M. Sheila P. Wandera-Simwa na Nabea Wendo (2019) "Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Mshikamano wa Kitaifa" katika *Mwanga wa Lugha–Makala Teule ya Kongamano la CHAKITA 2018* (ISSN: 2412-6993). Moi University Press.
- Mpesha, N. (1996) Children's Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of its Growth and Development. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Musau, P. na Pamela, N. (1997) "Research in Kenyan Universities: Where are we now?" Katika: Rose Marie-Beck Lutz Diegner, na Thomas Geider (wh), *AAP 51. Swahili Forum*. Afrikanistische Arbeitspapiere. Institut fir Afrikanistik. Koln. 219-229.
- Muthubi, F. (2005) Mikakati na Mbinu za Usilimishwaji katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Nandwa, R. (2006) *Nampenda Mama wa Kambo*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nandwa, R. (2013) *Madalala Abadilika* Nairobi: Queenex.
- Ngugi, P.M. (2009) The State of Children's Literature in Kenya. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Vienna, Austria.
- Ngugi, P.M. (2012) "Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati." katika: S. Omari na G. Mrkaria (wh) *Mulika*. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na. 31. 2012 12 - 26 ISBN 0856-0129.
- Ngugi, P.M. (2014) Fasihi ya Watoto katika Kutekeleza Mahitaji ya Mtoto Kisaikolojia, katika: D.P.B. Massamba na L.H. Bakize (wh) *Kiswahili Journal of the Institute of Kiswahili Studies* (TATAKI). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vol. 77.2014 170- 180 ISBN 0856-048 X.
- Ngure, A. (2003) *Fasihi Simulizi*. Nairobi: Phoenix.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyambeka, T. (2017) *Ahaa! Roda*. Nairobi: Queenex.
- O' Donovan, W. (2000), *Biblical Christianity in Modern Africa*, Carlisle: Paternoster Press.
- Robert, S. (1952) *Adili na Nduguze*. London: Macmillan.
- Somba, J.N. (1969) *Alipanda Upopo na Kuvuna Tufani*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- Swingewood, A. (1975) *The Novel and Revolution*. London: The Macmillan Press Ltd.
- Tume ya Mackay (1981)

- Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix.
- Wamitila, K.W. (2006) *Kesi ya Kuchekesha*. Nairobi: Vide-Muwa.
- Wamitila, K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchangunuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-muwa Publishers.
- Wamitila, K.W. (2016) *Kamusi Pevu ya Kiswahili*. Nairobi: Vide-Muwa.
- Warah, R. (Ed) (2008). *Missionaries, mercenaries and misfits*. Central Milton Keyes: Author House.
- Warren, A. na Wellek, R. (1973) *Theory of Literature*. London: Penguin Books.
- Waruta, D.W. (2005) “Marriage and family in Contemporary African Society: Challenges in Pastoral Counseling.” Nairobi: Action Publishers.